ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3. Mhe. Omar Yussuf Mzee	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4. Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7. Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad	-	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10. Mhe. Juma Duni Haji	-	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11. Mhe. Zainab Omar Mohammed	-	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12. Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13. Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14. Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16. Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18. Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20. Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21. Mhe. Othman Masoud Othman	- Mwanasheria Mkuu
22. Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23. Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24. Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29. Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31. Ali Mzee Ali	- Kuteuliwa na Rais
32. Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
36. Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

40. Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

41. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

42. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

43. Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

44. Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

45. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

47. Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

48. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

49. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

50. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

51. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

52. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

53. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

54. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

55. Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

57. Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

58. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

61. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

62. Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

63. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

65. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

67. Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

68. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

69. Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

70. Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

72. Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

73. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

76. Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

77. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

78. Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

79. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

80. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Thalathini - Tarehe 27 Julai, 2011

(Kikao Kilianza Saa 3.00 asubuhi)

Mhe. Naibu Spika, *(Ali Abdalla Ali)* alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salimin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 206

Kutengenezwa Barabara za Ndani *(Feeder Road)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza:-

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inajitahidi kutengeneza barabara za Unguja na pemba ili kuwaondoshea usumbufu wananchi. Lakini pamoja na jitihada hizo barabara za ndani *"feeder road*" zimesahaulika kwa muda mrefu mfano wa barabara hizo ni Konde-Kipange, Konde- Gombani, Konde Matangatuwani – Kiuyu, Konde – Ungi.

Je, Mhe. Waziri ni lini barabara hizo zitashughulikiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 206 lenye kifungu kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara imekua na mpango wa kutengeneza barabara mbali mbali za Unguja na Pemba ili kuondoa usumbufu kwa wananchi, hata hivyo kipaumbele kinawekwa zaidi kwa barabara kuu.

Kwa upande wa *Feeder Road* Wizara imekuwa ikijitahidi kuzitengeneza barabara hizo kupitia program ya matengenezo ambapo fedha hizo zinazofadhiliwa na mfuko wa barabara.

Barabara ya Konde – Ungi yenye urefu wa kilomita 2.5 ipo katika mpango wa matengenezo wa mwaka 2010/2011 hivyo tunategemea kwamba itaingizwa katika *program* ya mwaka 2011/12 na itatengenezwa katika *fase one* ya *guater* ya kwanza katika mfumo wa utengenezaji wa mfuko wa barabara.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize suala moja la nyongeza.

Miongoni mwa barabara ambazo nilizozitaja Je, tunategemea zaidi kupata barabara gani, kwa sababu hizi barabara za *fielder road* ni nyingi na hujaweza kuainisha ni aina gani ya barabara ambazo tunaweza kuzisaidia, je, ni zipi miongoni mwa hizo zinaweza kusaidiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ni kweli kwamba Mhe. Muwakilishi ameeleza barabara nyingi ziliomo katika jimbo lake ambazo anaomba Wizara iendelee kumsaidia, kwa kipindi hiki kwa maana ya *quarter* ya kwanza ni barabara mbili ambazo zitajengwa, barabara ya Konde hadi Msuka na Konde hadi Ungi.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri ambayo umejibu ndani ya jimbo letu la Kikajuni tunazo barabara sabaa ambazo sasa ni mwaka wa nne mpaka na zaidi zinaendelea kuombwa siku hadi siku. Sasa je, katika mwaka huu wa fedha ni barabara ngapi za ndani ya jimbo la Kikwajuni ambazo pia zitaonekana katika bajeti yetu ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa suala halikugusa Kikwajuni. Lakini kama una uwezo mpe maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Kwa bajeti yetu hii iliyopitishwa hapa mwaka huu barabara hizo za kikwajuni hazimo katika mpango wetu, lakini hata hivyo kama tutapata fedha kutoka mfuko wa barabara hatuna sababu ya kutokumsaidia mwenzetu kwani wananchi hao wanapaswa kupata huduma hiyo ya barabara nzuri.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara yake imekuwa na utaratibu wa kutengeneza *fielder road* ziwe sambamba pamoja na barabara kuu na kwa kuwa *fielder road* ziko nyingi hapa Zanzibar na katika majimbo mbali mbali zikiwemo *fielder road* zile za Jimbo la Magomeni.

Je, Mhe. Waziri ni utaratibu gani ambao umejiwekea katika kuzitengeneza hizi *fielder road* katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri na hilo msaidie lakini halikugusa suala mama.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Utaratibu ni kwamba aidha kwa kuandika maombi kwa Wizara, kwa Mkurugenzi au kwa kuona uhalisia wenyewe wa barabara hizo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inapata nguvu tunakuwa tunatekeleza au tunasaidia katika kurekebisha barabara hizo zikiwemo hizo za *fielder road.*

Nam. 207

Kutengenezwa Kwa Kivuko na Mlima

Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa kuwajengea Skuli na Hospsitali ya kisasa wananchi wa Mkia wa Ng'ombe. Hata hivyo, wananchi hao wanakabiliwa na tatizo la kivuko cha mto pamoja na mlima mkubwa.

Je, Mhe. Waziri ni jitihada gani zitakazochukuliwa kuhakikisha kwamba watu wa Mkia wa Ng'ombe wanapata daraja iliyowekewa *"culvert"* na Mlima uliotengenezwa na kutiwa kifusi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 207 kama ifuatavyo:-

Mhe.Naibu Spika.Wizara yangu inatambua usumbufu unaowapata wananchi wa kijiji cha Mkia wa Ng'ombe kutokana na ukosefu wa daraja sehemu yanapokatisha maji ya Bahari.

Hivyo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara itaweka makalvati katika eneo hilo. Hivi sasa wataalamu wa Idara wameshaikagua sehemu hiyo na kuona kwamba makalvati ya midomo minne(4).ya mzunguko wa 90cm yanatosheleza kukidhi haja kwa huduma hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Kutokana na uchache wa fedha kwa bajeti ya mwaka huu, kazi hii itapangwa katika bajeti ya mwakani 2012-2013 kifungu cha matengenezo ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, kazi hiyo itajumuisha pamoja na kufukia makalvati hayo na pia kuuchonga na kuufukia Mlima ambao nao pia unasumbua hasa katika kipindi cha mvua. Tunamoumba Mhe. Mwakilishi ajenge imani na atupe muda kutekeleza kazi hiyo.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri aliyojibu lakini na hivyo aangalie hali halisi ya Mkiang'ombe na muda ambao ameutoa, watu wa Mkiang'ombe kwa muda mrefu wana mambo mawili katika eneo lao. Kwanza wana skuli wanajenga na vile vile kuna hospitali ambayo inatakiwa kupelekwa dawa sasa dawa zitashindikana kupelekwa kutokana na hali ya mlima na watu wa skuli watashindwa kuendeleza kutokana na hali ya ule mlima, hiyo *culvert* tunaweza kusubiri kidogo lakini mlima haiwezekani.

Sasa ningemuomba ni lini Mhe. Waziri ataweza kujenga imani kwamba tuweze kutengenezewa kabla ya kipindi ambacho amekitaja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Wizara yangu imekiri kwambwa watu wa Mkiang'ombe wanapata usumbufu kutokana na maji ya bahari kukatisha, lakini pia wizara imekiri usumbufu unaowapata kutokana na mlima ule. Kikwazo hapa ni upatikanaji wa fedha kwa mwaka huu hatuwezi kuji- *comet* kutekeleza kazi hii hatuna fedha, lakini mjenge imani

Mhe. Muwakilishi kwamba tutaendelea kuhangaika kuona kwa kiasi gani tunaendelea kuwasaidia wananchi wetu kuondoa usumbufu huu hasa kwa huduma hii ya upande wa kuchonga mlima.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri kama wananchi hao kilio chao cha muda mrefu huoni ule msemo wa kula ng'ombe mzima na kubakisha mkia ndio kilichosababisha kukosa bahati hiyo wa Mkia wa Ng'ombe. Na akama atakuwa tayari kusaidia Wizara yako itakuwaje kusaidia wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Wizara yetu haina pingamizi kikwazo chetu sisi ni fedha kama kutakuwa kuna msaada huo wa fedha tutatekeleza, lakini kama tulivyosema awali kwa mwaka huu hatuna uwezo wa kufanya hivyo isipokuwa tutarajie mwakani katika mwaka 2012/2013 ikiwa kuna mtu ambae yuko tayari kutoa msaada Wiara yetu iko tayari kutoa msaada wa vifaa, ufundi na mengineyo.

Nam. 151

Kushuka kwa kiwango cha Kufaulu

Mhe. Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Hassan Hamad Omar) - Aliuliza:-

Katika matokeo ya mitihani ya Kidato cha VI mwaka 2011, kiwango cha kufaulu kwa Skuli za Zanzibar kimeshuka sana. Kwa mfano Skuli ya Lumumba na Fiedel Castro ambazo zimewahi kuwa miongoni mwa Skuli bora Tanzani. Zina matokeo mabaya nay a kutisha ambapo Lumumba ni ya 314 na Fidel Castro ni ya 331 kati ya Skuli 334.

a) Je, Wizara yako imeyachukuliaji matokeo haya.

b) Je, Wizara imechukua hatua gani katika kuzitafuta na kuzifahamu sababu za matokeo hayo mabaya.

c) Je, Wizara ina mpango gani katika kutatua sababu za matokeo haya mabaya na kurejesha hadhi ya skuli hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 151 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifutavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Skuli za Sekondari za Zanzibar hazikufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita kwa mwaka 2010, pia ni kweli kuwa matokeo ya mtihani wa Sekondari ya Lumumba na Fidel Castro ni mabaya ambapo skuli ya Lumumba imeshika nafasi 314 na Skuli ya Fidel Castro imeshika nafasi ya 331 katika skuli 334 za Tanzania nzima zilizofanya mtihani huo huo wa taifa. Matokeo haya ni tofauti kubwa na matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne wa mwaka 2010 ambapo Skuli ya Sekondari ya Lumumba ilishika nafasi ya 17 na Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro ilishika nafasi ya 132 katika skuli 3,195 za Tanzania zilizofanya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2010 zenye watahiniwa zaidi 40. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu imesikitishwa sana na matokeo mabaya ya mtihani wa kidatu cha sita kwa Skuli za Sekondari za Zanzibar licha ya juhudi kubwa iliyochukulia kuzipatia skuli husika, vifaa mbali mbali vya kufundishia vikiwemo vitabu mbali mbali vya masomo katika ngazi hiyo.

b) Wizara imechukua juhudi ya kutafuta sababu za msingi zilizosababisha wanafunzi wengi washindwe katika mitihani ya kidato cha sita kwa kuandaa mikutano na walimu wakuu kwa pamoja, kutafakati sababu zilizopelekea wanafunzi wetu kufanya vibaya. Miongoni mwa sababu hizo ni uchache wa walimu wenye sifa za kufundisha madarasa ya sekondari ya juu hasa katika masomo ya Baiolojia, Kemia, Fizikia na Hisabati ukilinganisha na wingi wa wanafunzi walipo. Kwa mfano kwa mwaka 2010 skuli ya Sekondari ya Lumumba ilikuwa na wanafunzi wa kidatu cha sita 306 kati ya hao wanafunzi 182 walikuwa wanafundishwa somo la kemia na mwalimu mmoja tu, baada ya walimu wawili kwenda masomoni. Sababu nyengine zilizosababisha matokeo mabaya ni upungufu wa vifaa vya maabara msonamano mkubwa wa wanafunzi katika madarasa na mazingira mabaya ya skuli na dakhalia kwa wanafunzi hasa katika Skuli ya *Fidel Castro*.

c) Wizara imeandaa mipango madhubuti ya kutatua matatizo yanayozikabili skuli mbali mbali za sekondari ili ziweze kutoa elimu bora itakayowezesha wanafunzi wetu kufanya uzuri mitihani yao, miongoni mwa hatua hizo ni kufungua skuli mpya 16 katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba ambazo zitakuwa na vifaa vyote muhimu vya kufundishia na pia zitasaidia katika wanafunzi. Pia Wizara inakusudia kuajiri walimu wapya watakaomaliza masomo katika Chuo Kikuu cha Taifa cha

Zanzibar na vyuo vikuu vyengine ambao watachangia sana katika upatikanaji wa walimu wenye sifa. Vile vile, skuli zitapatiwa vifaa vya kufanyia kazi hasa kimpyuta na vifaa vya maabara. Aidha, Wizara inakusudia kupendekeza mabadiliko ya mishahara ya walimu kama ni njia mojawapo ya kuwamotisha walimu waweze kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake kasema kama hivi karibuni wana mpango wa kuajiri walimu waliomaliza Chuo Kikuu na kwa sababu tatizo zaidi linakuja kwenye masomo ya sayansi ndio wanafunzi wanafanya vibaya zaidi, sasa kati ya hao walimu watakaowaajiri wa sayansi ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Tuna mpango wa kuajiri walimu wa sayansi zaidi ya 300.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Elimu Zanzibar imeanza zamani lakini kila siku zikenda mbele watoto wetu wanafeli hasa sayansi kwa sababu ya kutokuwa na vifaa vya sayansi na walimu bora wa sayansi kama Mheshimiwa alivyoeleza.

a) Je, hatuoni kuwa Wizara ya Elimu imeshindwa kufanya kazi yake kama inavyotakiwa ili kutimiza lile lengo la kuwapa vijana wanaofaa katika kufanya kazi zetu.

b) Kama watoto wote watakuwa wanafeli sayansi na wakati kuna walimu wanaosomesha sayansi, haoni Mhe. Waziri kuwa sasa tunakwenda kinyume kabisa na dira ya dunia kuwatoa watoto wetu katika hali hii ya elimu ya sayansi na teknolojia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haijashindwa ila matatizo yanaweza kutokea wakati wowote na kwasababu matatizo tumeyaona na nimekiri kama matatizo yalikuwepo, nadhani anakumbuka ndani ya bajeti yetu ni namna gani ambavyo tulizungumza tuna nia ya kuboresha elimu katika kuajiri walimu, wakiwemo walimu wa sayansi. Lakini pia kuwa na vifaa vya maabara katika skuli zetu, sasa nadhani vitu hivyo vikipatikana basi wanafunzi wetu wa sayansi watafanya vizuri tu.

Mhe.Salma Mussa Bilal: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza suali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa ulikiri kwamba ufautu wa wanafunzi wa kitatu cha sita unashuka siku hadi siku kutokana na ukosefu wa walimu katika skuli zetu, Je, Wizara yako ina mpango gani wa haraka haraka wa kutafuta hawa walimu wenye sifa kwa ajira maalum ili kuweza kunusuru hali hii haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Wizara yangu ina mpango wa kuajiri walimu wenye sifa haraka iwezekanavyo na tayari tumeshagawa fomu karibu mia mbili (200) kwa wanafunzi ambao mwaka huu wanamaliza vyuoni.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi, ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuna wachangiaji sita kwa hivyo tutumie muda vizuri ili tuweze kumwita Waziri kwa muda mzuri vile vile.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kutukutanisha hapa tukiwa wazima kabisa na wenye afya njema katika kuzungumzia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri kwa kazi ambayo wamepewa ya kuleta au kuhuisha maslahi ya Wazanzibari katika masuala ya kuendeleza biashara na viwanda pamoja na masoko yake, mimi kwanza nilikuwa nataka nije na tafsiri ya hii Wizara hasa, tafsiri ya wizara inasema biashara Viwanda na Masoko na jina hili ni jna asili kwa uchuji wa Zanzibar, historia inatueleza kwamba uchumi wa Zanzibar katika miaka mingi ulikuwa ukitegemea zaidi masuala ya biashara na Zanzibar ilikuwa ni kituo cha biashara katika nchi za Afrika ya Mashariki. Kwa hivyo wizara hii ina kazi kubwa ya kuendeleza ile historia ambayo imeachwa na wazee wetu ambao wamepita.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nije na suala zima kwanza niaze na biashara hii ni sekta mtambuka unapozungumza biashara unazungumzia suala la kilimo, uvuvi na mambo mengine yote yanaingia katika suala zima la biashara, lakini

biashara Zanzibar sasa hivi inaonyesha imekubwa na msuko suko mkubwa sana na msuko suko wa biashara wa Zanzibar Mhe. Spika, uko katika maumbile ya visiwa vyetu vya Zanzibar ardhi tuliyokuwa nayo haitoshelezi kwa Wazanzibari kuweza kujitosheleza kwa chakula vile vile kwa kilimo cha biashara. Kwa hivyo ndio maana wananchi wengi wa Zanzibar wakawa wanajihusisha zaidi katika masuala ya biashara na baadhi yao wakawa wanajishughulisha na masuala ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, biashara Zanzibar ina changamoto kwa jambo kubwa ambalo kila siku imekuwa katika midogo yetu, ni mashuhuda kwamba Zanzibar katika miaka ya 1995/2000 Zanzibar ilikuwa imepiga hatua nzuri kidogo kibiashara, ingawa biashara zenyewe zilikuwa sio za ndani sana zilikuwa ni kama *transit* zinatoka nje zinaingia Zanzibar zinapelekwa upande wa pili wa muungano, nyengine zinavuka mpaka katika nchi ya jirani. Lakini Mhe, Naibu Spika, tukitaka tusitake tatizo la *TRA* kwa Zanzibar linachangia sana kudumaza biashara Zanzibar sote sisi mashahidi ilikuwa ikifika kipindi kama hichi cha kukaribia Mwezi wa Ramadhani ukienda pale Darajani utakuta harakati za wananchi, vijana wetu wanafunga mizigo kupeleka upande wa pili wa Muungano wengine wanapeleka Zambia, wengine wanapeleka Ruanda, Burundi kila sehemu. Lakini kutokana na matatizo ya *TRA* biashara ile sasa hivi imekufa kabisa.

Mhe. Spika, hata ukiangalie hii nakisi ya uagiziaji bidhaa baina ya kusafirisha bara na Zanzibar nakisi hii kila siku inakuwa inaongezeka kwa sababu sisi tunakuwa tunasafirisha kidogo, sote mashuhuda wenzetu kutoka Bara walikuwa wanakuja kununua bidhaa hapa Zanzibar lakini sasa hivi mambo yamegeuka sisi Zanzibar tunatoka hapa kwenda kununua bidhaa Tanzania Bara. Bora tungekuwa tunanunua bidhaa zinazozalishwa pale Tanzania Bara lakini tunanunua bidhaa ambazo zinazalishwa nje ya nchi tunakuja kuuza hapa kwetu Zanzibar, kwa hivyo ndio maana unakuta sasa hivi bei za bidhaa hapa Zanzibar zinakuwa juu ukilinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, ukiacha bidhaa za nguo tuje vifaa vya ujenzi sasa hivi vifaa vya ujenzi wafanya biashara wananunua kutoka bara wanaleta hapa Zanzibar, tujiulize nini tatizo kama hatujarekebisha matatizo katika suala zima la *TRA* hapa Mhe. Naibu Spika, bado Wazanzibari wataendelea kupata tabu katika kusimamia na kuendeleza biashara katika kuinua maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nilikuwa nafuatilia sana mikutano ya kampeni ya Mhe. Rais, alikuwa anaeleza wazi wazi kwamba atahakikisha anaboresha zao la karafuu. Lakini vile vile ataangalia maslahi ya wakulima wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, Rais wa Zanzibar alipolizindua Baraza tukufu la Wawakilishi alizungumza wazi wazi katika hotuba yake. Atahakikisha kwamba karafuu, wakulima wa karafuu na maslahi ya wanaolima karafuu na waohudumia karafuu atawaimarisha.

Mhe. Naibu Spika, tunashukuru na tunaomba sana waheshimiwa mawaziri wafate nyayo za Mhe. Rais. Mhe. Rais analolizungumza analitekeleza. Mwaka mmoja haujafika tokea kutamka kauli zake hizo, leo tumemsikia Mhe. Waziri wa Biashara anakuja kutueleza hadharani kwamba bei ya karafuu imezidi tena imazidi mara mbili.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nilikuwa naomba kitu kimoja. Kwanza sisi wenyewe kama Wazanzibari visiwa viwili Unguja na Pemba. Sisi hatukuungana, sisi ni nchi moja visiwa viwili, hetu sasa hivi tuanza kuimarisha zao letu la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi suala la karafuu lilikuwa linasemwa magendo, karafuu zilikuwa hazisafirishwi kwa magendo, watu walikuwa wanasafirisha tu, maana magendo alau ujifiche. Lakini karafuu zilikuwa zinasafirishwa kwa makusudi na wanaosafirisha karafuu ni Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata bahati kutembelea Mombasa kule Shimoni, kipindi kile ilipokuwa jahazi ilipozama na Wazanzibari baadhi yao wakafariki. Tukatumwa sisi kwenda kushughulikia maiti za Wazanzibari. Katika Bandari ya Shimoni pale sisi baada ya kufika tu tulipata *information* zote za karafuu, wanaosafirisha karafuu, wanaopokea, madalali, ma-*agent*. Tukaambiwa hapa hebu subiri ikifika kuanzia saa 8-12 zitaingia jahazi si chini ya tano. Mhe. Mugheri bahati mbaya hayupo hapa .

Mhe. Naibu Spika, kuanzia saa 8-12 zinaingia mashua tano za karafuu zimejaa shehena. Hamna Mkenya, hamna Mtanzania Bara, hamna Mganda. Wazanzibari wenyewe, watu anapigiana simu itaingia saa ngapi. Wenzetu kule Kenye karafuu sio agendo wale ile biashara sio kwa wao ni haramu, kwao wao ni halali. Kwa hiyo ikifika pale inapokelewa na Forodha, wanakwenda wana *record*, wanalipa kodi pale, kila kitu mpaka wale wachukuzi wanaobeba magunia ya karafuu kutoka kwenye zile mashua ni Wazanzibari. Tulikuwa tunajiumiza wenyewe kwa wenyewe. Sasa hivi kutokana na maslahi bora yaliyowekwa katika karafuu. Mimi nadhani hebu tuweke mkakati maalum.

Mhe. Naibu Spika, suala la wanaosafisha karafuu lilikuwa wala sio tatizo kubwa maana unakwenda pale unakwenda na nyavu, unawateka basi. Kwa sababu walikuwa hawajifichi. Mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, suala

hili tulishughulikie. Lakini vile vile nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wenzetu ZSTC suala la bei ya karafuu ingelikuwa imepanda zamani. Kwa sababu walikuwa wanazungumza lakini tulikuwa hatuwasikilizi.

Mhe. Naibu Spika, karafuu zinamsimu wake wa kuuza. Pale karafuu zinapovunwa hasa Zanzibar bei inakuwa inashuka. Ikishakumaliza kuvunwa ikikaa miezi miwili au mitatu bei inakuwa inashuka. Ikishamaliza kuvunwa karafuu ikikaa miezi miwili au mitatu, bei inapanda. Tatizo ZSTC tulikuwa hatujawawezesha kuwa na mtaji mkubwa kuweza kununulia zile karafuu kwa wakati. Pesa walizokuwa wananunulia ZSTC walikuwa wanakopa Benki, wakishakukopa Benki *deposit* milioni 50 hazirudi, mbali pesa wanazokopa kuna riba. Ina maana ile gharama yote baadaye wanakuja kumtwika mkulima. Ndio maana bei ilikuwa haipandi.

Mhe. Naibu Spika, lakini sasa hivi nashukuru kwa kuwa sasa hivi serikali imeamua kuwawezesha *ZSTC* na tumeona hapa mnataka kuboresha katika kuboresha msije mkawafukuza hawa, kwa sababu wanao uwezo. Tusije tukatafuta ndugu zetu tukawaweka pale wale tukawaona walikuwa hawafai. Mheshimiwa walikuwa wanafaa, maarifa walikuwa wanayo mazuri, kwa hiyo waendelee kuwepo, tuwape nyenzo wafanye kazi.

Mhe. Naibu Spika, tuliwahi kushauri, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha baadaye ndio nikamrithisha swahibu wangu Mhe. Salmin. Tuliishauri sana serikali, tuiwezeshe tuangalie matatizo yao, tuwape mtaji, tuwape muda. Mbona *PBZ* ilipokuwa inakaribia kufilisika ikawezeshwa na serikali, ikalipwa na serikali, ikapewa mtaji, mbona sasa hivi *PBZ* wanajiendesha kwa faida. Ina maana *ZSTC* hatukuwapa nafasi.

Mhe.Naibu Spika, kutokana na muda sitaki niseme sana lakini nadhani Mhe. Waziri amenielewa. Kwa bahari nzuri mpaka Naibu Waziri alikuwa mjumbe wangu wa Kamati. Kwa hiyo anajua vizuri namna gani tulivyokuwa *ZSTC* walivyokuwa wana uwezo wa kuweza kushughulikia zao la Karafuu na kuweza kuinua bei. Kwa hiyo naamini hawato watimua isipokuwa watawapa nyenzo ya kwa ajili ya kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye suala la maonyesho. Mimi naomba kitu kimoja, hebu tungekuwa na wataalamu. Wataalamu tunao ingawa siku hizi wanakimbia wanakuja kwenye siasa. Tunao wataalamu kina Mhe. Shamuhuna, kina Mhe. Omar Yussuf hao wataalamu wazuri sana kutokana na hali ngumu wataalamu hatuwashughulikii wanaamua kuja kubanana kwenye siasa humu.

Mhe. Naibu Spika, hebu tuwe na mkakati maalum. Mhe. Shamhuna alikuwa Waziri wa Mipango na Kitega Uchumi kipindi hicho, katibu wake Mkuu

alikuwa Mhe. Omar Ali Yussuf, watu wa mipango kweli kweli. Naamini sasa hivi tutakwenda vizuri, kwa sababu hawa ni watu ambao akili zao ziko makini, zinafanya kazi, na zinaona mbali. Dk. Mwinyi na yeye pia mtaalamu na hawa waliokuwepo hapa mbele wote wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, nazungumzia suala la maonyesho. Kwanini nikasema maonyesho? Suala la monyesho lilikuwepo na likatengwa eneo la mabanda ya maonyesho. Lakini ghafla rafiki yangu leo hayupo Mhe. Harouna, kalichukua Chuo Kikuu. Mheshimiwa hii mipango ni lazima iwe endelevu. Hii mipango wakati mwengine tusiitie mikono mikono. Sisi wana siasa tuje na mambo yetu lakini wataalamu wakishatupangia mambo ya kiuchumi tuachie iendelee. Eneo la Tunguu lilikuwa ni eneo zuri sana kwa ajili ya maonyesho ya Zanzibar. lilijengwa pale ukapelekwa umeme haraka haraka, barabara ipo lakini leo ghafla tukaja tukabadilisha tukaweka Chuo Kikuu. Ndio tumefanya maamuzi lakini pale kwa suala la Chuo Kikuu si pazuri sana. Chuo Kikuu kinatakiwa kiwe pahala faragha. Leo Chuo Kikuu kipo barabarani, Pembeni kote kumegaiwa viwanja, watu pale watasoma vipi pale.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani hili ndio tatizo letu kwamba hatuna ile strategic hasa za kiuchumi kwamba Zanzibar ili itoke katika umasikini iende huku kwenye mipango hii. Kwa hiyo ina maana kiongozi yoyote atakaekuja mule hamtiwi mikono bali anaimarisha tu. Mhe. Mwenyekiti, nayakubali sana mawazo ya Mhe. Waziri kuanzisha tena eneo la maonyesho ya biashara. Lakini kama nilivyosema yale mambo mengine ya kizamani ambayo yalipangwa tusiyatupe.

Mhe. Naibu Spika, bado nipo kwenye maonyesho lakini maonyesho ya sabasaba. Kwanza tunashukuru wizara imejitahidi kwa muda mrefu kuhamasisha wafanyabiashara wetu na kuwapa taaluma mpaka sasa wanaingia katika masoko ya maonyesho ya biashara ya tualii. Pale Dar-es-Salaam katika kitabu hiki Mhe. Waziri nitaomba aje anipe ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki wameeleza kwamba wafanyabiashara karibu mabanda 50 wamekwenda katika maonyesho. Lakini kwa taarifa tulizonazo ni kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar ni 47. Hapa nilikuwa nataka ufafanuzi, kwa sababu pale kuna fedha ambazo zimeahidiwa na humu Mhe. Waziri nashukuru amezitaja na Mhe. Raisi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete.

Kwanza tunampongeza kwa kuwajali Wazanzibari. Katika mabanda yao alikwenda na akayaona na akakagua. Kutokana na kuvutiwa kwake, lakini vile vile akahisi bado hawa watu wako duni kimtaji, aliamua kuchangia shilingi milioni 200 ahadi. Lakini tunaamini ahadi za Mhe. Raisi hazikawii sana. Hapa

Mhe. Waziri alisema zinamipango mingi lakini mimi nilikuwa nina ushauri. Kwa saabu hawa wafanyabiashara safari hii walipata tabu sana katika kwenda kwenye maonyesho. Wao walichangiwa Shs 13,000/- nadhani na Wizara ya Uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara hawa kwa sababu wamo majimboni kwetu. Kila wanaposafiri virungu mfululizo, lakini virungu vyao vya faida kwa sababu wanakwenda kujitegemea. Katika hizi pesa shilingi milioni 200 nilikuwa naomba, kwa sababu nimeshaona zimepangiwa mipango mingi na Mhe. Waziri. Nilikuwa naomba nusu yake wale waliokwenda kwenye maonyesho wagaiwe wao, ili kuja kuongeza mtaji wa zile biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, hayo maonyesho mnayoyaona yanakwenda kule, yale matayarisho yake basi kupitia kwa wabunge na wawakilishi sio mitaji yao. Wabunge na Wawakilishi ndio wanaohamasisha, ndio wanaowezesha zile biashara mnazoziona kule, sio mitaji yao. Sasa hichi kitu kidogo, kwa sababu hapa imeelezwa zitakuja kuwasaidia wajasiri amali wote wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, milioni 200 wajasiri amali wote wa Zanzibar, leo tumeshatoa mikopo ya AK na JK zaidi ya bilioni moja watu wanalalamika hatujapata pesa hazijatosha. Je leo milioni mia 200 ukijaukianza kuzitafutia wajasiri amali wengine huko mitaani. Mimi nadhani tungeliwatendea haki wale waliokwenda kwenye maonyesho ili hizi fedha wakapewa nusu yake wakagawana na hata wakishakugawana kwani nyingi, sijui milioni tano tano. Pesa yenyewe hata yeye mwenyewe Mhe. Mazrui anaweza akatoa akawagaiya tu, milioni 200 sio pesa nyingi. Lakini tuwawezeshe ili wajenge imani na ule utaalamu wao walioupata kule. Wengine wamepata mafunzo kule lakini mtaji hawana, sasa watapelekea nini.

Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, hili nilikuwa naliomba sana. Mhe. Waziri nafikiri kanisikia na naamini anatalishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, matatizo ya viwanda Zanzibar yana mambo mengi, kuna baadhi yao Mhe. Waziri humu hakueleza. Moja katika suala ambalo lilikuwa linachangia viwanda kufa ni masoko. Ndio maana hii wizara yake inasomeka Wizara ya Viwanda na Masoko. Kwa sababu ukiwa na kiwanda kama huna soko, kitakufa. Mheshimiwa Mjumbe wangu hapa wa kamati yangu Mhe. Mohammed jana kazungumza vizuri. Tulikuwa tuna viwanda hapa vya Sigara Zaraha na Zakuchuja. Sigara hizi zilikuwa zinapendwa sana na wenzetu upande wa pili wa Muungano, kwa sababu ukiivuta ile unasinzia baridiiii.

Mhe. Mwenyekiti, ilifika pahala sigara zile zinasafirishwa zikifika Dar-es-Salaam mwezi mzima ziko Bandarini zinasokotwa, sijui hivi. Matokeo yake wakenda wakashindwa soko kule wakarudi hapa, viwanda vinakufa.

Lakini kuna kiwanda pale Maeneo Huru Amani, pale kulikuwa na kiwanda cha kutengeneza madirisha na milango ya viyoo ya aluminium. Mhe. Mwenyekiti, wale walikuwa wanatengeneza vifaa vya aluminium utafikiri labda vinatoka Ulaya. Wenzetu walipokuwa wanasafirisha kupeleka Bara vinakaa bandarini vifaa vyao miezi miwili. Wanaambiwa mmedanganya hivi vifaa havitoki Zanzibar vinatoka Indonesia, sijui vinatoka wapi. Kwa hiyo matatizo yaliyouwa viwanda ni mengi. Lakini Mhe. Waziri humu hakuyasema anaona haya. Usione haya Mheshimiwa sema tu.

Jengine lililouwa viwanda Zanzibar wizi, humu haukutajwa, viwanda walikuwa vinaibiwa sana. Tulikuwa tuna kiwanda cha *Cotex* pale na labda Mhe. Waziri atakuja kunieleza vile viwanda vya *Cotex* lakini na Mhe. Waziri wa Fedha baadaye na yeye atakuja kutueleza. Vile viwanda pale vinafanya nini au wametuwekea makuta tu sasa hivi. Tunataka sasa hivi rasilimali zote za Zanzibar zitumike ili wananchi waneemeke. Sasa hivi pale pamebakia magofu tu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa kumalizia nilikuwa nataka nitoe ushauri. Mwaka huu mnatubinya kwa sababu bajeti hii ndio tunazungumza Wazanzibari wataishi vipi na watakula nini. leo dakika mnazotupa zinakuwa kidogo mpaka kanuni zetu tunazikiuka.

Mhe. Naibu Spika: Dakika 20 nimekupa za kawaida.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, lakini tuwe na dakika za kukopeshwa, mambo ni mengi. Nilikuwa naomba sana baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura, tunaiyunga mkono hotuba hii hasa baada ya kupata maelezo ya wafanyabiashara wa saba saba, kwa sababu miongoni mwao wamo wananchi wa jimbo langu la Kwamtipura walionileta hapa. Ndio maana hapa nina asilimia 80 asili 20 zipo kwa Mtipura. Naamini zitapatikana ili tuweke asilimia mia juu ya mia. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Naomba wajumbe niwape taarifa kwamba tumetembelewa na wageni wa Chuo Kikuu *SUZA* wanafunzi, wamekuja kusikiliza michangio. Tunaomba wasimame tuwaone. Ahsante kaeni.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, nitaenda haraka hara ili usinikopeshe dakika.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yake ya watendaji, wakiongozwa na Katibu Mkuu ndugu Rafael na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na hatimaye kuja na hotuba nzuri hii ambayo Mhe. Waziri ameiwasilisha hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia niipongeze Wizara kwa kupita kiwango cha ukusanyaji wa mapato ambacho wizara ilijipangia na kukusanya ongezeko la asilimia 22 ya lengo lililowekwa.

Pili naomba niipongeze serikali kupitia wizara hii kwa ongezeko la bei ya karafuu lakini hasa nimpongeze Mhe. Rais kwa kutekeleza yale ambayo tuliyowaahidi wananchi wakati tunaomba ridhaa. Sambamba na uongezekaji wa bei ya karafuu namuomba Mhe. Waziri pamoja na timu yake ajitahidi sana na udhibiti wa magendo. Pia wizara inone haja ya kuzingatia bei ya vibarua, wakati Mhe. Hija jana akichangia alimuomba Mhe. Waziri aweke angalau muongozo kwa wale matajiri wenye mikarafuu ili na vibarua na wao wafaidike na bei hii ambayo imepanda.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri pamoja na bei ya vibarua pia aangalie fidia kwa wale wanaoanguka wakati wa kuchuma karafuu. Lakini pia niipongeze serikali kwa kuanzishwaji wa mfuko wa karafuu. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija atutolee ufafanuzi juu ya deni la serikali kwa *ZSTC* vipi, limefikia wapi, limekwisha au limekwenda wapi?

Mheshimiwa nikiachana na karafuu nilikuwa naomba kidogo nichangie kuhusu zao la mwani. Jana Mhe. Panya wakati anachangia alisema kwamba kule Kaskazini kunakina mama wengi ambao wanatanda dagaa. Lakini mimi nasema kule Kusini kuna akina mama wengi ambao wanapanda zao hili la mwani. Kwa hiyo Mhe. Waziri nilikuwa namuomba kwamba alipe kipa umbele zao hili kwa sababu ni ajira kubwa ya wanawake kule vijijini. Kwa hiyo nilikuwa namuomba angalau awasaidie zao hili nalo liwe na tija kwao. Sambamba na hilo nilikuwa naiyomba Wizara pia isimamie bei za bidhaa hususan za kula na mafuta na hasa tunakoelekea katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri asimamie suala la wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanauza bidhaa mikononi kama maziwa ya makopo na tambi za macron hasa hapa eneo la Darajani. Watu wale wanauza vyakula ambavyo vipo *out dated* au *expired*.

Wakati napitia malengo ya utekelezaji ya Wizara katika mwaka 2011/2012 nimeona kula lengo la kuanza utekelezaji wa Sheria ya Viwango yani (*ZBA*).

Nilikuwa namuomba Waziri aharakishe utekelezaji wa sheria hii ii wananchi waepukane na matatizo ya kuuziwa bidhaa zilizokuwa hazina ubora.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, mimi kwa ufahamu wangu najua Baraza la Biashara lipo chini ya Wizara hii. Lakini katika hotuba hii yote ya Mhe. Waziri sikuona popote ambapo ameongelea kuhusu hili Baraza la Biashara. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija atwambie *progress* ya Baraza hili limefanya nini au linajipanga kufanya nini.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii fupi kwa kuchangia hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012 ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko. Moja kwa moja nianze kwa Shrika la biashara, Shirika la Magari kama lilivyoelezwa katika ukurasa wa 58.

Mhe. Naibu Spika, shirika hili lilikuwa likifanya kazi vizuri hapa mwanzo. Likinunua magari na vyombo vyengine vya moto na alhamdulilah wakiuziwa wananchi kwa bei nafuu na walikuwa wanawakopesha. Lakini kwa mujibu kitabu kinavyoeleza ni kuwa shirika limekosa sana mtaji na uwezo wake ni mdogo na limeingiwa na ushindani, hivi sasa limo katika utaratibu wa kutaka kufungwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwa ushauri wangu mimi binafsi ningeliomba hili shirika lisifungwe lakini badala yake liimarishwe ili tuweze kufaidika nalo. Nasema hivyo kwa sababu ya kimsingi.

Mhe. Naibu Spika, tuna Shirika la Meli, limepewa meli na serikali na siku zote meli zile humalizika, hufa na huwa hazifanyi kazi tena. Kila siku tukisema hili Shirika lifungwe halisaidii chochote, lakini serikali inakataa. Naomba kujua ni kwa nini Shirika la Meli ambalo hatuoni tija yake inayofanywa, linaimarishwa na hili la magari lenye faida zaidi linafungwa.

Hilo ni moja la pili hatuwezi kuendelea bila ya kuwa na viwanda. Nchi hii kwa makusudi kulikuwa kuna viwanda chungumzima ambayo ilikuwa ikizalisha bidhaa viwandani na sote tukifaidika na baadhi ya bidhaa zikiuzwa nje na kupata fedha za kigeni. Tulikuwa tunaviwanda kwa mfano kiwanda cha Sukari, kiwanda cha viatu, kiwanda cha sigara, viwanda vidogo vidogo na hata kiwanda cha nguo, vyote hivyo vimekufa na bado katika wizara imo viwanda.

Mimi ningeliomba kwanza Mhe. Waziri hasa atueleze sababu ilikuwaje wakati hivi viwanda vilijengwa hapa kwa manufaa yetu kwa makusudi kabisa kukuza uchumi, vikaachiwa vikafa kimoja kimoja vyote wala hakuna hata kimoja

kinachoendelea. Kulikwua kuna sababu gani? Hivi sasa wamejipanga vipi katika kuendeleza viwanda vyengine ili visije vikatokewa na kama vile vilivyokuja. Lakini kwanza tupate sababu.

Hapo hapo naomba Mhe. Naibu Spika, kuwa kiwanda cha Sukari ni kiwanda muhimu sana, kilishughulikiwa na tukasikia kuwa tayari wameshajitokeza watu kukiendesha na ni muda mrefu hivi sasa. Lakini mpaka hivi sasa hatuoni chochote. Kwa hivyo Mhe. Waziri haoni kuwa upo umuhimu kama hao wawekezaji wameshindwa serikali ikachukua tena kiwanda hichi na kukishughulikia tukanufaika zaidi kuliko kukiacha kikafa moja kwa moja kwa kutegemea kufungua viwanda vyengine. Na ni kipi kiwanda zaidi ya hichi cha sukari kitakachofanywa ili tufaidike?

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu kama tunavyoona ni nchi ambayo imezungukwa na bahari na ni nchi yenye mazao mengi sana baharini. Kwa makusudi naomba Mheshimiwa katika hivyo viwanda ambavyo amevipigia macho aone kuwa tumefaitika na kupata kiwanda cha kusindikia minofu ya samaki ambayo nina hakikisha kuwa mali ghafi hii itakuwa ni yetu wenyewe haina gharama ya kununua popote na sisi tutaweza kufaidika.

Mhe. Naibu Spika, nizungumze kuhusu zao la karafuu. Naipongeza Serikali tena naipongeza sana kwa kuona imeongeza bei ya zao hili la karafuu katika kiwango ambacho mimi mwenyewe sikitarajii. Hapa kidogo naomba nizungumze kama hivi inavyofuata.

Mhe. Naibu Spika, kwanza karafuu muuzaji apate haki yake. Mizani zinazotumiwa ni mizani nyengine labda niseme ni kabla ya Mapinduzi. Mizani zinazotumiwa hazina sura hawa ya kuwa ndio mizani za kutumiwa. Tatizo linalotokea moja ni kuwa watu wanapimiwa karafuu zao na wataalamu wanajua pishi moja ya karafuu kavu ni kilo moja na nusu lakini kila wanapokwenda karafuu zao wanakatwa na kuibiwa pesa nyingi sana.

Ushauri wangu ili mali iingie serikalini kama tulivyokusudia ni kuhakikisha kuwa muuzaji kapata haki yake. Mimi binafsi sitoridhika kuona kuwa mizani zile kwa vile zilivyo zitaendelea kutumika tena. Ushauri wangu zitafutwe mizani mpya kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba tuahirishe kikao kwa muda mpaka umeme utakaporejea.

Kikao Kiliahirishwa Kwa Muda Kutokana na Kukatika Kwa Umeme

Muda Mfupi Baadae Kikao Kilirejea

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia kuhusu mizani. Kwa hivyo, naomba mizani hizi kama nilivyosema tokea kabla ya Mapinduzi, mizani za tokea enzi ya Sayyid Barakhash ziondoke na tutafute mezani zinazofaa.

Mhe. Naibu Spika, halafu kuhusu bei, kama nilivyosema na nashukuru katika kutafuta habari tumeambiwa kuwa safari hii pamoja na karafuu kuwa juu kama nilivyoeleza na shukurani zangu nazidi kuzitoa, ni kuwa hapana mkulima atakayekwenda kuuza karafuu zake akaikopesha serikali, yaani fedha ziko za kutosha kwa kununua karafuu zote. Hili nashukuru sana na halafu tuna taarifa kuwa bei ikizidi kupanda duniani na huku karafuu zinapandishwa bei na haziteremki tena, hii ni neema kwetu.

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo kwa sababu na mimi hupenda kuelezwa naomba ufafanuzi kidogo. Ni kwamba tunavyojua kuwa serikali yetu haina fedha ya kutosha na kuna wizara zimepata makisio hata asilimia 12.1 ya matarajio waliyoweka wenyewao. Hii pesa yote ya karafuu imepatikana wapi? Kama kuna mwekezaji tayari wa kununua karafuu amejitokeza tujue na kama ni wengi tujue ni viwango gani vilivyotumika mpaka akachukuliwa huyo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika karafuu naomba vile vituo ambavyo zamani vilikuwepo vya kununulia karafuu na vikavunjwa baadaye basi virejeshwe ili wakulima wapate urahisi wa kuuza zao hili. Mhe. Naibu Spika, nikiendelea ni kuwa tuna shamba la Mtakata ambalo *ZSTC* inalitumia kwa kupanda miti ya aina kwa aina mikaratusi ya mafuta, mikaratusi ya dawa pamoja na miti mengine na pale penye kiwanda wanatoa mafuta na mafuta yale wanauza kupelekea nje. Sijui hivi sasa lakini nataka kuelezwa ni kuwa zamani shamba lile mpaka tulipotembelea lilikuwa bado wanakodishwa na walikuwa wakilipa fedha za kigeni. Kwa sababu shamba lile ni la serikali kwa nini Mhe. Waziri haoni kuwa ipo haja hivi sasa ya kuona kuwa shamba lile limekabidhiwa *ZSTC* moja kwa moja ili waendelee na upandaji wa miti na uzalishaji wa bidhaa ambazo wanauza nje na kuingiza fedha katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kuwa siku zote katika biashara tunahitaji faida na faida tunaipata kutokana na kipato tunachochukua, biashara zetu zote hapa tuna vituo viwili vikubwa vya kukusanya kodi. Kuna *TRA* na *ZRB* katika nchi hii

moja na biashara kubwa kama vile ya magari na kadhalika *TRA* ndio wanaohusika. Mhe. Naibu Spika, mimi nauliza kwa sababu hii ni nchi tuna serikali yetu na tunajitafutia mapato kwa kuendesha nchi hii kwa manufaa ya nchi yetu na tumo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni lazima sasa tuoneshe mabadiliko ya kweli katika kukuza hali za kijamii. Ni kwamba kuna ulazima gani wa *TRA* kukusanya kodi hapa Zanzibar au ni kwa sababu *ZRB* hawana utaalamu wa kukusanya kodi hiyo, na ikiwa hawana kwa nini haifanywi mpaka ikaonekana kuwa fedha za Zanzibar zinakusanywa na *ZRB* na hizo ambazo zitaalamika kwenda huko *TRA* zitoke kwenye *ZRB* na isiwe vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hakuna kitu kikubwa kama hasara naamini serikali yetu inajitahidi mwisho wa uhodari wake kuona kuwa hali ya nchi inabadilika kimaendeleo. Lakini kuna mambo kama hatukuyaepuka hata tukajitahidi vipi siku zote itakuwa hali yetu itabakia chini.

Mhe. Naibu Spika, siingilii katika wizara lakini mimi naona adui wetu mkubwa sana anayetupa mashaka katika nchi hii ni umeme. Hivi sasa tunadaiwa bilioni 50 na Serikali ya Muungano inasema kuwa hawasemehe deni hili kwani ni kubwa sana kwetu sisi. Kwa hivyo, ili kama watataka tuendelee ni lazima tujitegemee kwa nini Mhe. Waziri hashauriani na mheshimiwa anayehusika wakafanya kila inavyowezekana kwa kuishauri serikali kuona kuwa Zanzibar kwa vile inataka kuwa nchi ya viwanda inataka iendelee na iwe inajitegemea kwa umeme wake mwenyewe badala ya kutumia umeme ambao malipo yake hatuyamudu. Sisi itakuwa kazi yetu hapa ni kuchumia umeme tu sio kuchuma kwa kunuwafaisha wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ni suala la mwani najua akina mama wetu wanajitahidi sana na biashara hii na biashara hii wanaifanyia kazi katika mazingira magumu sana. Naishukuru serikali kwa kuondoa utata wa zao la karafuu mpaka wakaona njia ya kupita ili wananchi wafaidike kwa uongezaji wa bei. Mhe. Naibu Spika, na yule mtu wa kati kati naye amewasiliana kule kunakonunuliwa karafuu moja kwa moja kwa hiyo hapa bei Alhamdulilahi ilipanda juu. Lakini mwani mpaka hivi sasa kwa taarifa zako ni kuwa kuna watu wanakuja wenyewao wanatia bei wanaotaka wenyewe na ndivyo wanavyonunua na tunasikia kwamba huenda pengine wakafika mpaka shilingi mia nne kwa kilo kwa kazi ya mwani kwani bei ingali fedha ni ndogo sana.

Mhe. Naibu Spika, tunasikia sasa kuwa mwani duniani unanunuliwa kwa shilingi 2500 kwa hivyo ni lazima mnunuzi amjali mkulima kwa hiyo ningeliomba ile *formula* inayotumiwa mpaka bei ya karafuu ikaweza kuongezeka vile vile itumiwe kwa mwani pamoja na biashara nyengine hasa kwa sababu Shirika la *ZSTC* limejitoa katika kutafuta bei ili wananchi wafaidike. Kwa hivyo, serikali naiomba sasa itafute hii njia ambayo

yakuwasilianana wale wanaohusika moja kwa moja badala ya kuleta mtu hapa ikawa siku zote anatuangusha.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mimi nashukuru sana.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema na uhai asubuhi ya leo, lakini pili mheshimiwa nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kuwapongeza kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri na watendaji wao kwa jinsi wanavyojitahidi katika kuchapa kazi na katika kujenga dhamira ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mchango wangu nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, waswahili wana msemo wanasema haja ya mja kunena muungwana ni kitendo. Mhe. Naibu Spika, pongezi hizi natoa kwa sababu Mhe. Rais wetu ameanza kuonesha kwa vitendo kauli zake, alikuwa akitoa kauli tangu wakati wa kampeni mpaka baada ya kampeni katika maeneo mbali mbali kwamba moja katika mambo ambayo atasimamia ni kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kuondokana na umasikini. Nalo hili limeonekana kwa vitendo baada ya kuwasaidia wakulima wetu wa karafuu kwa kuweza kuwapandisha bei ya zao hilo la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu wa pili nilikuwa naomba kuchangia suala la wafanyabiashara. Hapa naomba nieleweke sana kwani napata kigugumizi kwa sababu biashara ina taaswira mbili, mwanzo ni wafanyabiashara wa jumla na pili ni wanyabiashara wa reja reja. Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi kirefu tunapiga kelele jinsi ya baadhi ya vyakula kuuzwa kwa bei ya juu wakati duniani tunaambiwa biashara hizi ziko chini.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba pana tatizo na nimuombe sana Mhe. Waziri katika hili aanze kulifuatilia, aanze kulifanyia uchunguzi wale wafanyabiashara ambao wanapewa vibali vya kuingiza bidhaa nchini inasemekana kuna mtindo wa wao kwenda katika ile njia ambayo zamani tulikuwa tunasema njia ya unyonyaji. Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwauzia biashara wadogo wadogo kuna mtindo wa watu kujitokeza kati kati wanafanya wao kuwa wajanja na baadaye biashara ile kuipandisha bei hata ikifika kwa mtu wa chini unakuta lengo na dhamira ya kuwasaidia wananchi halipo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mchele unapoingia bandarini tu basi mfanyabiashara aliyepewa kibali cha kuingiza mchele ule baada ya kwenda kuwauzia wafanyabiashara wa reja reja anaanza kumuuzia mfanyabiashara mwengine kwa bei ya 40,000 na mfanyabiashara yule anamuuzia mtu mwengine kwa bei ya 45,000 hata ukifika chini basi mchele ule unakuta mwananchi wa kawaida anaununua kwa bei ya juu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri utaratibu wa vibali wanavyovitoa vina utaratibu gani kwa wafanyabiashara wetu kwa sababu hili inaonekana bado ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nilikuwa naomba nimuulize Mhe. Waziri anisaidie atakapokuja kutoa majumuisho yake hapa, kuna maghala ya akiba ya Saateni, maghala haya kwa nia njema tu serikali yaliyaweka ili kuweka akiba za vyakula kwa wananchi wake. Kwa hivyo, naomba aje anieleze kwamba yale maghala sasa hivi yako mikononi kwa nani, yamekodishwa, yameuzwa na kama yamekodishwa au yameuzwa umefuatwa utaratibu gani kwa sababu kuna mashaka.

Mhe. Naibu Spika, mashaka yetu ni kwamba yale maghala yalikuwa kwa ajili ya kuweka akiba ya vyakula, lakini sasa hivi maghala yale yanatumiwa katika njia ambazo hazistahiki sijui kama mikataba wale waliopewa ndio inaruhusu kuyatumia katika njia ile wengine wamefanya gereji, wengine wameweka saruji, wengine kuna maeneo wameshaanza kubadilisha muundo wameeanza kuweka hospitali. Kwa hivyo, hili namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anisaidie majibu ili na mimi nijitosheleze pamoja na wananchi wangu kujua namna ya maghala yale yalivyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa naomba nichangie kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa eneo la Maruhubi. Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza wafanyabiashara basi kuna nyanja nyingi, kuna wanaofanya biashara kubwa, kuna wa kati lakini pia kuna wafanyabiashara wadogo wadogo. Mhe. Naibu Spika, eneo lile pana wananchi ambao walikuwa wanafanyabiashara kwa muda mrefu za kujipatia rizki za maisha yao, eneo la Maruhubi karibu na Kiwanda cha Maziwa.

Mhe. Naibu Spika, eneo lile ubavuni kwake kumejengwa na pana mmiliki pana kampuni pale kuna kauli kwamba mmiliki yule ameanza kuwabughudhi wafanyabiashara wale ambao wanaishi pale kwa muda mrefu na wanatafuta rizki zao na tayari ameshaanza kuwaambia kwamba wafanye maarifa ya kuondoka. Sasa hili sijui kama Mhe. Waziri analifahamu kwa sababu wale ni binadamu ambao wanahangaika kutafuta rizki kwa kufanya biashara zao ndogo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kutokana na mwelekeo wa Mhe. Waziri na jinsi anavyosisitiza watu kuondosha umasikini na kuwasaidia nilikuwa nafikiria labda watu wale wangejengewa eneo lile katika mustakbal mzuri ili kuweza kufanya biashara zao kwa uhakika. Lakini nasikia kwamba wameambiwa wafanyabiashara wale waondoke na sehemu ya kwenda hawapajui. Kwa hivyo, hili namomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atusaidie kwamba hilo kweli lipo au halipo na kama lipo atasaidia vipi wafanyabiashara wa eneo lile la Maruhubi katika Jimbo la Chumbuni.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika suala la wafanyabiashara wa mikononi eneo la Darajani. Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wenzangu walizungumza kwamba biashara zile hazina viwango, lakini mimi sizingumzii suala la viwango nazungumzia kwamba biashara zile zinazouzwa pale nyingi zinakuwa zimeshamaliza muda wake. Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tunapiga kelele sana hapa na kuzilaumu baadhi ya taasisi na hususan Wizara ya Afya kwamba wagonjwa wanaongezeka, huduma haziwi nzuri lakini biashara mbovu nazo zinachangia kuwapa wananchi maradhi.

Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo ambalo sasa hivi limejitokeza huu ulimwengu wa leo mheshimiwa ni ulimwengu wa teklonojia sasa hivi tuna mashaka kwamba kwa baadhi ya wafanyabiashara wana vifaa vya ku-*print* na vifaa hivi vinapelekea kubadilisha taaswira ya biashara zinazouzwa pale mheshimiwa kuna biashara ukiiangalia dukani biashara hiyo hiyo inauzwa shilingi 5000 lakini ukenda pale inauzwa shilingi 1500.

Mhe. Naibu Spika, hili suala linatuumiza kichwa nimuombe Mhe. Waziri kupitia kitengo kinachohusika apite katika maghala ya wafanyabiashara kukagua biashara zao. Pia aangalie hawa wajanja wenye vifaa vya ku-*print* karatasi katika kuweka *expire date* utaikuta biashara ile ile unaiona kwamba bado haijafika muda wake wa kumalizika, lakini kumbe biashara ile imefanyiwa ujanja na wafanyabiashara hii ni hatari kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa namuomba Mhe. Waziri ajitahidi na kuhakikisha kwamba anawalinda wananchi wa nchi hii. Baada ya mchango huo mheshimiwa kwa kuheshimu muda wako kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia asubuhi hii kupata nafasi hii na mimi kuchangia angalau kwa muhtasari hotuba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Lakini pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri juu ya uwasilishaji wa bajeti yake katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikikiangalia hiki kitabu cha bajeti katika upande wa pili kuna picha nzuri sana ya karafuu mbichi na karafuu kavu zilizopo chini yake. Hii ni kuonesha kwamba uchumi wa Zanzibar bado unalitegemea zao la karafuu pamoja na mengine ambayo yapo lakini zao la karafuu litakuwa ni zao mama.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu mkubwa mimi utazingatia sana suala hili la zao la karafuu Zanzibar hasa ukizingatia kwamba muda ulionipangia ni mchache. Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba Mhe. Waziri aliangalie suala zima la karafuu katika maeneo mbali mbali, mbali ya bei nzuri ya karafuu iliyotangazwa hivi juzi mimi nampongeza kwa bei hii, lakini kuna changamoto kadhaa ambazo zinawakabili wavunaji wa zao hili la karafuu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie vyema na alifanyie kazi kwa kina ili wachumaji wa karafuu wafanikiwe katika uchumaji wao wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa changamoto hizo ni malalamiko makubwa ya wachumaji wa karafuu kuhusu mezani hivi sasa inalalamikiwa sana wauzaji wengi wa karafuu wanalalamika kwamba hazitimizwi katika vipimo vya mezani. Kawaida ya karafuu pishi moja ya karafuu ni kilomoja na nusu, lakini wanapopima katika mezani karafuu kwa kweli zinakuwa hazitimii kiwango hicho. Na karafuu ni mpya zimechumwa juzi tu bado hazijakuwa nyepesi kiasi hicho, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie vyema kwa sababu mezani hizi ni kongwe. Pamoja na kukaguliwa mezani za vyakula lakini na mezani za *ZSTC* zikaguliwe ili zifikie viwango.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo changamoto ya pili ambayo inaikabili zao hili la karafuu kwa wakulima ni grade za karafuu kwamba kuna *grade* I, ya II na *grade* ya III. Hapa ndipo panaposababisha watu wengi wakapeleka karafuu zao kwa watu wa magendo kwa sababu watu wanaochukua magendo hawana *grade* karafuu pishi ni shilingi 2000, kwa nini serikali kupitia *ZSTC* iuze bei ya kwanza, ya pili na ya tatu. Mhe. Naibu Spika, karafuu za Zanzibar katika kiwango cha jua kali basi hazina grade ya tatu wala grade ya pili. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri awawezeshe wachumaji wa karafuu kwa kuwatafutia vifaa makini vya kuanikia karafuu ili labda hizo karafuu zisianikwe katika maeneo holela zikakosekana hivyo viwango ambavyo vinatarajiwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo linakuwa ni changamoto kwa wachumaji wa karafuu namuomba Mhe. Waziri hapa apaangalie kwa kina, uchumaji wa karafuu kwa kweli ni uchumaji wa hatari kwa sababu ni juu. Mhe. Naibu Spika, kuna watu wengi huanguka mikarafuu, wengine wakapoteza roho na wengine wakapoteza viungo. Mhe. Naibu Spika, kuna watu walioanguka mikarafuu tokea mwaka 2009 hivi sasa wako kitandani. Je, wizara hii kupitia *ZSTC* watu

hawa waliopata ulemavu na wengine bado ni wagonjwa huu mwaka ni watatu hivyo wanawaangalia vipi kwani na wao walikuwa wanaokoa zao hili la taifa?

Mhe. Naibu Spika, lakini mbali ya hayo niende katika taarifa tuliyoisikia asubuhi katika vyombo vya habari kuhusiana na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mhe. Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba amesema kwamba karafuu hairuhusiwi katika Mkoa wake kuchuma shehia moja zikaanikwa katika shehia nyengine. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo kwa sababu mfano Jimbo langu la Chambani lina wakulima wa karafuu asilimia 90 mikarafuu yao iko katika shehia nyengine, hivyo wanachuma karafuu kwa kutegemea kuzisafirisha kwa baiskeli, punda, gari za ng'ombe na mengineyo. Mhe. Naibu Spika, mtu kama huyo atawezaje kuchukuma karafuu kutoka Shehia ya Chambani akaanika karafuu Shehia ya Mtambile na hana kambi. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri nakuomba utuwekee sawa ili wachumaji wetu wa karafuu wasibabaike na kauli hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna taarifa ambazo tumezipokea katika baadhi ya shehia zetu, kuna baadhi ya maeneo Kengeja wameonekana askari polisi wakifuatana na sheha kuchukua karafuu za wananchi ambazo zimeshakauka kwa kuwa wenyewe hawajazipeleka *ZSTC*. Mhe. Naibu Spika, karafuu kwa wanyonge ni mali ya akiba, watu wamechuma karafuu kwa ajili ya kutatua matatizo yao mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, leo Sheha anaambatana na askari kwa ajili ya kuzichukua karafuu hizi kuzipeleka katika kituo cha polisi. Mhe. Naibu Spika, nakuomba kwa heshima na taadhima utuwekee sawa tatizo hili kama liko kwa sababu nahofia kesho au keshokutwa kukawa na mapigano baina ya wachumaji karafuu na vyombo hivi ambavyo vinasimamia uchumaji wa karafuu katika shehia.

Mhe. Naibu Spika, pia jengine ambalo nataka nilizungumze inasikitisha sana kwamba nchi jirani mwaka 2001 mpaka 2009 imesafirisha karafuu tani 9510 tujiulize sisi karafuu hizi tumezikosea nini na kwa nini tuzikose? Mimi nahisi kwamba tumezikosa kwa sababu karafuu bado hatujataka kuzitangaza bei halisi ambayo inakubalika. Mhe. Naibu Spika, kwa mantiki hii basi ili kuzuia mwenendo wa magendo kwa kasi basi Shirika la *ZSTC* pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikae pamoja kwa kina iangalie bei inavyoendana kwa sababu nchi jirani inauziwa karafuu kutoka Zanzibar na inauza karafuu katika nchi za nje. Kwa nini sisi tushindwe kuziuza karafuu kwa bei nzuri na wakulima wetu wa karafuu tukawapa bei nzuri ambayo itakata miguu ya hawa watu wa magendo.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache na kwa kuokoa muda wako mimi naiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja pamoja na machache ambayo nimeyataja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chambani, ahsante sana.

Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama leo na kuja hapa Barazani. Lakini la pili nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Aidha, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti hii pamoja na watendaji wake wote kuanzia Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi. Kitabu chao ni kizuru, kimeandika vizuri na Mhe. Waziri amekisoma vizuri nasema hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, historia ya wizara hii katika muundo imekuwa ikienda ikibadilika, zamani ilikuwa ni Wizara ya Biashara na Viwanda baade ikawa ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kama sasa ikabadilika tena ikawa Wizara ya Biashara, Viwanda, Utalii na Uwekezaji na sasa imerudi katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa hakika hivi ilivyo nahisi itatusaidia kutenda kazi vizuri wakati ule ilipokuwa na utalii, uwekezaji shughuli za viwanda vilidorora kwa sababu shughuli za utalii nazo ni muhimu katika uchumi wa nchi na shughuli za uwekezaji nazo ni muhimu katika uchumi wa nchi. Bahati nzuri sasa uwekezaji umekwenda Wizara ya Fedha na utalii uko Wizara ya Habari.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa dunia imebadilika sana kibiashara na ndio maana bei za bidhaa zimebadilika zimekuwa za juu. Nchi za Ulaya ambazo kwa muda mrefu zimetawala soko la dunia hata nazo zina hofu kwa sababu nchi za Asia kama China, India na Brazil uchumi wao umekuwa sana na wanalikamata Soko la Dunia na zaidi la Afrika. Kwa hivyo, sisi huku nchi masikini tunatakiwa tujipange vizuri ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu hautetereki na tunasonga mbele katika kuimarisha maslahi ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, nianze kwa kumuomba Mhe. Waziri kwamba ni muhimu sana kwa Zanzibar kuhudhuria katika vikao vya kikanda, vikao vya *SADC* na vya *East Africa*. Kwa sababu kwa ngazi yetu sisi vikao hivi vinatusaidia kujiimarisha kiuchumi na kujijengea uwezo. Bahati nzuri miaka mitano iliyopita yote nilikuwa mshiriki wa shughuli za Afrika Mashariki nilikuwa naona pale jinsi maamuzi ya vikao vile ambavyo vinaweza kuigharimu au kuisaidia Zanzibar.

Kwa upande wetu tusiweke nguvu kwa vikao vya mawaziri tu, tuweke nguvu zaidi katika vikao vya watendaji wetu ambao ndio wanapanga na zaidi vile vikao ambavyo tunashiriki sisi na Tanzania Bara ndio pale maslahi yetu yanaanza kuangaliwa. Kwa hivyo, mimi sikubaliani na wale wanaosema kwamba wizara hii imepangiwa fedha nyingi za safari, mimi naona sio nyingi. Kwa sababu wana safari za kiuchumi na za kibiashara nafikiri kila mwezi sasa

ukisema shilingi milioni mia mbili ni nyingi mimi naona hatujaangalia vizuri. Kama kweli tunataka kuisaidia nchi yetu kiuchumi na kibiashara basi mimi ningeliweza kusema fedha hizi ni kidogo, lakini kutokana na hali yetu ya kiuchumi zibakie hizi hizi. Lakini wana vikao vingi vya kiutendaji ambavyo vitasaidia sana katika kuimarisha maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hilo nizungumzie suala la karafuu. Suala hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi na mimi bila shaka nastahiki kutoa mawazo yangu. Kwanza niunge mkono hii azma ya serikali ya kulifanyia mabadiliko Shirika lenyewe la *ZSTC*, nafikiri tayari limeshajadiliwa, muundo umetengenezwa ili kuwa na Shirika zuri litakalofanya biashara vizuri. Mhe. Waziri namuomba aendelee na utaratibu wake kwa uangalifu mkubwa ili kuona kwamba maslahi tuliokusudia yanafikiwa.

Lakini pia hii biashara yenyewe ya karafuu. Kwanza tumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa sababu katika ziara zake kabla ya kuchaguliwa na baada ya kuchaguliwa mikoani na wilayani Mhe. Rais alikuwa akisema kwamba mkinichagua na kwa mujibu wa Ilani ya CCM kifungu Nam. 128(h) kinazungumzia kuimarisha mazao na zaidi karafuu. Sasa Mhe. Rais alipokuwa mgombea alikuwa akisema mkinichagua nitaimarisha zao la karafuu na kuliimarisha kwenyewe kwanza kwa mikarafuu yenyewe kupandwa upya, kuisimamia na kuweka bei nzuri kwa wakulima na mambo haya bahati nzuri yote kayafanya Mhe. Rais wetu. Anahimiza upandaji wa mikarafuu mipya, anahimiza kushughulikiwa kwa mashamba ya mikarafuu, lakini amesimamia upandishaji wa bei ya karafuu kwa kiwango kikubwa kabisa. Kwa sababu ukisema asilimia 80 ya bei ya soko la dunia unampa mkulima hiyo ni bei ambayo haijawahi kutokezea.

Lazima tukubaliane jamani, hapa tumeoneshwa na Mhe. Waziri kwamba mwaka 2001 mpaka 2009 tani ambazo zimesafirishwa Mhe. Waziri kasema nchi jirani hakuitaja lakini sisi tuseme Kenya ni tani nyingi tu, karibu 9,510 zenye thamani ya shilingi za Kimarekani milioni kumi na sita ni fedha nyingi sana kwa nchi kama ya Zanzibar. Sasa kipindi kama hiki magendo yanaposhika kasi na serikali kupitia *ZSTC* kushindwa kununua karafuu huitaratjii *ZSTC* tena ikawalipe walioanguka kwenye mikarafuu kwa sababu karafuu yenyewe haiwapati sijui watamlipaje mtu ambaye hawauzii yeye, huwezi kujua kama huyo aliyeumia kapeleka huko shimoni au kawauzia *ZSTC* kwa hivyo ilikuwa kizungumkuti. Lakini nina hakika sasa ilivyokuwa biashara hii serikali imesema iendeleze na nina hakika kupitia sisi Waheshimiwa Wawakilishi zaidi wale ambao majimbo yao iko mikarafuu ya kutosha tutahamsisha wananchi wetu waziuze karafuu *ZSTC* ili kwanza wapate bei nzuri wao wenyewe lakini na serikali iweze kufanya shughuli nyengine za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, unapofanya magendo kuna mambo mengi ya *risk* ukikamatwa karafuu yote inakwua sio yako na mtaji wako unakufa, ukiuzia *ZSTC* mambo yako mazuri, fedha zako unapewa, *cash* yako unatumia, unafanya shughuli zako na serikali inafanya shughuli nyengine za kimaendeleo.

Lakini pia mimi niunge mkono utaratibu huu wa kuendelea kuwa na madaraja ya karafuu. Mhe. Waziri ametueleza kwamba lengo letu Zanzibar tuwe na nembo ya karafuu yetu, dunia nzima itambulikane hii karafuu ya Zanzibar, sasa tukisema tuchanganye mawe, mchanga, kokoto lakini iuzwe tu kwa bei moja kuna siku tutakataliwa duniani kuuza karafuu hii na tutakapokataliwa tutakuwa hatuna vya kuifanya hata hiyo bei ambayo tunauza sasa hivi hatimaye itashuka na kila mtu ataikataa hiyo karafuu.

Wenzetu Bara huko wanasumbuka sana na zao la pamba, wengine wanazitia maji, wanaweka mawe, sasa hivi pamba inakuwa ni vigumu sana kuiuza duniani. Kwa hivyo, sisi tusijitie katika mtego huu pesa kila mtu anaipenda lakini lazima tuitafute kwa utaratibu mzuri. Kwa hivyo, *ZSTC* lazima wawe na madaraja yao daraja la kwanza, la pili na la tatu na nafikiri utaratibu huu kwa miaka yote tangu zao hili Zanzibar linaanza upo. Sasa kuna kasoro nyengine kwa sababu ukianza jambo jema lazima kutakuwa na changamoto, kama kuna changamoto za minzani sawa hilo litatuke, kama kuna changamoto za uanikaji litatuke lakini lazima tukubaliane kwamba tunafanya biashara hii katika kuiweka kwenye mazingira mazuri ya kusaidia nchi yetu na kuwasaidia wakulima wa zao karafuu.

Niwaombe basi wale wakulima kwa kupitia Waheshimiwa wenzangu hapa ni muhimu sasa kwa kuwa imeonekana biashara hii ina faida kila mtu akashughulikie mashamba yake na wale ambao wanaona ni vigumu kuyashughulikia wawauzie watu wengine, sasa hivi hata kununua mashamba ya mikarafuu nayo ni kazi nzuri kwa sababu kazi hii ina faida. Kwa hivyo, mimi naomba tutoe umuhimu kwa wakulima lakini pia wakulima nao wachukue wajibu wao wa kuisaidia serikali katika shughuli hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie bei za vyakula kwa sababu muda wenyewe nimepewa mdogo. Najua kuna juhudi za serikali za kupunguza makali ya bei za vyakula. Mimi naomba Mwenyezi Mungu akitujalia kesho Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo apate nafasi ya kulieleza Baraza hili jinsi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyojitolea kusamehe wafanyabiashara kodi ili wasipandishe bei kwa wananchi wao. Pengine nafikiri watu wengine hawajui kwamba serikali huwa inapunguza au kusamehe kodi ya mchele, kodi ya sukari na unga, na kwa sababu tunakwenda katika mwezi mtukufu wa Ramadhani nahisi ni wakati

wake Mhe. Waziri kesho azungumze na Baraza hili ili kuonesha kwamba serikali sio kwamba inapandisha kodi kwa kuwaumiza wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu umenambia muda ni mdogo basi ni malizie kwa kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa wenzangu tuunge mkono bajeti hii Mhe. Waziri naona amejipanga vizuri na serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yanasonga mbele.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kupata dakika chache sana kuchangia hoja hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri na wizara kwa jumla, kitabu kidogo lakini kizuri kabisa, kimeandikika na mambo yote ambayo kwa kweli tulitarajia nahisi yamo kwenye hotuba hii.

Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa vile ametuonesha kwamba hali ya biashara ilivyo ulimwenguni, hali ilivyo hapa kwetu na uzalishaji wake wa mazao kwa ujumla hapa kwetu ukoje, mwenendo wa bei na akatushauri jinisi ya kuweka sawa kupunguza hayo makali. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hayo.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nataka nigusie suala moja tu ambalo hata Mhe. Waziri mwenyewe amelizungumza katika ukurasa wa 66 kifungu 94 juu ya wafanyabiashara wetu. Mhe. Naibu Spika, naungana naye kuwashukuru wafanyabiashara wa Juwakali na wengine kwa ujumla kwa kutusaidia katika suala zima la biashara. Sote tunafurahi mahitaji yetu sasa wewe na pesa yako tu, chochote unachokitaka Zanzibar leo kinapatikana. Hilo ni jambo la busara sana ukitizama huko nyuma tulivyokuwa ambapo serikali ilikuwa ikijishughulisha na biashara.

Mhe. Naibu Spika, niungane na waziri kwa kuwashukuru wafanyabiashara lakini sasa mimi nitakwenda kwengine. Ilivyokuwa nasimamia Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, basi niungane naye sasa tufanye juhudi za pamoja kwamba wafanyabiashara wetu wafuate taratibu. Nikisema taratibu nakusudia zile biashara wafanye mahali gani. Kulikuwa na michango ya Waheshimiwa wawili wawatu wakiwalaumu askari wetu wa Manispaa kwamba wanawanyang'anya, wanawatesa wafanyabiashara wadogo wadogo. Hiyo sio dhamira ya Baraza la Manispaa wala Mabaraza ya Miji. Serikali haja yake iwashajiishe wafanyabiashara hawa wafanye kazi zao vizuri, hilo ndilo lengo letu. Lakini ninachoomba Waheshimiwa tushirikiane sote kufahamu kidogo

taratibu zilizowekwa, hawa wafanyabiashara wanatakiwa wafanye biashara wapi na kwa wakati gani.

Kwa sababu mabaraza ya miji na Baraza la Manispaa Mhe. Naibu Spika, kazi zake kubwa ni kubuni, kuratibu, kusimamia utekelezaji wa mipango ya kiuchumi, biashara, viwanda na maendeleo ya jamii katika miji yetu. Sasa hizi kazi za biashara tunakwenda sambamba au wenzetu wa biashara wanakwenda sambamba na Mabaraza ya Miji ili miji yetu ile haiba yake ionekane. Haitokuwa vyema Mhe. Naibu Spika, leo hapa panauzwa samaki, hapa watu wanajisaidia, hapa gari zinapaki, mji huo hautovutia.

Mhe. Naibu Spika, leo watalii utawakuta wanakwenda marikiti kupiga picha mnada wa samaki tu ule, sasa ni vizuri wale watu tumewaweka wote wauza samaki wako pahala pamoja, utaona watalii wanaingia sokoni wanapiga picha taa, hawamjui taa, pweza vile anavyopigwa ni kivutio kwake, sasa ile ndio mipango ya miji. Ukienda nyuma kule anakwenda kuangalia gungo halijui, lakini anajua bungo nitaliona wapi, ndizi ya mkono mmoja anajua wapi, matunda yote anayaona pale; akitoka anakwenda Mji Mkongwe anaangalia hiyo ndio mipango ya miji. Sasa haitopendeza wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wakapanga bidhaa chini kwenye barabara, pale ndio inapotokea kutofahamiana na Baraza la Manispaa.

Si nia yetu wala hatuwatumi kuwabughudhi, lakini ningeomba sana waheshimiwa tusaidiane tuwaelimishe watu wetu sisi ndio wenye wananchi tufuate taratibu za kufanya biashara. Na sisi tutapokea maombi wapi tuweze masoko mapya, itakuwa vizuri, tutakaa pamoja na Mhe. Waziri wapi tufanye soko jipya na kujua nyinyi mnauza nini? Samaki, basi kaeni hapa, nyinyi nini? Viazi kaeni hapa, washona nguo kaeni hapa, wafua vyema kaeni hapa, mji utapendeza.

Kwa mfano sasa hivi Mhe. Naibu Spika, kiasi cha saasabaa au nane wende zako Skuli ya Vikokotoni pale ile njia imefungwa kabisa, maana yake wewe mwenyewe kupita utaogopa, mara utakanyaga kitambaa cha watu mtu atakwambia ukinunue hicho umeshakichafua kitambaa changu. Mimi ningeomba sana Waheshimiwa hatuna dhamira ya kuwatesa wala kuwasumbua wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini naomba sana tushirikiane nao na waheshimiwa tusaidiane kuwafahamisha lengo letu, hiyo ndio kazi ya miji yetu kuleta haiba ya mji wetu na kivutio kwa watalii na sisi wenyewe tutajua nataka kitu fulani niende mahala fulani.

Mimi Mhe. Naibu Spika, huo ndio ulikuwa mchango wangu tu, kuwa wenzangu tushirikiane kuleta haiba nzuri na kupanga hasa mradi huo mpya

unaokuja wa kuisaidia *Zanzibar Municipality*. Ahsante Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwana nichukue fursa hii nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Baada ya kukushukuru naomba niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, napenda nitoe pongezi na shukurani zangu kwa Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutimiza majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nasikiliza kwa makini michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Na takriban wengi waliozungumza walizungumzia suala la kukuza biashara nchini, suala la kuendeleza viwanda na suala la kuimarisha masoko yetu nchini. Kwa kweli wizara hii imefanya kazi kubwa katika jitihada za kufanya shughuli hiyo, kwa hivyo, Waheshimiwa Wawakilishi na serikali tunazungumza lugha moja yenye nia ya kuimarisha sekta zetu muhimu hizi za biashara, viwanda na masoko.

Kwa hivyo, nataka niwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa michango yenu na kuahidi kwamba serikali imo katika jitihada hizo za kuhakikisha kwamba sekta hizi inaziimarisha.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi walizungumzia suala la punguzo la kodi kama ni sehemu moja ya kuimarisha biashara Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, punguzo la kodi wakati mwengine lina athari zake, kwa sababu tunaisikia hapa namna ya waziri alivyojipanga kuimarisha viwanda vyetu. Kodi hizi nyengine zinawekwa kulinda uzalishaji nchini kwa maana ya kuimarisha viwanda na sote tulimsikia Waziri wa Kilimo na Maliasili alivyoelezea namna anavyoimarisha kilimo ili kiwe sehemu ya malighafi za viwanda ambavyo Zanzibar zinakusudia kuzitekeleza. Kwa hivyo, moja katika suala hili la punguzo la kodi la ushuru athari yake ni kuumiza ile *base* ya kuimarisha viwanda vyetu hapa nchini. Kwa sababu unazichukua biashara za nje za nchi ambazo tayari wamepiga hatua kubwa katika maendeleo haya ya uzalishaji nakuzishindanisha na bidhaa zako za ndani.

Hata zile jitihada zetu za kuendeleza kilimo kwenye maeneo mengine vile vile tunaweza kuvunja moyo sana wakulima wetu hasa wafugaji wa kuku, mayai na kadhalika. Kwa hivyo, jitihada hizi zinazowekwa za kikodi maana yake moja ni kulinda uzalishaji wa ndani.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, kwa mfumo wetu huu tunaotumia soko moja ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maana yake unapopunguza kodi unaiambia bidhaa ipitie sehemu ambayo kodi umeipunguza na kwa mujibu wa kutumia soko moja unahitaji uwiyano ulio sawa katika suala zima la kodi. Msingi wake ni kwamba ili soko liwe moja basi lazima na kodi ziwe moja, huwezi kupunguza kodi upande mmoja ukaongeza upande mwengine halafu hapo ushindani ukawa uliosawa. Hiyo haiwezekani. Kwa hivyo, unapopunguza kodi kwa upande wako ina maana unajitoa katika ule mfumo wa soko la pamoja na matokeo yake sasa inabidi ukiingia katika soko hilo unaingia kwa asilimia mia moja ya *tariff* ya upande huo. Kwa hivyo, utaratibu wetu tulionao huu wa Jamhuri ya Muungano ni kwamba tunalo soko moja kwa hivyo viwango vyetu vya kodi lazima viwe vimoja, hakuna namna ambayo utafanya ili uweze kupunguza upande mmoja.

Lakini upande mwengine tumo kwenye mfumo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa hivi utaratibu wa kikodi unapangwa katika Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki. Inawezekana kabisa kupata unafuu wa kodi kwa baadhi ya bidhaa ambazo zinatumika ndani ya nchi yako na ambazo kuweka kodi kubwa zinaleta taathira. Kwa mfano, hapa Zanzibar tunayoa fursa ya kupunguza kodi kwa mchele, lakini tumekubaliana pamoja ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, bidhaa ile inatakiwa itumike pale ilipopata unafuu huo tu, kwa maana kama ni Zanzibar ule unafuu iliyopewa utumike katika soko letu tu, na haitaruhusiwa kupeleka katika soko la mwengine. Unapoipeleka bidhaa ile katika soko la mwengine maana yake ni bidhaa inakuwa kwa mujibu wa utaratibu wa kodi huu ni bidhaa inayotoka nchi nyengine na msingi huo inabidi itozwe kodi kwa asilimia mia moja.;

Kwa hivyo, unapokwenda kinyume na wenzako katika mfumo wa kikodi wanakutoa katika ule utaratibu mzima wa kuwemo katika soko la pamoja. Hivyo, lazima tutizame kwamba taathira hizi za punguzo la kodi zisije zikatuathiri kwenye masuala mazima ya nia na dhamira yetu ya kukuza biashara hapa Zanzibar. Vile vile masuala haya juu ya mifumo ya kikanda yanaungana pia na mwelekeo wa dunia. Hivyo hatuwezi kuwa nje ya utaratibu huu wa *WTO* kama sisi ni nchi. Lazima tukubaliane kwamba tunayoyafanya yote lazima tuyapime kwa msingi tufanye shughuli zetu pia zenye mwelekeo utakaoweza kukuza biashara yetu, viwanda vyetu, utakaozidisha uzalishaji nchini.

Tumetoa fursa hapa ya punguzo la kodi na nyote ni mashahidi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, fursa hiyo tulioitoa ya punguzo la kodi kwenye mchele na sukari lakini bado tunalalamika kwamba bidhaa hizi bei zake ni kubwa. Hii maana yake ni kwamba wafanyabiashara wetu hata tunapowapa nafasi ya

punguzo la kodi bado wanatumia bei kwa vigezo vya ile kodi kamili na matokeo yake si wananchi wote wanaopata nafuu bali wanaopata nafuu ni baadhi ya wafanyabiashara. Kwa hivyo, lazima serikali kwenye jambo hili tuipe nafasi ifikirie kwa kina ione hatua za kuchukua.

Hatua nzuri za kuchukua ni hizi Mhe. Waziri wa Biashara ambazo amezieleza kwa kina, kwamba mwelekeo wetu ni kuelekea kwenye bandari huru kwa Zanzibar, lakini kwa kuwa bado hatuna miundombinu ya kutosha ya kufikia hatua hiyo ni lazima twende hatua kwa hatua na ndio maana Mhe. Waziri akaelezea *special economic zone,* suala la *export process zone* akaelezea suala la *free port facilities*, yote haya ni ya hatua za awali zinazoelekea kwenye bandari huru. Sasa mimi naomba Waheshimiwa wenzangu tumuunge mkono Mhe. Waziri na jitihada zake hizi. Kwa sababu jitihada hizi zinakubalika kikanda, zinakubalika kimataifa na zitaweza kusaidia katika mfumo mzima wa kuendeleza biashara nchini na kukuza uchumi.

Mimi naamini kabisa kwamba jitihada zetu hizi zitazaa matunda na kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha biashara katika Afrika Mashariki na niseme hata na nchi nyengine ulimwenguni. Kwa hivyo, tumpe nafasi Mhe. Waziri na serikali katika jitihada ambazo anachukua.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu urari wa biashara. Ni kweli upo urari wa biashara hasa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa sababu sisi Zanzibar tunaagiza bidhaa nyingi za kilimo kutoka Tanzania Bara, ndio maana serikali yetu ikaweka mkazo maalum wa kuimarisha kilimo ili tuweze kujitosheleza kwa bidhaa za kilimo na tupunguze basi uagizaji kutoka nje na kutoka Tanzania Bara na hiyo itakuwa ndio njia moja ya kuziba pengo.

Huko nyuma kulitolewa mifano kwamba Zanzibar ikisafirisha zaidi kupeleka Tanzania Bara. Ni kweli lakini ilikuwa ni *re-export,* ni bidhaa zile zinazotoka Malaysia, China, Indonesia na kwengine, hizo zilikuwa zikija Zanzibar na kupelekwa Tanzania Bara. Hiyo ilitokana na kwamba mfumo wa kodi uliokuwepo ulikuwa unasababisha kuwe na upungufu wa kodi kwa upande wa Zanzibar kwa hivyo, ulikuwa unatoa nafasi kwenda kuuza Tanzania Bara. Sasa kwa mujibu wa hali halisi ilivyo utaratibu huo huwezi ku-*apply* na ndio maana tukapata matatizo haya ambayo yanajitokeza.

Kwa hivyo, cha msingi sana ni kuimarisha jitihada zetu za uzalishaji, kuimarisha kilimo, kujenga *base* nzuri na kuimarisha viwanda ili uzalishaji wa ndani uwezekane kuepukana na huu urari wa biashara. Kwa sababu mwelekeo wa ulimwengu huko tunakokwenda ni kwenda kwenye zero time, kwa hivyo utakachokuwanacho ndicho utakachouza kwa mwenzako n asana inategemea comparative adventage yako katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, juu ya kwamba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alionesha suala la bidhaa zetu ipo tofauti kubwa, lakini alionesha sana suala la *trade in goods* kwa maana ya bidhaa na hakuonesha *trade in services* huduma. Sisi kama kisiwa uchumi wetu una muelekeo mkubwa wa kwenye kutoa huduma na moja katika kipaumbele chetu kikubwa ni suala la utalii. Mimi naamini kabisa hatua zilizochukuliwa sasa katika kuweka vizuri takwimu zinazotokana na mapato ya utalii, tutakapomaliza kuweka vizuri takwimu hizo nina hakika kabisa mauzo yetu ya utalii yatakuwa yanaondosha hili pengo linalojitokeza katika biashara kati ya Zanzibar na ulimwenguni.

Kwa sababu hivi sasa Mhe. Naibu Spika, unapokwenda kwenye maduka haya ya kuuza fedha za kigeni unazikuta msingi wake ni kwamba zipo na zinaingia nchini na *source* yetu kubwa ya kuingiza fedha hizo ni utalii. Kwa hivyo, hapana shaka yoyote kwamba ukifanya utafiti wa kina kwenye mauzo ya utalii basi suala zima hili la *trade visit* kwa Zanzibar inaweza kuwa imefunikika. Lakini hayo kwa sababu serikali inaweza kuchukua hatua ya kuweka takwimu hizi za utalii naamini Waziri atakapokuja katika bajeti inayokuja ya mwakani atalieleza kwa kina hili na tatizo hilo litakuwa limeondoka.

Mhe. Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wajumbe walituuliza suala la vipi tumetayarisha kuingia katika soko la pamoja. Mhe. Naibu Spika, nataka niwahakikishie wajumbe wako na Baraza lako tukufu hili kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitayarisha vizuri sana katika kuingia kwenye mfumo huu wa soko la pamoja.

Mhe. Naibu Spika, hizi jitihada zetu za kwanza za kuongeza kasi ya upatikanaji wa elimu hayo ni sehemu ya matayarisho. Lakini mkakati wetu kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini ni sehemu ya matayarisho. Mkakati wetu wa kuimarisha biashara kwa maana ya kutoka katika ule mfumo wa uchumi hodhi na kuwa biashara huria ni sehemu ya kujitayarisha katika kuingia katika soko la pamoja. Ndio maana tukavutia uwekezaji kwa kuanzisha kituo cha uwekezaji nia yetu ni kuvutia uwekezaji hasa katika utalii, biashara, viwanda, uzalishaji, bandari huru, mawasiliano, uvuvi, kilimo cha viungo na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachoamini tunaweza kuwa kituo kikuu cha Utalii katika Afrika ya Mashariki, tunaweza kuwa kituo kikuu cha Mawasiliano katika Afrika Mashariki, tunaweza kuwa kituo kikuu cha Uvuvi katika Afrika Mashariki, tunaweza kuwa kituo kikuu cha Taasisi za Fedha katika Afrika Mashariki, muhimu hapa ni kuendelea kushirikiana na kujenga nchi yetu.
Mhe. Naibu Spika, mazingira ya sasa yanaturuhusu sana chini ya mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maana mazingira haya yanajenga mazingira mazuri zaidi ya amani, utulivu, kitu ambacho kinavutia zaidi uwekezaji. Kwa

hivyo, ningependa nikawatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwahakikishia kwamba suala letu la kushiriki katika umoja wa soko la pamoja inawezekana sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda ningependa tu nimalizie haraka haraka kusema kwamba pia tunajenga uwezo kwa kujadiliana na taasisi za kiuchumi kama vile *World Bank, IMF na WTO* ili kupata maamuzi yenye maslahi kwa Zanzibar. Maneno haya mara nyingi Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameyazungumza sana katika kuimarisha uchumi wetu na mimi napenda nimshukuru na nimpongeze sana kwa sababu jitihada hizo zinafanywa na yeye kadri anavyozidi kutuelekeza ndivyo tunazidi kujenga ufahamu mkubwa kwa kuweza sasa kupata nafasi ya kushiriki kikamilifu katika jumuiya hizi za kikanda na za kimataifa kwa maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba niunge mkono hoja na nawaomba wenzangu sote kwa pamoja tumuwezeshe Waziri na muipitishe bajeti yake hii vizuri bila ya buti, bila ya vishindo, ili akafanye kazi hii kwa vizuri sana. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia na mimi fursa ili niweze kuzungumza machache katika hotuba hii ya Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia sote hapa afya njema na tukaweza kufika hapa na kutekeleza wajibu wetu kama ambavyo serikali imetuagiza.

Mhe. Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini na kuniteua kushika nafasi hii ya Naibu Waziri katika Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Naomba nimuahidi Mhe. Rais kwamba *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatushushia kila lenye kheri na atatupa uwezo katika kufanya kazi zetu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, siwezi kabisa kuwasahau wananchi wa Jimbo la Fuoni ambao wamenichagua kwa kura nyingi za kupigiwa mfano ili niweze kuja kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu. Mhe. Naibu Spika, kupitia kwako naomba niwaahidi kwamba sitowaangusha.
Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba niichangie hotuba hii kama ifuatavyo. Kwa ujumla tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wametuchangia katika Wizara hii na tunasema kwamba tunawaahidi michango yao tunaichukua kwa kuifanyia kazi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tukienda kwa mchangiaji mmoja mmoja nitakwenda katika ile mantiki yaani hoja na si kwa mwakilishi mmoja mmoja.

Mhe. Naibu Spika, namsaidia Mhe. Waziri kujibu hoja hizi kwa niaba yake. Kuna waheshimiwa wawili wamezungumzia suala zima la zao la mwani. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaangalia ni jinsi gani tutaweza kuendeleza zao la mwani ili tuweze kuliongezea bei baada ya kuongeza thamani yake. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala hili tayari tumelichukua kwa kulizingatia na lipo katika kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile waheshimiwa walizungumzia suala zima la uzalishaji wa zao la chumvi. Mhe. Naibu Spika, wakati tunatembelea katika taasisi mbali mbali mara baada ya kukabidhiwa wizara hii na serikali mimi na Mhe. Waziri tulibahatika pia kutembelea vikundi vya wazalishaji wadogo wadogo. Tulipofika Pemba Mhe. Naibu Spika, tulikiona kikundi hichi cha uzalishaji wa chumvi ambacho kinaitwa *AZASO* kipo pale Wawi tunashirikiana nao kwa karibu sana kwa msaada wa *UNICEF*.

Mhe. Naibu Spika, wizara inakubaliana kabisa na mawazo ya waheshimiwa waliochangia suala hili kwamba soko la chumvi lipo. Hivi sasa wizara inalishughulikia kwa kina na tunawapa ushirika huu mashirikiano ya karibu na tumehakikisha kuwa chumvi wanayozalisha inawekewa *iodine* kama ambavyo viwango vya uzalishaji wa chumvi vinavyoelekeza. Kwa hivyo, tunawaomba waheshimiwa wafahamu kwamba suala hili tunalo na tunaendelea nalo na ushauri wao tutauzingatia katika kufanikisha zaidi uzalishaji wa chumvi.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwaongezea taaluma wazalishaji wadogo wadogo nalo limezungumziwa kwa nguvu zote na Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Mhe. Naibu Spika, Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, lakini pia na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto huwa tuna utaratibu wa kuwapatia elimu wazalishaji hawa wadogo wadogo.

Kuna vipindi maalum kwa wakati maalum na kwamba tunalifanyia kazi. Kwa hiyo, nawaomba waheshimiwa wafahamu hivyo kwamba serikali tayari imeagiza vyombo vyake hivi ili kuwawezesha wazalishaji wetu waweze kuzalisha mazao yao katika viwango vinavyotakiwa na tuweze kukabiliana na masoko ya Afrika Mashariki na katika soko la *SADC*.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la kutafuta eneo la ujenzi wa jengo la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko nalo limezungumziwa. Mhe. Naibu Spika,

naomba niwajulishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba suala hili nalo kwa upande wa Pemba tayari eneo limeshatengwa kwa ajili ya ofisi, lakini kwa upande wa Zanzibar bado tumo katika kutafuta eneo. Lakini wakati tunatafuta eneo tumeona ni vyema tukahuisha mazingira yetu katika ofisi ambayo tupo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kupitia kwako niwajulishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tayari jengo letu la wizara pale Forodhani limeshafanyiwa marekebisho makubwa sana na inakidhi haja kwa sasa. Kwa hivyo, waondoe wasi wasi kwamba mazingira ya kiutendaji hayaridhishi. Tunajitahidi watendaji wetu wamefanya kazi nzuri sana japokuwa tuna ufinyu wa nafasi lakini ubora wa jengo sasa hivi kidogo ni mzuri ikilinganishwa na hapo nyuma na kwa kweli matengenezo bado yanaendelea.

Mhe. Naibu Spika, katika kuwasaidia wazalishaji wetu suala zima la uzalishaji wa mazao ya kilimo na hasa matunda limejitokeza kwamba matunda yetu hapa Zanzibar sasa yanaharibiwa na wadudu. Wadudu hawa aina ya nzi limezungumzwa sana tatizo hili hapa wakati tunachangia Wizara ya Kilimo na Maliasili. Lakini kwa kuwa matunda nayo tunayaelekeza kuwa ni mazao ya kibiashara basi na katika wizara yetu pia imezungumziwa. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mchango wao na nataka niwaahidi hapa kwamba tayari hili suala tunalishughulikia kwa kushirikiana na Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika, tumezingatia kwa kina sana tatizo hili kwamba wadudu hawa wamerudi kwa kasi na kwa hiyo panatakiwa mkakati maalum. Nataka niwaondoe wasi wasi waheshimiwa kwamba tayari wataalam wetu wanakutana kutoka wizara hizi mbili ili kuona mkakati huo unafanyiwa kazi na nzi hawa wanaondoka na hatimae matunda yetu yatakuwa mazuri na yatakubalika kama hapo mwanzo wakati yalipokuwa yakisafirishwa nchi za nje ili kuliongezea pato taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwapatia wajasiriamali mkopo nalo limezungumzwa. Tunashukuru kwa michango yao waheshimiwa na tunataka tuwaambie kwamba tayari Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika tunalifanyia kazi suala hilo. Kwa sababu suala hili ni la mtambuka hawa wazalishaji ndio hawa hawa tunawashajihisha sote kwa pamoja mkiwemo na nyinyi pia waheshimiwa. Kama wengi wetu walivyosema hapa kwamba wazalishaji wengi ndio wapo huko majimboni kwa hiyo tuangalie utaratibu wa kuwawezesha kimtaji.

Mhe. Naibu Spika, serikali imeliona hilo na ndio maana ikaweka Wizara ya Uwezeshaji. Lakini kwa umuhimu wa suala hili pia kazi hiyo imepewa Wizara ya Kilimo na Maliasili, lakini pia imepewa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kama nilivyosema hapo awali.

Kwa hivyo, naomba niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali imeliona hilo na ndio maana imeweka taasisi hizi kwa pamoja zishirikiane kuona wananchi wetu vijana na wanawake wote kwa jumla wanafaidika na mazao yao yanakubalika. Hatimae wanaweza kutoka hapa walipo sasa kiuchumi wakaweza kuuza mazao yao katika viwango vinavyotakiwa na kukubalika katika masoko sio tu Zanzibar lakini na nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wako pia wamezungumzia suala zima la eka tatu ambazo Mhe. Muasisi wa Taifa letu alizigawa kwa wananchi wa Zanzibar ili kuendeleza suala zima la kilimo ikiwemo zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, tumeulizwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imejipanga vipi kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako kwamba hivi sasa serikali ina mpango wa kuimarisha na kupanda mikarafuu mipya. Hili tumekuwa tukisikia na sisi tuliokuwa tukifuatana na Mhe. Rais katika ziara zake tumekuwa tukimsikia jinsi gani alikuwa akisisitiza suala hili. Kwa bahati nzuri sana tuliwahi kufika kwa mkulima mmoja tukakuta ni jinsi gani ambavyo tayari yeye alikwisha jiimarisha kwa zao la karafuu katika eka karibu 30.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba suala hili la uimarishaji wa mikarafuu na hasa katika hizi eka tatu tatu tunalishughulikia kwa pamoja na Wizara ya Kilimo na Maliasili ili kuona kwamba zao hili la karafuu linakuwa endelevu.

Mhe. Naibu Spika, katika wachangiaji wako pia pamezungumzwa suala zima la maendeleo ya viwanda. Mhe. Naibu Spika, maendeleo ya viwanda serikali imeliona na ndio maana wizara hii ikapunguziwa jukumu la utalii ili kuboresha suala zima la viwanda, biashara na masoko kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, serikali katika kulifanyia kazi suala hilo imeona hapo mwanzo kuliachia kwa sekta binafsi ili waweze kuwekeza katika uzalishaji wa viwanda.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwepo na wakati ule wa mpito wa kubadilika kwa sera za uendeshaji wa uchumi ulimwengu mzima na hivyo ikapelekea serikali yetu pia kuelekea pia katika sekta binafsi. Lakini sasa katika mkakati mpya huu

ambao serikali inajipanga kupitia wizara hii tunafanya mapitio ya sera ya viwanda ili kuona ni jinsi gani viwanda vyetu tutaweza kuvishughulikia vikiwepo vidogo vidogo na vya kati na kati ambavyo ndivyo zaidi tumejielekeza katika nchi yetu.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu wafahamu kwamba suala hilo tayari serikali imeliona na tunawashukuru kwa mchango wao. Kwa kulisisitiza hilo tutayachukua mawazo yao hayo ili tuweze kuyaingiza katika uandaaji wa sera hii mpya ya viwanda ili tuone kwamba hatukwami kama ambavyo wengi wa wawakilishi wameonesha wasi wasi kwamba maadam huko nyuma viwanda havikuweza kuendelea basi huenda na sasa tukaja tukakwama. Kwa hivyo, tutachukua mawazo yao na tutawaomba wasituchoke hapo tutakapokuwa tunawaalika katika vikao kuja kutupa mawazo ili kwa pamoja tuweze kuendeleza sekta hii ya viwanda.

Mhe. Naibu Spika, suala la ukaushaji wa karafuu kwa kweli karafuu ili ziweze kubaki na ubora wake unaotakiwa ni vyema zikaendelea kukaushwa kwa jua. Kwa hivyo, namuomba ndugu yangu Mhe. Panya Ali Abdalla kwamba hakuna mashine za kukaushia karafuu na pia si vyema kwa sababu zitaondosha ule ubora wa zao hili katika soko la dunia. Ila tutaendelea kuboresha utaratibu wa kutumia majamvi yaliyo safi yenye viwango ili karafuu hizo zibaki katika ubora wake badala ya kuzikaushia chini kwenye sakafu au katika barabara za lami.

Mhe. Naibu Spika, zao la mpira nalo limezungumziwa hapa. Zao hili liliachwa liendelezwe na sekta binafsi kwa muda mrefu. Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, naomba niwaarifu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia kwako kwamba wizara inachukua mawazo yao na italifuatilia suala hili kuangalia ni utaratibu gani zaidi utafaa kuufuata katika kuendeleza zao hili la mpira. Kwa sababu ni kweli zao hili lina soko na tutazidi kuwasiliana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ndio wizara mama katika kuhakikisha kwamba tunaweza kuisaidia sekta binafsi ya mpira ili hatimae kuliendeleza kiuchumi na kuona mapato yake yanasaidia serikali yetu na maendeleo ya nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, pia pamezungumzwa kuanguka kwa uzalishaji wa zao la nazi. Kweli Mhe. Naibu Spika, zao la nazi Zanzibar limeanguka kwa kiasi kikubwa bei za nazi zimepanda sana na tatizo hili sote tunaliona. Hapo zamani tunakumbuka kwamba zao hili lilikuwa likivunwa kwa wingi na lilikuwa linachangia sana uchumi wa nchi yetu. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunaomba tuwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hivi sasa kwa kuliona hilo na kwa kuchukua maoni na maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe, basi wizara tutazidi kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na masuala

mengine lakini na uimarishaji wa zao hili la nazi pia nalo tutalizingatia. Tushauriane kwa pamoja vipi tutaweza kuliendeleza tuweze kuona tija yake.

Mhe. Naibu Spika, pia pamezungumzwa suala la matumizi mabaya ya vipodozi, nampongeza sana Mhe. Panya Ali Abdalla kwa kuliona hilo. Ni kweli wengi wa vijana wetu hasa wa kike tumeona wakijiharibu rangi zao za asili kwa kutumia vipodozi. Lakini naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili liliwasilishwa na Wizara ya Afya wao ndio wana Sheria ya Vyakula, Dawa na Vipodozi na kwa hivyo inafanyiwa kazi na wizara hii. Kwa hivyo, ujumbe wa Mhe. Panya kuhusu matumizi mabaya ya vipodozi bila shaka serikali imeshasikia kupitia wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, vile vile pamezungumzwa tena sana suala zima la makontena ya Darajani. Ni kweli kwa karne ya sasa na ulimwengu huu wa sasa hivi pale hapapendezi, hiyo ni dhahiri wala haihitaji tochi. Tunachukua ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe kwamba hapana budi tukae pamoja na wizara inayohusika tuone pale tunapaendeleza ili pawe na maduka ya kisasa ziweze kuendelezwa shughuli za biashara za kisasa kuliko vile inavyofanyika sasa hivi. Kwa hivyo, ni suala zuri na tutashirikiana na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo sekta hii ipo chini yake ili tuone ni jinsi gani tutaweza kupaendeleza pale na zaidi kuwaendeleza wajasiriamali wale walioko pale.

Mhe. Naibu Spika, nataka nipongeze michango yote iliyotolewa kwa jumla ni mizuri. Lakini kuna suala pia linalohusu kuwaongezea bei wale vibarua wanaochuma karafuu. Mhe. Naibu Spika, suala hili tayari tumeshalifanyia kazi katika wizara yetu na nitaomba mstahamili kidogo tu muda si mrefu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atakupeni takwimu halisi jinsi ambavyo wizara imejipanga katika kuwaona hawa wachumaji wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, suala la akinamama wanaolima mwani nimeshalizungumza na kwa wale wanaoanguka katika mikarafuu. Kama tumesikiliza vizuri hotuba ya Mhe. Waziri amelizungumza suala hili kwamba katika kuona karafuu kwa ujumla wake inarudishiwa hadhi yake basi na hawa watakaoanguka kwenye mikarafuu kuanzia sasa wizara itaweka mpango maalum ili waweze kushughulikiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watuelewe kwamba ni kuanzia sasa kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunakwenda lakini utaratibu baadae hapo kati kati ukawa haueleweki vizuri. Kwa sababu karafuu zilikuwa zinauzwa kimagendo kwa hivyo suala hili wakawa wanatupiana wale wanaopeleka magendo likawa halieleweki. Lakini kuanzia sasa wizara itaweka mpango maalum kwa wale wanaoanguka kwenye

mikarafuu ili waweze kushughulikiwa. Kwa sababu tunajua bila ya kufanya hivyo mkakati mzima huu hautokuwa mwepesi. Kwa hivyo, tunachukua michango hiyo ya waheshimiwa na hili tumeshalizingatia na tayari lipo katika kufanyiwa kazi kupitia Shirika letu la *ZSTC*. Kwa hivyo, wanaoanguka mikarafuu wote watawekewa utaratibu maalum katika kuwashughulikia.

Mhe. Naibu Spika, suala moja limejitokeza kwamba tumepewa hapa changamoto ya *Zanzibar Bureau of Standard* ianze kazi haraka. Tunasema hilo tayari tumeshapitisha sheria na tumearifiwa hapa na Mhe. Spika kwamba Mhe. Rais ameshaweka saini. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tukiletewa tu sheria hii wizarani tutaanza kuifanyia kazi mara moja.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa Mhe. Wanu Hafidh Ameir alitwambia kwamba tumelisahau Baraza la Biashara la Zanzibar. Namuomba arejee katika hotuba iliyowasilishwa na Mhe. Waziri hapa katika ukurasa wa 50 kifungu cha 75 Baraza hilo limezungumzwa pale na hatukuweza kulisahau. Tunajua kwamba ni moja katika taasisi ambazo tunashirikiana ili kuendeleza sekta nzima hii ya biashara hapa Zanzibar.

Mhe Naibu Spika, baada ya kumsaidia waziri wangu katika hoja hizo chache, niombe sasa kuunga mkono hotuba hii mimi binafsi lakini na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ninawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu basi na wao watusaidie kwenye kuipitisha, ili hatimaye tuweze kuifanyia kazi, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

MAJUMUISHO YA HOTUBA YA BAJETI YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO KWA MWAKA WA FEDHA 2011-2012.

Mhe. Waziri wa Bishara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukuwa fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati kabisa itokayo katika sakafu wa moyo wangu Waheshimiwa wote waliochangia bajeti hii, michango yao tunaithamini sana na miongozo tutaichukua kwa hali yote tuitekeleze kwa vitendo katika malengo yetu tuliyojipangia kwenye utekelezaji wa kazi za kawaida kwa mwaka 2011- 2012. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wametoa hoja zao nzito kwa hekima na busara za hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru kwa namna ya kipekeea Mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe Salmin Awadh Salmin, mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, pamoja na wajumbe wa kamati yake kwa hutuba yao nzuri iliyotolewa na Mhe. Abdalla yenye kutoa dira, muelekeo, miongozo na maelekezo ambayo yatasaidia sana katika utekelezaji

wa bajeti hii na tunahakikisha katika Baraza hili kuwa miongozo yote iliyotolewa tutaitekeleza kwa vitendo.

Vile vile naomba kuwashukuru wajumbe wote wa baraza hili kwa kuunga mkono hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ya biashara Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2011-2012.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwataja wajumbe wote waliochangia bajeti hii. Mhe. Naibu Spika, waliochangia katika bajeti hii ni wajumbe 26 kwanza kabisa ni:

Mhe. Abdalla Mohammed Ali Makamo Mwenyekiti
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Rashid Seif Suleiman
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Assa Othma Hamad
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Abdalla Juma Aballa
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Abdi Mosi Kombo
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Mussa Ali Hassan
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Mohamme Haji Khalid
Mhe. Ashura Sharif Ali
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Wanu Hafidh Ameir
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Ali Salum Haji
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana wajumbe hao waliochangia pamoja na wajumbe wengine waliochangia kwa maandishi nawashukuru sana nao ni:

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Farida Amour Mohammed

Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa
Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
Mhe. Nassor Salim Ali (Jazeera)
Mhe. Mohammed Said Mohammed

Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana kwa kuchangia kwa maandishi, kwa kweli michango yetu imetupa changamoto na imetusaidia sana katika kuongoza wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende katika hoja za wajumbe ambazo walizitoa, nizijibu ili mambo tuyaweke sawa. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wa Jimbo la Kitope alisema suala la kupanda kwa bei za chakula.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu kwamba serikali imekaa pamoja na wafanyabiashara na kuunda kanuni maalum kwa ajili ya kushughulikia mwenendo wa bei za chakula kwa kujumuisha gharama zote; hivyo wizara itakuwa inatangaza bei hizo kila kipindi na kila inapoktokezea mabadiliko ya gharama. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie wajumbe wote kwamba suala hili la kupanda kwa bei za chakula kuanzia sasa itakuwa sio rahisi tena kama ilivyokuwa mwanzo na nyinyi mtaona, tangu kuanzia mwezi wa Januari mpaka leo chakula hakijapanda bei kimekaa pale pale kwa sababu tumo katika kuziongoza. Sasa hivi kanuni zimeshatoka na bei itatangazwa rasmi na serikali na kwa hivyo itakuwa hakuna kupandisha bei kiholela.

Ujenzi wa uzio pembezoni mwa kiwanda cha maziwa. Kiwanda cha maziwa ambacho kipo chini ya mwekezaji kina mipaka yake ambayo na ukuta wake ambao unajulikana, eneo la mbele la kiwanda hicho ni la wazi na tunaamini kwamba taratibu za utoaji ardhi zimefuatwa na serikali katika kuliendeleza eneo hilo.

Mkataba wa Kiwanda cha Mahonda. Mhe. Makame Mshamba Mbarouk, alitaka mkataba ule nije nao, mkabata huu ninao hapa na akitaka nitamuonesha kidogo dakika tatu kisha niraurudisha. Serikali imeingia mkataba halali baina yake na mwekezaji wa kiwanda cha sukari ambao upo hivi sasa. Suala hili la mkataba huu kwa sasa linashughulikiwa na Kamati Maalum ya Sheria ya BLM, chini ya mwenyekiti wake Mwanasheria Mkuu wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taathima tunaliomba Baraza lako tukufu liipe muda Baraza la Mapinduzi kukamilisha kazi iliyoipa kamati hiyo na kamati nyengine mbili ambazo zinashughulikia masuala ya kiwanda cha sukari.

Mhe. Makame Mshamba Mbarouk sio peke yako unapata shida kuhusu kiwanda cha sukari. Lakini sote sisi tunasononeka kuona kwamba sukari katika kiwanda kile haitoki na hatupendi kuona kunazalisha spiriti na sio sukari. Kwa hivyo, tunaomba utupe muda na hiyo kazi tutaifanya kwa muda mfupi, tumeazimia na wewe Mhe. Mshimba unajua, kwa sababu umeshashiriki katika kikao cha kwanza na vikao vinaendelea na kwa kweli hatua zitakazofaa zitachukuliwa, tukifanya papara yatakujakugeuka mambo ya *Richmond*, hatutaki. Tunataka kutumia sheria, tutumie vigezo na tupata uwamuzi uliokuwa safi na utakaoridhisha pande zote.

Kuhusu kiwanda cha kuwekea mifugo. Mhe. Mshimba mimi nimefurahi sana kwamba una utafiti mzuri na unaangalia vizuri. Kweli tunaelewa kwamba mwekezaji amepewa kiwanda hicho kwa mkataba maalum na tunatambua kutumia kiwanda hicho nje ya makubaliano ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba huo. Kwa hivyo, wizara yetu inazungumza na wizara husika kuona kwamba kiwanda cha mufugo kiwe kinafanya kazi inayokusudiwa na kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano na sio kuweka saruji au kushughulika na shughuli za uzalishaji wa vyakula vya wanyama. Ahsante sana kwa taarifa hii na tumeifanyia kazi kwa kweli haturidhishwi na hali hiyo hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la uchumaji wa karafuu vipi utasaidia wananchi katika masuala ya vifaa kama majamvi, karabai, magunia na kadhalika. Shirika la *ZSTC* lilikuwa linatoa huduma hizo hapo zamani kwa mkopo. Ilikuwa ikiwakopesha huduma hizo lakini bahati mbaya sana karibu wananchi 5,000 walikopeshwa kwa kupitia njia hizi na mpaka mwaka 2006 *ZSTC* ilikuwa inadai zaidi ya milioni 71, ambazo hazikurejeshwa hadi hii leo. Kwa masikitiko makubwa sana tunasema kwamba *ZSTC* haitoweza tena kukopesha masuala ya vifaa kama majamvi, karabai au magunia na kadhalika kwa sababu ni suala gumu la kutokurejeshwa. Lakini wizara chini ya Shirika la *ZSTC* tumeandaa mkakati maalum ambao wafanyabiashara wameshaleta majamvi haya kwa aina zake, tunaziangalia hizo aina ikiwa majamvi hayo yatakuwa na viwango basi tutawaruhusu walete majamvi hayo na vifaa hivyo vyengine wawauzie wananchi tena kwa bei ambazo tutaridhiana pamoja, ili wananchi wapate bidhaa hii kwa bei muafaka na *ZSTC* sio itakayouza vifaa hivyo kama majamvi au karabai, lakini *ZSTC* itashughulikia masuala ya magunia.

Mhe. Naibu Spika, tumeongea na wafanyabiashara wote wanaofanyabiashara Pemba ili kuhakikisha kwamba kipindi chote hiki vyakula vinapatikana kwa wingi tena bila kuongeza bei kwa kutokana na suala la kuongezeka kwa bei ya karafuu. Sisi tunaliangalia hili na tunalichunga kwa tahadhari kubwa sana na tutahakikisha kwamba *Inshaallah* tutaliweza.

Katika suala la bei ya mchumaji wa karafuu Mhe. Mshimba aliuliza suala hili na waheshimiwa wajumbe wengi wameuliza Mhe. Hija Hassan Hija na wajumbe wengine wengi sana wameuliza suala la mchumaji wa karafuu itakuwaje. Serikali inazingatia suala hili na kwa sasa bei ya mchumaji wa karafuu kibarua isipunguwe Shs. 2,000 kwa pishi. Tajiri ana haki ya kuongeza kutoka Shs.2,000 akenda mpaka mbinguni, lakini mchumaji asipunguziwe chini ya Shs. 2,000 kwa pishi.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo naomba nichukuwe fursa hii kutangaza rasmi bei ya makonyo. Makonyo makavu tutayanunua kwa kilo moja Shs. 1,500. Naamini kwamba wananchi wote watafurahia bei hii na watayafanyia kazi makonyo na makonyo yote yatanunuliwa *ZSTC*. Kwa hivyo, tunaomba makonyo yote yasitupwe, hasiharibiwe yapelekwe *ZSTC* kwa kununuliwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliongea kuhusu suala la kujenga vituo zaidi vya kuuzia karafuu. Ndio sisi tutajitahidi kwa kila njia kuongeza vituo vya kuuzia karafuu, lakini tunaomba kuwanasihi wawakilishi wote wawaeleweshe wananchi wetu kwamba vituo hivi ni kwa ajili yao. Kwa hivyo, vituo hivi wavitunze, kwa bahati mbaya ukenda katika vituo hivi utakuta mabati yameng'olewa milango hamna imevunjwa vunjwa, jamaa wanafanya ndio *toilet.* Wafanyakazi wakienda asubuhi mpaka afanyekazi ya manispaa ya kusafisha. Kwa hivyo, hujuma kama hizi zinavyoofisha vituo vyetu. Tuhakikishe kwamba vituo tunavilinda haviibiwi vitu katika vituo vile, vile vile havifanywi kuwa ni vyoo kwa watumiaji, iwe ni sehemu ya kuuzia karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara hii tumejidhatiti kununua karafuu pale ilipo. Mwananchi yeyote ambaye ana karafuu yake yuko nyumbani au yuko kambini, ambayo inazidi kiwango cha gunia tatu basi apige siku 0777410667. Akipiga simu hiyo gari itakuja itamchukua na gari yake ya karafuu na itamuweka mbele kwenye gari bwana mkubwa mpaka *ZSTC* kwa kumuuzia karafuu zake. Kwa hivyo, usione tabu piga simu tutakufuata hapo ulipo, hata kama itabidi tukuchukuwe kwa gari ya punda, tutaita gari ya punda lakini mzigo wako tutakuchukulia mpaka *ZSTC* ukauze karafuu zako. Mkulima yeyote mwenye kuanzia karafuu zake gunia 3 apige simu tu mahali popote tutamfuata na karafuu itanunuliwa kwa bei ile ile inayouzwa karafuu.

Kuhusu upimaji wa karafuu Mhe. Naibu Naibu Spika, nataka niwahakikishie wawakilishi wote na wananchi wote kwamba mizani zote zimeshahakikiwa, wiki mbili kabla ya kuchuma karafuu kama mnavyojua uhakiki wa mizani umo katika wizara yetu ya biashara na wamekwenda katika vituo vyote vya *ZSTC* zimepimwa na zimehakikiwa. Mizani ambazo hazina viwango zimeondoshwa na mizani zote zinazotumika katika vituo vyetu ni sahihi na hazina matatizo

yoyote. Tutaendelea kuzikagua mizani hizo na kuhakikisha kwamba mizani hizo hazichezewi na kuchakachuliwa.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba muwafahamishe vizuri wananchi wetu. Tunapoongea pishi moja unapata kilo moja unusu basi afahamu mwananchi nini maana yake. Kwanza karafuu zenyewe zote ziwe na vichwa, karafuu zilizokuwa hazina vichwa pishi moja hupati kilo na nusu. Kwa hivyo, karafuu iwe na vichwa na wakati wa kupima katika pishi, pishi yako uitikise tikise ili karafuu zako zijae katika pishi, ukifanya hivyo basi karafuu hizo zitatimia kilo moja na nusu. Lakini ukiwa unabandika bandika bila kutikisa basi ukipima mwenyewe nyumbani basi haifiki pishi moja au pishi moja na nusu.

Mhe. Naibu Spika, karafuu ambazo hazina vichwa pishi moja hupati kilo moja na nusu, utapata kilo 1.3. karafuu ambazo ni magwa au kamfiria hata pishi ukiishindiliaje haifiki kilo moja na nusu ni kilo moja na kidogo. Kwanza wananchi suala hili walielewe na sisi hizo pishi tuzielewe yanapokuja malalamiko tuyaulize kwanza haya yamefikia viwango hivyo. Kwa hviyo, mtu ambaye amepima karafuu zake kwa ukamilifu, akafika kituoni akaona kwamba pana mfanyakazi anataka kuchakachua, basi akatae kuuza karafuu zake aziweke pale. Apige simu nambari hiyo 0777410667 kisha mtu huyo tutamshughulikia. Mtu ambaye anata kumdhulumu tutamfukuza kazi hapo hapo. *(Makofi).*

Kwa hivyo, mwananchi asiondoke kituoni mpaka awe ameridhika na mauzo yake anayoyauza katika kituo hiko. Ili kuondosha urasimu *ZSTC* imejipanga kwa dhati ili kuondosha dosari zote za urasimu na ndio maana tumejipanga kuzifuatia karafuu majumbani na makambini. Lakini kumejitokeza tatizo moja, kuna watu wengi wanapeleka karafuu manyalia hazijakauka katika kituo. Akiambiwa karafuu zako hizi ni manyalia hazijakauka. Anasema, haya huyo sasa anaanza usumbufu wake tena. Hatuwezi kununua karafuu manyalia. Tunaomba karafuu zako zianike vizuri mpaka zikauke ziwe msumari kabisa, halafu yake zidondowe zisiwe na majani, zisiwe na mawe na zisiwe na gololi zije pale karafuu safi zipasishwe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Waheshimiwa Wajumbe wote nataka kuwaarifu. Juzi nimetoka kisiwani Pemba, nimetembelea vituo vyote na nimeona hakuna hata mtu mmoja aliyeuza karafuu *grade two* wote ni *grade one*. Mpaka nilipoondoka mimi zote karafuu zilizonununuliwa ni *grade one* hakuna *grade two* wala hakuna *grade three*. Kwa hivyo, mambo yanakwenda vizuri na bei wanatoa nzuri, tushirikiane tulinde magendo ya karafuu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, naye kazungumzia suala la kupanda kwa bei ya karafuu kutapelekea kupanda bei za bidhaa. Mimi nasema kwamba bei

za bidhaa ambazo zimo katika kanuni tutazi-*control*, hatutokubali kabisa bei za bidhaa ambazo ziko katika kanuni zichezewe kwa sababu ya kupanda bei karafuu. Lakini natoa indhari ili tuelewe kwamba iingiapo neema haiingii upande mmoja bali inaingia kwa nchi nzima.

Mhe. Naibu Spika, mimi naondoka pemba naambiwa kikombe cha chai Shs. 400 ndio ulimwengu ndio dunia. Ikiwa anapata mwenye karafuu, apikae chai apate, apikae ugali apate, huo ndio uchumi. Uchumi king'ang'anizi wa kwamba ukae pahala pamoja ni kwamba hakuna suala hilo jambani, uchumi ni lazima uzunguke kila mtu anufaike, hakuna ubaguzi katika suala la uchumi, uchumi ukiingia pahala unafaidisha watu wote. kwa hivyo, naomba hilo tulikumbuke kwamba katika uchumi wa karafuu Pemba zitaingia fedha nyingi na watu wote watatajirika, isiwe mwenye karafuu tu, hata muuza chai, muuza kahawa na muuza tangawizi. Kwa hivyo, huo ndio mfumo wa kiuchumi na lazima tukubali mfumo huo bila hidhi tutakuwa tunakwenda kinyume na uchumi na tutapingana na mawimbi ya bahari.

Kuhusu tawi la *ZSTZ* Dar es Salaam. Naomba nimuhakikishie Mhe. Mshimba na Waheshmiwa Wawakilishi wote kwamba tunafanya mabadiliko makubwa ya marekebisho ya Shirika zima la *ZSTC*. Tunabadilisha sheria yenyewe ya *ZSTC*, tunabadilisha mfumo wote wa *ZSTC*, huu ni ukarabati mkubwa ambao utazingatia matawi yake yote duniani na ikiona kwamba ipo haja ya tawi kuendelea basi litaendelea, haipo haja ya kuendelea basi litafungwa. Utafiti wa kina utafanywa na tunaamini kwamba katika muda mfupi Baraza lako tukufu Mhe. Spika, litapitisha sheria mpya ya *ZSTC* ambayo ni imara itakayoweza kukabiliana na miongozo yote.

Kuondosha Magendo ya karafuu Mhe. Spika. Nimefurahishwa sana na wawakilishi wote isipokuwa mwakilishi mmoja tu. Mimi napenda kusema ukweli, sipendi kuficha ficha. Wawakilishi wote waliochangia na hasa Mwakilishi wa Chonga nampenda sana. Alisema kwamba yeye mwenyewe binafsi atashirikiana na sisi katika kulinda magendo. Lakini wawakilishi wote waliochangia wameyaponda na kuyalaani magendo, isipokuwa Mhe. Mohammed Haji Khalid. Yeye magendo hakuyaponda na aliwahurumia sana wanamagendo wasije wakazama katika bahari.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema wazame wote. hatukubali kuona kwamba kuna watu bado mpaka kiwango hiki bado wanataka kufanya magendo na kuifisidi nchi. Kufanya magendo ni ufisadi zaidi ya ufisadi. Naomba niwashukuru wote mliochangia kwamba mnakubaliana na umoja wa kuhifadhi na kuzuia magendo yasiende katika nchi jirani, ahsanteni sana.

Mhe. Naibu Spika, magendo ya karafuu tumejidhatiti kwanza kwa upande mmoja kuongeza bei na kadiri bei itakavyopanda katika soko la ulimwengu na sisi tutapandisha kama inavyowezekana, ili asilimia ile 80 tuliyotoa ahadi basi ahadi iko pale pale na tukipandisha bei hiyo na bei ya mchumaji vile vile tutampandishia kama tulivyomuahaidi hivi sasa. Kwa hivyo, tunaomba kwamba suala la magendo lazima tulipige vita sote kwa pamoja, mtu mmoja hawezi kupiga vita.

Suala la ulinzi Mhe. Mshimba na Waheshimiwa Wajumbe wenzako mlichangia suala la ulinzi, naamini vikosi vyote vya ulinzi vimepewa jukumu la usalama wa karafuu na wananchi kwa ujumla. Kuanzia sehemu ya masheha, serikali za mitaa, polisi jamii, wawakilishi, wabunge. Kwa hivyo, mnaomba Waheshimiwa Wawakilishi, mjitahidi kadri inavyowezekana tupate karafuu zisiende na magendo.

Kwa taarifa ya wawakilishi wa mkoa wa Kaskazini, mwaka uliopita tumepata karafuu tani 25 tu. Kwa hivyo, nataka wawakilishi muniahidi kwamba mwaka huu Kaskazini tutapata tani 3,000 za karafuu. Mkoa wa Kusini tulipata tani 2,000 mwaka jana, huo ni mfano wa kupigiwa mfano. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa Mkoa wa Kaskazini tushirikiane kwa hili ili karafuu Kaskazini zisitoke. Ukweli usemwe naomba niwe muwazi tufanye kazi ili tuokowe zao la karafuu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman yeye alizungumzia vipaumbele na uchumi hasa katika kuendeleza biashara na viwanda. Serikali imelisikia suala hili na tunaamini ugawaji wa rasilimali katika bajeti zijayo utazingatia zaidi na kwenda sambamba na vipaumbele vya kukuza uchumi.

Kuhusu mfumko wa bei na ghala za akiba kama tunavyojua kuwa sheria ya usalama wa chakula, hivi karibuni wawakilishi katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kila sekta ilipangiwa majukumu yake, ikiwemo wizara yetu kwa mujibu wa sheria hiyo. Kwa hivyo, namuahidi Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili ambayo ndio imepewe majukumu kwa mujibu wa sheria ambayo sote hapa tumeipitisha kuhusu suala la ghala la akiba. Mimi nakubaliana naye kabisa kwamba suala la ghala ya akiba ni muhimu sana na kazi zake ni mbili kama nilivyoeleza.

Kwanza ni kuwasaidia wakulima na pili ni kuvunja mfumko wa bei za bidhaa. Tunaamini kwamba kwa mipango tunayopanga na Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kifupi kijacho, tatizo hili tutaweza kulitatua ipasavyo na tutashirikiana na nyinyi vile vile katika bajeti ijayo mtaona kimefikia kiwango gani, mtatusaidia mawazo zaidi. Kweli kazi tumeshaanza na tunaifanya na ghala la akiba litakuwepo na matumizi ya kilimo yanaendelea na sisi tutafanya

masuala ya *importation.* Kwa hivyo, tushirikiane na ghala litakuwepo *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu urari wa bidhaa. Kwa kweli hili ni tatizo sugu sana, tuna matatizo makubwa sana. Urari wa biashara baina ya Zanzibar na nchi za nje ni mkubwa sana, baina ya sisi na Tanzania Bara ni mkubwa sana. Suala hili linatokana na uzalishaji mdogo tulionao katika nchi yetu. Kwa hivyo, taratibu sera ya mipango tuliyopanga hapa ni kuona kwamba wizara inashughulikia mikakati ya kusafirisha bidhaa ili kuibua maeneo yatakayoweza kupunguza urari wa biashara hasa uwekezaji katika rasilimali za bahari. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tutahakikisha kwamba tunazitumia rasilimali zote za bahari ziingie katika uchumi wa Zanzibar na tuweze kusafirisha bidhaa hizo kupeleka nchi za nje. Sote sisi tunasononeka na suala hili, halitupi raha haya kidogo, kama wewe Mhe. Rashid Seif Suleiman huna raha na hili na sisi vile vile hatuna raha. Lakini tunaamini kwamba ikiwa tutashirikiana basi tutafika pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mizani za barabarani ushauri huu ni mzuri na tutauchukua ili kuangalia uwezekano wa kuufanyia kazi zaidi. Lakini kuweka mizani chini ya bandari ni muhimu zaidi, itaweza kutupa data halisi ya bidhaa inayotoka nchini. Hii vile vile tutaichukulia hadhari na tutaifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha chumvi. Mhe. Naibu Waziri ameshalizungumza, kweli chumvi nyingi ipo, lakini *quality* yake sio nzuri. Hatuna hara ya kuwa tumezungukwa na bahari lakini chumvi inatoka Tanga na Mombasa na kuja kuuzwa Zanzibar, suala hili halipendezi hata kidogo. Kwa hivyo, tunaifanyia kazi na kiwanda cha chumvi cha Wawi pale ni kizuri mimi mwenyewe nimekikagua, tatizo lao ni *dryer* ya kukaushia chumvi. Tutalifanyia kazi ili wapate *dryer* ya kukaushia chumvi ili waweze kusafirisha chumvi yao kupeleka kila pahala. Kwa hivyo, hili hatukulipuuza, tunalitambua, tunalifanyia kazi na kipindi kijacho kifupi mtapata ripoti yake *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu sera ya viwanda. Alizungumzia Mhe. Rashid Seif Suleiman. Ni kweli kwamba sera ni kitu changine, kutunga sera ni kitu kimoja na kutekeleza sera ni kitu chengine. Mhe. Naibu Spika, ni kweli sera ilikuwepo ya tokea mwaka 1998 mpaka 2008, lakini haikufanyiwa kazi na ilikuwa imewekwa kwenye makabati.

Kwa hivyo, mimi nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko imejidhatiti kuweka sera inayotekelezeka, sera ambayo tutakuwa na uwezo nayo ya kuitekeleza na tunamuahidi kuwa tutafanyakazi hiyo vizuri, kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji, ili waje wawekeze katika viwanda wawekezaji kutoka nje pamoja

na wale wa ndani ya nchi yetu. Hivyo, tunamuahidi Mhe. Mjumbe kuwa hili tutalifanyiakazi na wala hatutolikalia kitako.

Utafiti wa kufa kwa viwanda. Mhe. Naibu Spika, ni kweli viwanda vingi vimekufa na utafiti hasa bado haujafanyika, sababu kubwa ni kukosekana kwa mali ghafi za kutosha kwa ajili ya viwanda hivyo na serikali inafanya viwanda, sasa ilikuwa uajiri unakwenda, yaani kiwanda kina wafanyakazi 50 na wanaotakiwa ni 10 ni mambo mengi sana ambayo yalisabishia hali hiyo.

Kwa kweli hii ni rai nzuri na utafiti utafanywa na serikali iliamua viwanda vile kuvibinafsisha, kwa sababu kuvibinafsisha kwa sababu vimekufa kabisa. Kwa mfano, tukiangalia kwenye Maeneo Huru ya Amani vile viwanda hivi sasa vinafanyakazi na vimekodishwa kwa wawekezaji.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Rashid Seif Suleiman tupate nafasi tukatembelee katika Maeneo Huru ya Amani angalau aone zile shughuli ambazo zinafanyika pale, kwa sababu zile shughuli zinazofanyika pale za wawekezaji ni nzuri na zinakwenda vizuri. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Rashid Seif Suleiman pamoja na wenzake wanaotaka kwenda basi twende tukaangalie na ninaamini kwamba watapate ile sura halisi ilivyo. *(Makofi)*

Udhibiti wa maeneo ya viwanda vilivyokufa. Mhe. Naibu Spika, sheria zetu za zinazotumika kwa wawekezaji, kwa mfano Sheria ya *ZIPA* inatoa *incentive* kwa wawekezaji. Kwa hivyo, viwanda vile vilivyokufa vingi walipewa wawekezaji, yaani vilipelekwa *ZIPA* na baadaye wakapewa wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya kweli kuna baadhi ya viwanda baada ya kuanguka pale kama vile vya Usumba na vyengine, basi jamaa walivamia na kujenga majengo mengine ya kuishi pamoja na mambo mengine. Lakini huu ulikuwa ni udhibiti ambao haukuwepo hapo zamani na mimi katika wizara yangu kwa wakati huo sina hata meno ya kuweza kuyarejesha maeneo hayo, kwa sababu tayari yameshajengwa na watu wameshahamia na tayari imeshasahauliwa.

Malalamiko ya wafanyabiashara, Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kwamba wafanyabiashara wana malalamiko yao, tunatambua kwamba malalamiko ya wafanyabiashara yanaendelea na tunaamini kwamba mzigo utakaopita kwenye eneo la Forodha ndani ya Jamhuri ya Muungano unatakiwa utozwe kodi hapo hapo.

Kwa kweli Mhe. Mjumbe suala hili amelieleza kwa urefu kabisa, kwa vile Zanzibar imo katika eneo moja la Kiforodha ndani ya Jamhuri ya Muungano, kutozwa kodi mara mbili ni kubaguliwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar

ndani ya nchi yao. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi inalishughulikia kwa karibu sana suala hili na wala hatuliridhii.

Jengo la ofisi ya wizara Mhe. Naibu Waziri amelieleza hili na ninaamini Mhe. Rashid Seif Suleiman amelifahamu.

Mhe. Subeit Khamis Faki. Kweli miundombinu ya uwekezaji haikufanyika katika sehemu ya Fumba na Micheweni na hii ni kutokana na ukwasi wa fedha. Lakini sisi tunaamini kwamba miundombinu inayohusika katika sehemu hizo tutashirikiana na wizara zinayohusika kama vile Wizara ya Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati, katika masuala ya maji na umeme, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika masuala ya barabara, basi naamini kipindi kinachofuatia tunaweza kufikia malengo tuliyokusudia.

Kwa kweli malengo pamoja na nia tunayo, isipokuwa fedha ni chache tunazozipata ndio inayopelekea mpaka leo hatuyaweza kuyaendeleza maeneo haya. Kwa hivyo, tunaamini kwa kipindi kinachofuatia hiki kweli tumeeleza nguvu zetu zote katika maeneo haya ya Micheweni na tulimuona Mhe. Rais wa Zanzibar mwenyewe alikuja katika eneo la Micheweni na kuliangalia na mimi nilikuwepo. Kwa hivyo, Mhe. Rais ana nia thabiti ya kuona eneo la Micheweni linaendelezwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri maeneo yote aliyoyauliza Mhe. Mjumbe nadhani mineyazungumza kwenye maelezo niliyoyatoa nyuma.

Mhe. Hassan Hamad Omar alizungumzia kuhusu suala la kutobughudhiwa wafanyabiashara wadogo. Mhe. Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haipendi na wala hairidhiki kuona wafanyabiashara wadogo wanapata bughudha za aina yoyote ile.

Kwa hivyo, wizara itashirikiana na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi suala la kubughudhiwa wafanyabiashara wadogo na baada ya kuwabughudhi tutawasaidia ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad alizungumzia kuhusu mipaka ya Manispaa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iko wapi. Mhe. Naibu Spika, wizara inakamilisha Sheria ya Biashara, ambayo ndio itakayokuwa Sheria Mama itakayosimamia masuala yote yanayohusu biashara hapa Zanzibar.

Vile vile sheria itafafanua kwa kila majukumu ya kila taasisi katika kushughulikia masuala ya biashara. Kwa hivyo, suala hili tumeliona na wala si peke yake Manispaa, lakini kuna sekta nyengine mbali mbali ya kiuchumi zinaingilia masuala ya biashara. Mhe. Naibu Spika, ndio maana tukaona kwamba lazima turekebishe Sheria ya Biashara, ili iondoshe msongamano huo na hivyo tunafanyakazi hiyo na *Inshaallah* tutafika pahala pazuri.

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe akae mkao wa kula ikifika wakati wa sheria hii itakapokuja hapa na tunategemea kuja mwaka huu, basi aichangie vizuri sana katika maeneo yote ambayo anahisi yatatusaidia.

Kupatiwa mikopo kwa wajasirimali. Mhe. Naibu Spika, suala hili tutazungumza na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na yeye ndiye atakayetupatia mikopo ya wajasiriamali na sisi tunawaongoza wajasiriamali tutawatafutia masoko pamoja na mafunzo. Kwa hivyo, tutarajie kwa mpango huo wajasiriamali wa Zanzibar watatoka kwenye hali walio hivi sasa na kuweza kupata mafanikio zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Mhe. Assa Othman Hamad kwa maoni yake na tutayafanyiakazi na pia wizara itaendelea kupitia Balozi zetu katika kuvutia wawekezaji. Kwa hivyo, maoni yake Mhe. Mjumbe tunayachukua na tena ni mazuri na wala si ya kuzungumza tu, lakini ni ya kuyafanyiakazi.

Vile vile kuhusu suala la miumbombinu katika Bandari ya Wete. Mhe. Naibu Spika, ni kweli Bandari ya Wete haiko katika hali nzuri, lakini tumo kwenye mpango tunazungumza na wizara inayohusika kuona kwamba Bandari ya Wete, Mkoani pamoja na Chakechake zinaimarishwa, ili uchumi wa Pemba upate kufunguliwa.

Mhe. Rufai Said Rufai kuhusu wafanyabiashara wakubwa wanawakwamisha wafanyabiashara wadogo. Mhe. Mjumbe, suala hilo tumeliona na tunakushukuru sana na wewe kwa kuliona, sasa katika Sheria mpya ya Biashara hili tumelizingatia na utalikuta kwenye michango yako ijiweke tayari ili uweze kuja kuchangia vizuri.

Kwa kweli hili tumelikuta hata hilo suala la kufanya *Sale* basi lazima utumie sheria na sio unaamua asubuhi. Kwa mfano, kitu kilikuwa shilingi 3,000/= unafanya *Sale* shilingi 2,800/= au vyenginevyo, hakuna. Kwa hivyo, lazima tutumie sheria yaani kama unataka kufanya *Sale* kwanza ukaguliwe na uonekane ile biashara yako ulikuwa ukiuza kiasi gani na kwa nini unataka kufanya *Sale*, baada ya kuruhusiwa ndio utafanya *Sale* tena kwa muda maalum.

Mhe. Naibu Spika, pia suala la uuzaji wa bidhaa zisizo na viwango *ZBS*, kama mlivyotaka na sheria imeshatiwa saini na haribu itaanza kazi zake na itazuia masuala yote ya kuingiza bidhaa nchi ambazo hazina viwango.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla kuhusu suala la biashara huria. Kwa kweli biashara huria na kila mtu anaruhusiwa na wala hapa hatuna vibali. Mhe. Naibu Spika, watu wengi wanafikiri kuleta mchele, sukari na unga uwe na kibali. Kwa kweli unachotakiwa ni kufuata sheria tena ziko wazi kabisa.

Kwa mfano, kama unayo leseni ya biashara basi unakwenda kuchukua kibali kutoka Wizara ya Afya, ambayo ndio inayotoa vibali vya kuleta bidhaa za vyakula na kunaweza kuleta mchele, sukari na unga na wala hakuna watu maalum ambao wanapewa na wengine hawapewi.

Kwa maana hiyo, kila Mzanzibari anaruhusiwa kuleta bidhaa zote bila ya pingamizi zozote na wala hakuna watu maalum au wenye Hatimiliki za kuleta bidhaa za vyakula. Mhe. Naibu Spika, kila mtu au kila Mzanzibari anayo haki ya kuleta bidhaa za vyakula na wala sio watu maalum. *(Makofi)*

Wafanyabiashara wakubwa wamelihodhi soko hilo kwa muda mrefu na kudhibiti soko kwa wale wanaohitaji kuingia kwenye soko hili na hivi sasa wanapata tabu kidogo. Lakini tunawaomba wawe wastahamilivu na wawe wajasiri, ili waingie katika soko na kupambana, hivyo tunaamini kwamba wakiingia kwenye soko na kupambana basi wanaweza kufanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, suala la mfumko wa bei. Kwa kweli masuala yote ya kusababisha mfumko wa bei na wafanyabiashara yamezingatiwa na kwenye Sheria pamoja na Kanuni zetu mpya tulizotunga basi yatachukuliwa hatua. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Rufai Said Rufai asubiri kipindi kifupi basi tukitangaza bei za vyakula ukiona bei zinapanda bila ya mpango aje atuambie.

Lakini tunaamini kwamba tukitangaza Kanuni tunazifanyia kazi, tukitangaza bei ya vyakula nayo pia tutaifanyiakazi na mtu yeyote atakayepandisha bei ya chakula kinyume na ile ambayo imetangazwa na serikali itakuwa ametenda kosa na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Bei ya *petrol* hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wa Zanzibar wa *petrol* wanakaa na serikali kwa ajili ya kufanya marekebisho ya bei baada ya kila miezi mitatu na tofauti na mfumo wa Tanzania Bara. Kwa mfano, Bara wenzetu wana mfumo tofauti sana, Mhe. Abdalla Juma Abdalla alisema kule kulikuwa na matatizo haya, lakini sisi na Bara mifumo yetu ni tofauti. Kwa hivyo, usione bei Bara imepanda ya *petrol* na kwetu sisi iko chini ukaona ulinganisha hapana.

Kwa kweli sisi tunafanya marekebisho kila baada ya miezi mitatu na wenzetu wao wanabadilisha bei zao kile dola ikipanda pamoja na mafuta yakipanda katika Soko la Dunia, hivyo Bara na hapa ni tofauti na wala tusilinganishe.

Ahsante sana Mhe. Ali Abdalla Ali kwa msimamo wako juu ya magendo nakupongeza sana na tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote wawe na mfumo kama huo. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mosi Kombo alizungumzia kuhusu Viwanda Vidogo Vidogo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli mitambo imeuzwa na majengo yote yalipelekwa *ZIPA*. Hivyo, hivi sasa kuna viwanda mbali mbali ambavyo vimekaa na kufanyakazi. Mhe. Mjumbe wizara inamuomba ikamtembeze katika eneo hilo kwa vile yeye ni mwanzilishi.

Kwa kweli mimi nakumbuka Mhe. Mjumbe alikuwa kule Viwanda Vidogo Vidogo zamani na ndio maana viwanda vyote anavijua. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe afanye ziara katika viwanda vile na kuona tofauti baina ya pale mwanzo na kule nyuma.

Vile vile kuhusu ombi lake la kwenda Mkoa wa Kaskazini kwa ajili ya kuangalia namna gani tunaweza kuweka viwanda, basi hili tutalifanyiakazi na tutakuja Mkoa wa Kaskazini na atutembeze Mhe. Mjumbe na tuonesha anayo matunda gani tuyaone au samaki tani ngapi na tutamfanyia viwanda kama alivyoomba, kwa sababu sisi tunataka tufanye viwanda. Kwa hivyo, malighafi ipo na tutaweka kiwanda na wala msiwe na wasi wasi. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis tunakushukuru sana. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kushajihisha uwekezaji, viwanda na usindikaji samaki sekta hii imepewa imepewa kipaumbele, tayari wizara hizi mbili zimeshaanza kufanyakazi katika suala la mwani na itaendelea katika suala zima la uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, michango ya Mhe. Suleiman Hemed Khamis pamoja na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kuhusu misamaha ya kodi ya chakula. Kwa kweli naamini mengi sana mengi sana ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa nimeshayajibu na lililobakia ni kuhusu kodi ya chakula.

Katika suala hili nakubaliana na Mhe. Mjumbe aliposema kwamba tunapotoa tahafifu kwa mfanyabiashara ya bei ya chakula je tahafifu ile anaipeleka kwa mlaji? Hili ndilo swali. Kwa hivyo, sisi tunasema kwamba ikiwa mfanyabiashara kweli tukimpa tahafifu ya ushuru na yeye atapunguza bei ya chakula, basi hapo tunaweza kukaa kitako na kuzungumza. *(Makofi)*

Lakini ule mtindo wa kuondosha ushuru na bei ya mchele, sukari pamoja na unga iko pale pale na hili haliwezekani na wala siliungi mkono, hapo ndipo nitakaposema na kuunga mkono. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija alikuwa na hoja moja kuhusu ongezeko la fedha ofisi ya Pemba. Mhe. Naibu Spika, naomba nimfahamishe kidogo Mhe. Mjumbe kuhusu kadhia hii, kweli fedha za mwaka jana ni tofatui na mwaka huu zimeongezeka.

Lakini sisi tunapeleka katika wizara mahitaji yetu, sasa tunapopeleka mahitaji yetu basi tunapewa *ceiling* ya matumizi inabidi upunguze mambo kadha wa kadha, yaani ujihini kama inawezekena ili usipindukie *ceiling* ile. Sasa *ceiling* tuliyoekewa mwaka jana ilikuwa haitoshi, lakini tulikwenda hivyo hivyo na mara hii tukapeleka tena *estimates* zetu na *ceiling* tukapewa nyengine mpya. Kwa hivyo, *ceiling* hii imeongezeka kidogo kwa kuzingatiwa mambo haya yafuatayo:-

(a) Kwanza Pemba tunataka kuajiri *graduate* 7 kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi Kisiwani Pemba;

(b) Wafanyakazi wawili walikuwa wanapokelea mishahara yao Zanzibar walihamishiwa Pemba. Kwa hivyo, kuanzia hivi sasa watapokea kutoka Pemba;

(c) Safari zote za kikazi hivi sasa zitatoka huko Pemba, zamani zikitoka Zanzibar;

(d) Mshahara wa Afisa Mdhamini umeongezeka kwa asilimia mia moja. Kwa hivyo, *definitely* kutokana na sababu hizi matumizi ya Pemba yameongezeka.

Vile vile Mhe. Hija Hassan Hija alisema kwamba kuna fununu au amepata habari kuwa wizara yetu kupitia Shirika la *ZSTC* imeuza karafuu kwa dola elfu 8, pia kuna watu ambao walitoa dola elfu 9, 10 na 12. Mhe. Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe, kwamba kweli tumeuza karafuu tani 1,000 kabla ya kuzichuma.

Kwa hivyo, pia nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe kuwa hatukununua karafuu kwa dola elfu 8, isipokuwa tumenunua karafuu kwa bei kubwa ambayo siisemi na sababu ya kuwa siisemi, Mhe. Spika namuomba Mhe. Mjumbe afahamu kuwa masuala ya bei ya biashara hii ni siri na wala hatuwezi kuitanga hadharani, kwani isasababisha walanguzi watumalize kwa magendo. *(Makofi)*

Kwa kweli mimi siamini hata kidogo Mhe. Mjumbe atakubali awe sababu au kichocheo cha kuimarisha magendo. Lakini nataka nimhakikishie kwamba tumeuza karafuu kwa bei nzuri na ndio maana tukawapa wakulima bei nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, yalaiti tungeuza karafuu kwa dola elfu 8 basi tusingeweza kununua karafuu kwa wakulima kwa shilingi 12,000/=. Sasa kama tungenunua karafuu kwa dola elfu 8 kwa tani, basi tungenunua karafuu kwa wakulima kwa shilingi 8,000/= mpaka 9,000/= na wala tusingekuwa na ubavu wa kununua kwa shilingi 12,000/=. Lakini tunanunua karafuu kwa bei nzuri na ndio maana tumewapa wakulima bei nzuri.

Kwa hivyo, biashara ni siri, kwa sababu mambo kama hayo hayatangazwi hadharani. Hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe anivumilie pamoja na kunisaidia kwa hili kwamba hapakupita aina yoyote ya ubadhirifu katika ununuaji wa karafuu hizi. Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe nimelisimamia ipasavyo suala hili kuhakikisha kwamba hakuna uchakachuaji wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad vile vile kasema vipijamani huyu mnunuaji kapatikana vipi? Wanunuzi ni biashara mwenye kisu ndio mla nyama. Umekuja umetoa bei kubwa kuliko wenzako wote tutakubarikia mzigo na hivi sasa kuna watu wana karafuu tumewaambia nyote leteni *application* zenu.

Hivyo, *application* zote zipo pale ikifika siku tunayotaka kuuza karafuu tutawaambia njoni bei yetu kadhaa, atakaefika bei yetu juu kabisa tutamuuzia karafuu, bei ya chini ende juu, chini, kati, ende Kaskazini hapati, bei ya juu ndiye atakaepewa. Mkakati wetu ndio huo hatumuuzii mtu karafuu anayekuja na bei ya chini, bei ya juu ndiye tutakayemuuzia karafuu.

Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Wajumbe kwamba karafuu tumeuza katika bei ya juu kabisa kwa wakati ule na alitaka nimhakikishie kwamba fedha iliingia namwambia ndio. Fedha imeingia katika *account*, mnunuzi huyu kalipa *advance* na sisi sasa hivi tuna *excess* kutoka kwake ya shilingi 18.6 bilioni.

Kwa nini tukachukua pesa kutoka kwa mnunuzi? Kwanza tufahamu kwamba zao la mara hii angalau Pemba zitaingia shilingi 36 mpaka 40 bilioni, tuwe macho na majambazi, wezi na walanguzi pamoja na matapeli pesa zitaingia nyingi. *(Makofi)*

ZSTC haina maana yake ukifanya biashara hii kwa kifua kipana angalau uwe na shilingi bilioni ishirini mfukoni. *ZSTC* na wala *PBZ* hawana, yaani hakuna. Maarifa, hekima tunazo bilioni 8.9 *excess* ya *ZSTC*. Kwa hivyo, naliomba suala

hili mlifahamu na kwamba hakuna shagalabaghala wala uchakachuaji juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija naomba nimalizie hapo kuhusu hoja yako. Vile vile alisema kwamba Pemba kuna watoto wanaokota mpeta wanapigwa bakora. Mhe. Naibu Spika, nimepiga simu Pemba kuwauliza jamani tayari mpeta umo humo, mbona watoto mnawapiga bakora na huu ni utamaduni, kwamba karafuu zikeshavunwa basi vijana waingia kwenye miti kwa ajili ya kuokota na kupata fedha za Sikukuu, basi waliniambia hapana Sheikh na hivi sasa hakuna mpeta isipokuwa kuna karafuu nzuri msumari. Kwa hivyo, watoto wanakwenda na vibindo vyao na kuchuma karafuu matawi ya chini na kusema mpeta na huo si mpeta. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Naibu Spika nawanasihi wakuliwa wote ukifika wakati wa mpeta, basi waachie vijana kwenye mikarafuu kwa ajili ya kuokota mpeta. Hivyo, nawaambia vijana kwa wakati huu hakuna mpeta na wala wasiende kwenye mashamba ya watu watapigwa na waende baada ya kumaliza mavuno. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwanza hoja yake kubwa vipi Mhe. Nassor Ahmed Mazrui wizara nzima unakaa hapo kufanya biashara kwa shilingi milioni 30 na wewe mwenyewe huoni haya. Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba wizara yetu sisi ni *regulators* tu na wala hatufanyi biashara kusema, kwa hivyo hakuna *any source of income*.

Kwa maana hiyo, *source* ya shilingi milioni 30 inatokana na Kitengo kimoja tu cha Mizani na Vipimo, sasa kitengo hiki wakati tupopima mizani, magari ya mafuta, vituo vya *petrol* na wale tunawa-*charge minimum*, yaani kidogo tu angalau ile ya kuweka akiba, hivyo shilingi milioni 30 zinatokana na suala hilo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe afahamu kwamba hatuna biashara, kwa sababu mimi naamini kama kuna biashara basi ningekutengezeni kiasi cha bilioni 3 mpaka 4 kwa mwaka bila wasi wasi wowote, lakini bahati mbaya hakuna biashara. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza suala la posho la safari. Kwa kweli nadhani Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum), Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wote wameeleza. Lakini nasema mimi hasa ili niwe *comfortable* wizarani kwangu, kwa sababu Wizara yetu ya Biashara ni biashara na biashara ni safari.

Mhe. Naibu Spika, mimi kabla ya kuwa waziri nilikuwa na kikampuni changu kidogo tu pale na Mhe. Mjumbe anakijua, nasafiri mara 15 kwa mwaka. Sasa leo nina wizara nzima, yaani wizara ya nchi nzima yenye uchumi wa nchi nzima, basi siwezi kusafiri hata mara 10 kwa mwaka. Kwa kweli bajeti hii shilingi milioni 237/= na mimi niliona bajeti inayofaa kwa wizara yangu ni shilingi milioni 700/=, lakini kutokana na kwamba hakuna fedha ndio tumepewa shilingi milioni 237/=. *(Makofi)*

Vile vile tukumbuke kwamba kuna mikutano mingi pamoja na makongamano mengi ambayo tunataka tuhudhurie. Kwa mfano, kwanza *World Trade Organization (WTO)* wanatutaka twende kule kwa ajili ya kuzungumza na hivi sasa tumo katika masuala ya *branding*, kwa sababu tunataka kufanya kazi kubwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, pia kuhusu Masoko ya Karafuu, kama vile Marekani Karafuu za Zanzibar wamezigomea na miaka mingi sasa. Kwa hivyo, tunataka tufanyekazi, kwa sababu kule wako *AGOA* na Soko la Marekani tulipate tena, ili karafuu pamoja na mafuta ya karafuu yaende Marekani na ule utata uliokuwepo zamani tuondoshe, kwa kweli zote ni safari tena ni fedha.

Pamoja na hilo tunataka kuhudhurika katika Vikao vya *East African Community*, pia tunataka kuhudhuria kwenye Vikao vya Kanda hii ya Afrika ya Mashariki na Kati ya na *SADC*, kuna Mkutano wa *Indian Ocean Ring*, yaani kuna mikutano mingi sana itabidi tuende, lakini kwa bahati mbaya kutokana na fedha hizi kuwa chache basi hatutoweza kwenda mikutano mingi na labda tutakwenda nusu tu.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Mjumbe kwamba posho hili kwa wizara yangu mimi ni dogo sana na linaniuma sana, lakini sina hila. Kwa maana hiyo, naomba anikubalie kwa sababu hizi si fedha nyingi kwa wizara yangu.

Mhe. Mjumbe, pia ali-complene kuhusu posho ya *entertainment* kuwa shilingi milioni 15. Kwa kweli posho ya *entertainment* shilingi milioni 15 anaziona nyingi na mwaka jana zilikuwa ni shilingi milioni 2. Mhe. Naibu Spika, nimefika pale *all entertainment* nikitoa mfukoni mwangu kwa sababu fedha hapana.

Lakini napenda kumfahamisha Mhe. Mjumbe kwamba katika wizara ambayo ina wageni tena wageni mashuhuri ambao ni wafanyabiashara, hivyo wanapofika pale kama hukuwapa *dinner* au *lunch* hata kama kawaha hukuwapa basi wanakudharau sana na wala si mtu wa maana na si mfanyabiashara. *(Makofi)*

Kwa hivyo, shilingi milioni 15 kwa section ile ni ndogo sana, sasa tufanye nini na wala hatuna vya kufanya, inabidi twende hivyo nitanunua kipolo cha tende na kahawa basi. Lakini hasa *entertainment, you know the meaning of entertainment of business* na sio *entertainment* za kawaida. *(Makofi)*

Nikiendelea na majumuisho yangu sasa nizungumzie kuhusu kipengele cha mishahara. Katika kipengele hiki Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema kwamba Mipango, Sera na Utafiti, Utumishi na Uendeshaji mishahara yote ni shilingi milioni 323,373/= kwa hivyo kuna ongezeko la shilingi milioni 51,292/=. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka kumfahamisha Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu kwamba hii imetokana na muundo wa wizara yetu umebadilika na hivi sasa kuna Waziri na Naibu Waziri pamoja na Wakurugenzi nao wameongezeka. Kwa hivyo, viongozi wawili wameongezeka, Mkurugenzi pamoja na Naibu Waziri pamoja na mishahara ya Mkurugenzi imepanda. *(Makofi)*

Tukienda kwenye viwanda ongezeko la mshahara limeongezeka kutoka 25 kwenda 43. Kwa mfano, Mkurugenzi wa Viwanda mshahara wake umeongezeka, vile vile Sekta ya Viwanda imekufa fofoMhe. Mjumbe na tunataka tuifufue, yaani tunataka tuajiri *innovative and creative graduates* wa watano ambao watakuja kufanyakazi katika sehemu ya viwanda. Kwa hivyo, mishahara yao hiyo itabidi iongeze kasma ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu biashara je, ambayo ilikuwa shilingi milioni 81/= na hivi sasa ni shilingi milioni 106. Kwa hivyo, hapa Mkurugenzi wa Biashara mshahara wake umeongezeka na kwa sababu biashara inataka kushughulikiwa kutokana na sheria mpya inayokuja, ili tufanye kazi zivuri, basi tunataka kuajiri *graduates* watano katika *section* hii, kwa sababu mshahara utaongezeka.

Vile vile kuhusu posho maalum Mipango, Sera na Utafiti shilingi milioni 2 na Utumishi na Uendeshaji shilingi milioni 51. Kwa maana hiyo, posho limepanda na kuwa shilingi milioni 53. Mhe. Naibu Spika, hapa ilikuwa Mhe. Naibu Waziri zamani hayupo na hivi sasa Mhe. Naibu Waziri lazima apatiwe posho, kwa sababu kuna mshahara na posho, sasa hapa imebidi iongezeke.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu viburudishaji tayari suala hili nimeshalitoela ufafanuzi Mhe. Mjumbe. Lakini sehemu ya viwanda viburudishaji imeongezeka kuwa shilingi milioni 3, kwa sababu watu wameongezeka na tunatarajia *investors* wengi watakwenda kwenye uwekezaji wa viwanda hivi sasa ndio tunaweka kiwango hicho. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaomba baada ya kuzungumza hayo uridhike na niliyoyaeleza, ili atuachie tuendelee mbele. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu kupanda bei katika soko la dunia, haina maana kwamba bei hii ipande kwa kiwango hicho hicho katika soko la Zanzibar, kweli katika dunia imepanda asilimia saba, lakini bahati mbaya sana Zanzibar hatuna bahati, kilichojitokeza hapa waheshimiwa wajumbe zamani ilikuwa unga na mchele ulikuwa unakuja kwa kago inakuja meli nzima hapa inateremsha saruji meli nzima, mchele meli nzima tani elfu sita elfu tano, sukari meli nzima. Sasa hivi hakuna tena mpango huo kutokana na huu ugojwa uliopo Somalia pale inabidi sukari tutie ndani ya Makontena, mchele utiwe kwenye Makontena, unga ndani ya kontena kila kitu mpaka saruji ndani ya kontena, imepelekea kupanda bei kwa kago kwa asilimia zaidi ya kumi.

Mhe. Naibu Spika, *Insurance* kutokana na balaa hilo hilo imepanda sana mpaka imefika asilimia ishirini, halafu tena kwetu sisi tuna *problem ya exchange rate* Zanzibar *exchange rate* haiku sawa sawa inapanda haina mpango, kwa hivyo mambo matatu haya yanachangia kupanda bei sana kwa vitu na sisi tumepanga *cost bild up* tunaangalia alivyonunua ulaya, alivyonunua Vietnam, alivyonunua Thailand, au China tunafanya hesabu zote mpaka tunafika chini tunakubaliana faida yako Shs. 3,000 hapana punguza anapunguza, kwa hivyo tunakwenda mpaka tunafikiana bei muafaka. Siku itakayotokezea kule bei imeshuka tutamwita wazee kule bei imeshuka kwa sababu *cost bild up* tunayo na wao wanayo, siku ushuru umepanda tutakaa kitako pamoja, dola ikishuka tunazungumza, dola ikipanda tunazungumza. Kwa hivyo hayo nataka kumfahamisha mjumbe Mhe. Naibu Spika, na wajumbe wengine kwamba wasiwe na matumaini makubwa sana.

Kiwanda cha Zanzibar Milling kweli Mhe. Ismail Jussa Ladhu amesaidia sana kwa sababu laiti kama kiwanda kingekuwa kinafanya kazi basi unga ungezidi kushuka bei Zanzibar, *concern* yake mimi Mhe. Ismail Jussa Ladhu mimi naiunga mkono sana. Lakini suala ni hili kiwanda cha Bakharesa cha Zanzibar Milling jirani yangu pale Mtoni kilikufa hichi kwa sababu gani bandari ilikuwa ikitengenezwa, sasa ikija mali kutoka nje inakuja vile vile wanapampu pale wanatoa nganu inakwenda zake katika kiwanda, lakini muda mrefu bandari ilipokuwa ikitengenezwa kile kiwanda kilikuwa hakina malighafi, ikabidi kiwanda kifungwe wakaondoka na wakakisahau kwanza kabisa.

Sasa basi baada ya mazungumzo na mwenyewe tajiri ambaye ni Mzanzibari mwenye nia ya kusaidia Zanzibar na mwenye nia ya kuwekeza Zanzibar amesema kile kiwanda atakifufua, sasa hivi kiwanda kinafanyiwa ukarabaati mkubwa kimeongezwa mashine za kutosha ili kuzalisha tani 4,500 za unga kila mwezi. Sasa hivi anajenga mbili mpya na kila moja inachukua tani 10,000 ya

ngano, kwa hivyo atafanya kilo 4,500 Zanzibar atabakisha tani 3,000 zilizobakia atasafirisha unga atapeleka Comorro. Kwa hivyo Mhe. Ismail Jussa Ladhu *concern* yako tumeitambua ni nzuri na kwa kweli jitihada itafanyika kuona kwamba kiwanda hiki kinafanya kazi ili ku- *stabilize* suala hilo.

Kuhusu *SIDO* kweli Mhe. Ismail Jussa Ladhu laiti kama Unguja pangekuwa na *SIDO* sasa hivi tungekuwa mbali sana si uongo, lakini basi ingawaje *SIDO* si shirika la Muungano lakini wamekuwa *very gene race* kwetu sisi tunashukuru sana na tunashirikiana nao vizuri, wametusaidia mafunzo ya *food process* wametupatia mafunzo ya kupanda uyoga na *ku-process* uyoga na kila tunapohitajia msaada wanatusaidia hasa mafunzo. Lakini aidia yako tumeichukua na tunafikiria na sisi Zanzibar kuwa na *SIDO* yetu ili isaidie kupata viwanda vidogo vidogo.

Kuhusu bidhaa zilizopitwa na wakati au zilizo- *expire date* naomba nipewe muda mdogo tu *ZBF* ianze kazi, *ZBF* ikianza kazi kadhia yote ya mali mbovu maana yake hapa kuna tatizo moja, anasema kwamba hili friji halina viwango viwango ni kitu mbali na *freege used* ni kitu mbali unaweza kuona friji jipya lakini halina viwango ukiliweka katika plagi linaripuka jipya lakini halina viwango lakini unaweza kuwa na pasi kongwe lakini ina viwango, kwa hivyo viwango si suala la kuwa *used* hata kitu kiwe kipya kinaweza kuwa hakina kiwango, kwa hivyo *ZBF* itafanya kazi hiyo.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa na suala vipi leo Wizara kwa mwaka mzima mmeondosha au kuangamiza mali za *old five million* kweli, lakini wanaoangamiza sio peke yetu sisi tunaangamiza lakini tuna wenzetu kama kodi chakula, madawa na vipodozi ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya nao vile vile wanafanya kazi hiyo hiyo. Tunafanya kazi moja taasisi mbili kwa hivyo ukilinganisha yetu sisi na yao wao utakuta amount ya kuangamiza ni kubwa, lakini udhibiti halisi na mzuri utapatikana *ZBF* ikianza kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hakuna mchezo mchafu wala mchezo mzuri katika suala la bidhaa mbovu, bidhaa mbovu tutazifanyia kazi na mfanyakazi yoyote tutakayembaini anashirikiana katika mchezo mchafu au mchezo mzuri tutamchukulia hatua.

Mhe. Hamza Hassan Juma, ahsante sana sana kwa maelezo mazuri uliyotupa na haya ni mambo ambayo sisi tutayafanyia kazi kwa uzuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, uwanja wa maonyesho ni kweli suala muhimu sana mimi mwenyewe nimekwenda kwenye maonyesho ya saba saba nimeona choyo zile fedha ambazo wanaziingiza, fedha nyingi sana kwa hivyo mimi hasa ndio niliyekuwa chachu ya kuanza yale maonyesho ya Tunguu pale, na mimi ndio

nilikuwa chachu ya maonyesho ya Beit el Ajaibu kwa huvyo nitajitahidi kwa uwezo wote kuona kwamba Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko inajenga maeneo ya maonesho tena ya kimataifa, tena mazuri ambayo yatakuwa bora kwa Afrika ya Mashariki Nzima.

Mhe. Hamza Hassan Juma kasema Shirika la *ZSTC* liwezeshwe nakuhakikishia kuwa Shirika la *ZSTC* litakuwa shirika bora kuliko mashirika yote na tutalifanyia kazi nzito na wewe utakuja kushusha sheria hapa na naamini litafanya kazi nzuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma anasema zile asilimia hamsini wapewe wale jamaa waliokwenda katika maonesho ya saba saba, mimi nasema sio hamsini ni asilimia mia. Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete katoa zawadi ile kwa wale majasiri waliokwenda pale mpango utakaokuwa pale ni wakuzunguka lakini watu wa kwanza watakaofaidika ni wale ambao wamekwenda katika maonesho yale, ni wajasiri kweli wamekwenda pale na wale ndio Mhe. Kikwete aliowaona kwa hivyo nakuafikiri masuala yako moja kwa moja.

Kiwanda cha *Cotex* kweli Mhe. Hamza Hassan Juma kiwanda kile kimekaa kama kibanzi katika roho yangu na naamini Mhe. Machano Othman kinamuuzi zaidi, kiwanda hiki kimekaa muda mrefu pale hakifanyi kazi tumemuita muwekezaji tumeongea nae kwanza ahakikishe analipa madeni yote ambayo anadaiwa, ameshafanya kazi hiyo sasa hivi hadaiwi na mtu sasa tumemwambia atuletee mpango kitita anataka kufanya nini pale, tukiona kwamba shaghala baghala tutamshughulikia. Lakini kaonyesha kwamba ana hamu ya kuwekeza kwa hivyo tumpe nafasi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad alisema shamba la Mtakata *ZSTC* ni shirika la biashara hivyo limekodisha shamba la Mtakata kwa mkataba wa miaka 33 kuanzia mwaka 2002 kutoka Wizara ya Ardhi, kwa hivyo *ZSTC* pale haikuvamia imekodi na imeingia kisheria.

Shirika la magari Mhe. Sali Abdala Hamad samahani sana shirika hili limeshindwa kujiendesha kibiashara, tukiendelea kukaa na shirika hili tutakuta shirika linauza maembe mimi kama Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko sitokubali kuona hivyo, kwa hivyo tunasema kwa uamuzi wa serikali Shirika hili linavunjwa rasmi hivi karibuni.

Kwali matatizo ya umeme yanaathairi viwanda kwa hivyo Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Ardhi ili kuona kwamba suala la umeme linapatiwa ufumbuzi, hakuna umeme wa uhakika viwanda haviwezi kwenda mbele lazima tufanye hivyo.

Mhe. Ali Salum Ali kasema kuhusu wafanya biashara wadogo wadogo wa Maruhubi, wizara yangu ya biashara haipendi kuona mfanya biashara mdogo mdogo au wa kati au wakubwa wanabughuziwa nitashirikiana na Wizara husika kuhusu tatizo la kukabili wafanya biashara hao na kuhusu ujenzi ulioko karibu na Kiwanda cha Maziwa nimeshaeleza, kwamba haya kwangu mimi hayanihusu lakini wafanya biashara wadogo wadogo wote tutawasaidia kwa kila hali.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir anauliza habari ya fidia kwa wanaoanguka mikarafuu, Mhe. Naibu Waziri hapa kajibu vizuri sana lakini mimi nataka nifafanue zaidi, wizara yangu inatambua kwamba watu 237 walioanguka mikarafuu ambao wanadai fidia karibu shilingi milioni 43 Wizara imeshawasiliana na Wizara ya Fedha kuhusu utaratibu wa kufidia kwani *ZSTC* haikuwa na uwezo wa kulipa kutokana na magendo. Hivyo hilo ni jambo kubwa sana la kusikitisha unaambiwa wewe kaskazini nzima kumetoka tani 25 lakini walioanguka mikarafuu 200 wametoka wapi na karafuu hazikuvunwa ndio hapa pana mtihani, ndio maana *ZSTC* ikashindwa kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo naomba muwe wastahamilivu lakini Wizara yetu imejidhatiti kwamba kila mtu ambae kwamba anastahiki kulipwa fidia atalipwa fidia hata kabla ya kuuza zao hili la karafuu, kila mtu atashughulikiwa pale pale inapotokea kama ni fidia au matibabu atashughulikiwa hilo Waheshimiwa msiwe na wawi wasi.

Kuna mwengine kasema hapa kwamba Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini katangaza kwamba karafuu isitoke pahala pamoja na kwenda pahala pengine, nasema mimi Mkuu wa Mkoa huyu namuunga mkono mia kwa mia mvunja nchi ni mwananchi, mvunja sheria ni mwanasheria sisi humu ndani ndio watungaji wa sheria au siyo sasa ikiwa sisi ndio tunaotunga sheria lazima sheria tuzilinde na tuzienzi zifanye kazi yake. Sio mwanasheria ndio mvunja sheria kwa sababu gani Mahakamani anapokwenda mtu na kesi amekamatwa na ushahidi kamili bado jaji akamuachia akasema huyu hana kosa hiyo sheria kaivunjwa mwanasheria au siyo.

Sasa basi naomba nikusomee sheria Mheshimiwa Sheria namba 11 ya mwaka 1985 ambayo imesainiwa na Mhe. Ali Hassan Mwinyi wakati ule akiwa Rais wa Zanzibar inasema hivi.

Sheria namba 3 " No person other then the corporation shall export clove. What the meaning of export for the purpose of section three one export include the creating or transportation of the dry cloves from one area of the country to another without a valid permit issued for the purpose and the reasons for such packing or transportation being cated their rings. Move at cloved prohibited fom number four no person shall move un dried cloves , mother of cloves or cloves, stem from one area to another except with a valid permit.

Huruhusiwi kwa sheria kuchukua karafuu, matende ya karafuu yaani karafuu mbichi, matende ya karafuu mbichi wala makonyo kutoka sehemu moja ya nchi kupeleka sehemu nyengine. Huruhusiwi kusafirisha bidhaa za karafuu kavu kutoka sehemu moja ya nchi na kwenda sehemu nyengine ya nchi seuze kutoa nje ya nchi.

Kwa hivyo hizi ni sheria na mimi ni mwenyekiti wa *task force* nitahakikisha zinafuatwa na zinatekelezwa, nimekula kiapo mbele yenu hapa kwamba nitatekeleza katiba ya nchi hii na sheria zake, sitokubali mtu yoyote avunje sheria aachiliwe akija ni jaji nitamsema kavunja sheria, ikiwa nitamsema kavunja sheria, ikiwa mimi nimevunja sheria nambieni Mazrui umevunja sheria au waziri umevunja sheria, lakini sheria ni msumeno unakata huku na kule. Kwa hivyo Mhe. Mjumbe naomba wajumbe wote msome sheria za karafuu ili tuone kwamba tusitoe makosa au kuwalaumu viongozi wetu wao wametakiwa kutangaza rasmi, kwamba hakuna kupeleka hapa na hapa iwache hapo hapo ilipo mimi mwenyewe nitakuwa kila wiki niko Pemba niambie na nionyeshe. Lakini ni kweli bwana karafuu zikihamishwa ndio magendo yenyewe hayo, haturuhusu mtu yeyote kuuza au kununua karafuu mbichi hairuhusiwi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda.

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Naomba sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie hapo na nasema kwamba nakushukuru wewe binafsi kwa kuwa mvumilivu na kunisikiliza. Vile vile nawashukuru wajumbe wote waliochangia. Naomba kwa heshima na taadhima kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Sasa niwahoji wale waliokubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujamuita Waziri kwa ajili ya kuingia kwenye kupitisha vifungu, kwa kuwa muda wetu ni mdogo sana, namuomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais atoe hoja ili tuweze kuongeza muda tumalize shughuli yetu ya asubuhi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu

hivyo naomba tutengue kanuni na muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji, wanaokubaliana na hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ya kuongeza muda wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko sasa naomba baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 21 - WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0601	Idara ya Biashara	30,000,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	238,400,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Mhe. Waziri kwa kutoa majibu yake fasaha kabisa, katika hoja nyingi za upande wangu mimi takriban zote amezungumza na Mawaziri wengine wangekuwa wawazi kama Mhe. Waziri huyu hapa mambo mengi yangekuwa yanapita bila ya matatizo.

Sasa baada ya pongezi hizo katika masuala yangu kuna suala moja tu ambalo sikulisikia ufafanuzi wake nilikuwa naomba unisadie hilo Mhe. Waziri ili tuweze kuendelea, nilipokuwa nikichangia nilifanya marejeo katika ukurasa wa kumi wa hotuba ya Mhe. Waziri alipozungumzia suala zima la kuendelea kuwepo tatizo la wafanya biashara wa Zanzibar kulipishwa kodi mara mbili wanapopeleka bidhaa Tanzania Bara, nikasema katika maelezo yake yaliyokuwepo pale amesema kwamba kuna huu mfumo ulioanzishwa wa

import delegation dater base lakini nikasema bado haujatoa ufumbuzi wa suala hili kama inavyoonekana mara nyingi humu ndani.

Sasa nilikuwa naomba Waziri katika hili, nilimwambia nilitegemea kama yeye mfanya biashara aje atwambie hapa nini mwelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulipatia ufumbuzi suala hili, kwa sababu kama suala la mazungumzo tu na vikao vya Muungano limeshajadiliwa sana na tumeshaelezwa limeshaamuliwa kwamba litakuwa basi lakini kila siku tunashughudia linaendelea kuwa tatizo. Kwa hivyo naomba katika hili Mhe. Waziri anipe maalezo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Suala hilo aliniuliza kweli nasema kwemba kweli mpaka sasa hivi tatizo lipo, nimeeleza katika majibu yangu kwamba Zanzibar kama ni sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ni nchi moja basi mzigo wowote utakaoteremshwa Zanzibar hautakiwi tena kutozwa kodi ukifika Dar es Salaam, Bagamoyo au sehemu yoyote ya Tanzania na mzigo wowote unaoshuka Dar es Salaam au Tanga au Tanzania Bara ukifika Zanzibar hautoloshwi. Ni kweli mizigo yote ya Tanzania Bara ikija Zanzibari haitozwi kodi mara mbili, kwa hivyo hakuna sababu yoyote ya msingi kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar kupitiwa mara mbili.

Suala hili sio suala geni sote tunalifahamu mimi nafsi yangu nilikuwa mwenyekiti wa Kamati nimeanza kulipigania tangu alipokuwa Marehemu Kigoma Malima, mpaka kaja marehemu Sanare na mpaka leo bado suala hili halijapata ufumbuzi serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu ya saba nimepania kwamba suala hili lipatiwe ufumbuzi wa kudumu. Mazungumzo yatafanyika *very serious* ninachokiomba mutupe muda wa miezi saba au minane badi hatuwezi kutatua tatizo hili, tunaomba mutupe muda ili tulitatua na likitushinda tutawaambia limetushinda. Lakini mpaka sasa hivi bado mwelekeo upo mzuri na watupe muda tulifanyie kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, uongozi wa serikali unabadilika lakini serikali huwa ni ile ile inaendelea suala hili kama alivyosema Mhe. Waziri, limekuwepo kwa muda mrefu sana ilikuepo tokea zama za Marehemu Kigoma Ali Malima, lakini baada ya kuja kipindi hiki kinachoitwa *hamunazation* nakumbuka wakati huo Mhe. Moh'd Aboud Moh'd akiwa waziri wa biashara na kule upande wa pili alikuwepo Iddi Simba lilikuwa linazungumzwa wakati huo Mazurui alikuwa Rais wa Chama cha wafanya biashara, sasa mazungumzo haya Mhe. Mwenyekiti yameshachukua miaka mingi sana. Nadhani zaidi ya miaka thalathini lakini halipati ufumbuzi, sasa mimi nilidhani kuliko Mhe. Waziri kutwambia tumuachia kwa miezi sita mpaka minane na serikali inabadilka uongozi.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba ikiwa bidhaa za Zanzibar zinachukuliwa na *TRA* inayopaswa kuwa ni mamlaka moja kwa pande zote mbili, kwamba zinachukuliwa bidhaa za kigeni na kutozwa ushuru tofauti na vitu vyengine kama hivyo kwamba wakati umefika Zanzibar kama alivyopendekeza Mheshimiwa katika bunge kufanya maamuzi magumu, na ikiwa *TRA* inaibana Zanzibar kama hivyo basi tuifungashe virago kama tulivyoifungasha *SUMATRA* ili hapa Zanzibar ibakie *ZRB* itoze kodi zote za ushuru, halafu kama zitatozwa kule basi zitozwe kweli kama wanavyotozwa nchi nyengine.

Lakini huu utaratibu wa mazungumzo yanaendelea Mhe. Mwenyekiti hautusaidii kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atusaidie, hatuoni serikali imefika wakati kama *TRA* inasaidia kuhujumu uchumi wa Zanzibar tuifungashe virago kama tulivyoifungasha *SUMATRA*,

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, *cunsurn* ya Mheshimiwa muwakilishi haina utata kitendo cha wafanya biashara wa Zanzibar kutozwa ushuru mara mbili mimi nathubutu kusema kwamba kwa mujibu wa sheria ya *custom* ni kosa. Si sahihi hata kidogo kwa sababu sheria ya *custom* inaiweka bandari ya Zanzibar kama ni bandari halali. Kama kuna tatizo tumesema mwanzo kwamba wawachukulie hatua watendaji wao wa *TRA* sio wafanya biashara.

Lakini nataka nimwambie Mhe. Muwakilishi kwamba kuifukuza *TRA* Zanzibar na sisi tutakuwa tunavunja sheria na Mhe. Waziri pale amesema hata yeye hataki kuvunja sheria, *TRA* ni chombo chetu cha Muungano tumekiweka sisi wenyewe Watanzania mimi nadhani Mhe. Muwakilishi atupe nafasi safari hii, madhali tumeshakubaliana katika vikao vya kero za Muungano, pale mwanzo yalikuwa mazungumzo yanakwenda mpaka tumefikia pahali tumekubaliana kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar wasitozwe tena ushuru wanapopeleka bidhaa zao. Hilo tumeshakubaliana kwa hiyo halina utata. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tokea serikali yetu hii ilipoingia madarakani hatujafanya kikao cha pamoja chini ya Makamo wa Rais, tutakapokifanya uwamuzi wetu utakuwa ndio huwo. Tunalimaliza hili kwanza halafu ndio twende mengine. Namuomba mwakilishi atupe nafasi hiyo na tutalifanya kwa niaba ya wafanyabiashara na kwa niaba ya Wazanzibari.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwamba na sitokuwa navunjwa sheria, mimi nadhani wengine wanasema kwamba sumbuko huwa halisumbuki mpaka lipate sumbuko lenziwe. Sasa mara nyengine maneno ya wahenga huwa yanatusaidia sana haya. Kama ulivyosema tungelikuwa tunazingatia sheria tu Zanzibar ingekuwa imeshamalizwa zamani. Shirika la Bandari Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba hii Bandari ni suala la Muungano. Lakini tumeunda sheria hapa tumeanzisha Shirika la Bandari.

SUMATRA ilitumika hivyo hivyo magube magube na Katiba ya Muungano kwamba ihalalike kutumika huku. Tulipoona inatuathiri uchumi wetu tukaifungasha virago ikaondoka hapa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa muungano huu kweli una nia njema siku zote masuala yale yangelikuwa yanazungumzwa na wenzetu wangekuwa wanaheshimu. Kwa sababu suala hili serikali imeshatujibu humu humu ndani kwa kauli iliyotolewa nafikiri na Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwamba suala hili sasa limeshamalizika. Nafikiri hata katika hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais alipokuwa akitoa bajeti yake imo. Tukaona kwamba wamemfikisha pahala kiongozi ambaye tunamuheshimu Makamo wa Pili wa Rais ametoa taarifa ndani ya Baraza ambayo si sahihi. Kwa sababu mpaka watu mpaka leo wanaendelea kutupa takwimu na nyaraka zinaonyesha kwamba watu wanaendelea kutozwa.

Ndio maana nikasema kwamba tumefika pahala tufanye maamuzi magumu. Lakini nataka niheshimu hilo walilotuomba serikali, Mhe. Mazurui kasema, namuheshimu sana Mhe. Waziri wa Biashara na anajua hivyo, Mhe. Omar Yussuf kasema Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo kwamba tuwape nafasi wao.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanachoka mwisho masuala haya kama vile mpango maalum upo wa kudhoofisha uchumi wa Zanzibar katika kila hali. Kwa sababu mwisho ulikuwa upenu wetu ni kwenye magari na huko juzi wamekuingilia magari yakakwama. Sasa mimi nilikuwa nasema kwa sababu ya kuheshimu hilo na sitaki kuurefusha mjadala naikubali hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo. Lakini tukubaliane hapo, wamesema tuwape muda kwamba mwakani mimi nawapa mpaka mwakani katika bajeti inayokuja Mheshimiwa kama suala hili litaendelea kuwa tatizo kama serikali inaogopa kuamua wawakilishi tutaamua.

Baraza hili Mheshimiwa lina sifa hiyo lilifanya hivyo katika mafuta. Sisi hatuogopi kufanya maamuzi. Serikali tunaipa nafasi ikalifanyie kazi na mimi nawapa mwaka mzima mpaka mwakani lakini kama mapaka mwakani suala hili halijapata ufumbuzi Mheshimiwa Baraza lako tukijaaliwa litaamua. Naomba tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii. Mhe. Waziri katika suala la Kiwanda cha Sukari kwa kweli nimsifu amejibu vizuri. Lakini nimeomba tupatiwe mikataba sio mimi hata wawakilishi wa Baraza hili tukufu. Mikataba hiyo itaweza kuwasaidia hiyo tume iliyoundwa ya Baraza la Mapinduzi ili tuangalie kwa mujibu wa sheria na sisi tuwasaidie katika kuchakachua hizi sheria ili wamalize kwa vizuri bila kutupiwa serikali.

La pili kakiri Mhe. Waziri kuwa kiwanda cha utengenezaji wa vyakula imekuwa ghala sasa hivi badala ya kututolea watoto wa vifaranga pamoja na chakula. Naomba Mheshimiwa hatima ya hilo kosa lililotendeka Waziri ananieleza nini ili wananchi wapate kusikia mali yao huko nje.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mshimba cansern yako naifahamu sana na nimekwambia mkataba mimi nnao lakini kwa mujibu wa sheria hii ni *document* ya serikali kwa hivyo mimi ningeomba, Mwanasheria Mkuu yule pale akiniruhusu nikupe nitakupa. Lakini naamini kwamba hii mikataba ina sheria zake. Mwanasheria nakuomba muongozo wako.

Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani ni suala la utaratibu tu kwamba kwenye Kamati hii au Baraza likiwa kwenye Kamati sina hakika kwamba hiyo ndio hatima ya hoja inayotolewa kwamba kuna utaratubu wa kuleta mkataba, tukauonesha au ukasomwa. Kwa sababu kwa mujibu wa kanuni zetu kama taarifa anayoitaka Mhe. Mshimba iko kwenye waraka ambao anaweza akausoma akauelewa than hawezi kutoa hoja au hawezi kutaka maelezo kuhusiana na suala hili. Kama mkataba yeye anataka auone kwa wakati wake anaweza akaonana na Mhe. Waziri akausoma anaona vipengele viliopo. Lakini sidhani katika Kamati hii au Baraza likiwa katika Kamati ya Matumizi.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri utaratibu ulivyo sahihi wa vikao kama hivi ni kwamba mjumbe anapotaka chochote kile kama *document*, kwa hivyo Waziri anaipeleka kwa Spika ile *document* halafu yule mjumbe anakwenda kuiyona kwa Spika. Kwa hivyo Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda aupeleke mkataba kwa Spika, halafu *throw* Spika, ataupata huo mkataba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hebu anioneshe kanuni hiyo inayosema hivyo. Kwa sababu hiki ni chombo cha wananchi nchi ambacho ni haki ya kudai mimi. Sasa naomba kukiona kifungu hicho labda kimepitia miye anisaidie kunifahamisha ni ukurasa wa ngapi.
Halafu la pili nilimwambia Mhe. Waziri hii hatima ya kiwanda kile anaitamka vipi?

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mheshimiwa ni kweli ameeleza kuwa Kiwanda cha Mifugo kinasaruji ndani yake kimekodishwa. Kiwanda hichi kimekodishwa katika upelelezi tumeona hichi kiwanda hakikukodishwa. Hichi kiwanda hawa jamaa wamenunua na serikali ina sheha

zake. Nafikiri Waziri wa Fedha, Uchumi na Maendeleo, atanisaidia kwa sababu hili lipo chini yake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tumemsikia Mhe. Waziri katika majibu yake. Naamini Mhe. Waziri wa Fedha yupo hebu atueleze. Mheshimiwa kutaka *document* ili wananchi wapate kujua uhalali ukoje katika haya masuala ya kulinda mali za wananchi. Hatuna haya ya suala jengine. Mimi ninachoomba Mheshimiwa madhali mwenyewe Mhe. Waziri wa Biashara kama ni kweli umenunua sawa tunakubaliana na yeye lakini je, serikali ina sheha ngapi? Hii pia tunataka tujue Mheshimiwa.

Lakini pamoja na hivyo kuwa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo leo ana hotuba yake hilo moja ajue na ajiandae suala hilo sitoacha nae. Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, namuomba anisaidie Mhe. Mwanasheria katika lile suala ambalo alilolisema na mimi nikawa sikukubaliana nalo, kidogo naomba anielimishe.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa katika vikao kama hivi una mambo mawili kuna Kanuni pamoja na *customs* na *convention*. Sasa *customs* zetu zinavyosema *document* kama hiyo huwezi katika vikao ukaitoa pale pale ukaisoma kwa sababu ya muda. Lakini kilichokubaliwa ni kwamba *document* hiyo unaipelekwa kwa Spika, na hiyo imeshawahi kufanywa. Spika yeye anao uhuru wakati wowote kwa hivyo inapelekwa ile *document* kwa Spika, ukishakuipeleka kwa Spika, mjumbe anakwenda kuchukua.

Sasa anapokwenda kuchukua haina maana kwamba huwezi kuwaarifu wananchi wako. Pale utapata uhuru zaidi wa kutoa *photocopy* wa kufanya nini. Lakini humu mkataba kama ule unakurasa 20 utaweza kuusoma wote hapa. Lakini pale unapokwenda kwa Spika au kwa Mwenyekiti, pale unapata uhuru wa kusoma wakati wowote unaoutaka na hiyo ni mazoea yetu. Hiyo ndio taratibu zetu tunavyofanya za Kibunge na taratibu za Kibaraza la Wawakilishi ambao tumeshawahi kufanya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba ukimaliza utakuja kwa Spika, kuchukua mkataba.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naliomba Baraza lirudie katika Sheria Nam. 4 ya mwaka 2007 Juu ya Kinga Fursa na Uwezo wa Baraza, kifungu Nam. 19 naomba kwa ruhusa yako nikinukuu.

Kifungu Nam. 19 *"Privileges of witness subject the provision of subsection two and three of this section every person sermons to give evidence or to produce any document before the house or committee. Thereoff shall be entitled in evidence or disclosure of any communication or production of any such document to same right in privilege as before a court of law. Realy unless the president otherwise direct in writing no public officer shall refuse to give before the house or the committee thereoff any evidence."*

Kwa hiyo Mheshimiwa naomba kwa sheria hiyo Baraza hili lina haki kamili ya kupewa aina yoyote ile ya *document*.

Mhe. Mwenyekiti: Hicho kifungu anachokisoma tunacho hapa na sheria hii inasema ni Sheria ambayo inatoa fursa na Kinga kwa wajumbe wanapofanya kazi zao na mwahala mwengine. Hapa kifungu hiki kinazungumzia kumwita shahidi. Hapa hatuzungumzii kumwita shahidi. Kwa mfano unapokuwa na Kamati unamwita shahidi kutoka nje. Sasa shahidi huyo ndio atatakiwa atoe hayo aliyoyaeleza.

Lakini hapa tupo katika kamati na ni wawakilishi wenyewe, kwa hivyo kifungu hiki haki *apply* Mhe. Mwenyekiti. Kwa heshima zote namumba mjumbe labda ajaribu tena kutafsiri hii sheria au kumpata mwanasheria akamfahamisha, lakini hicho aki *apply* hapa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mheshimiwa suala la kiingereza linatafsiri namna pana *evidence* sio shahidi tu lakini *evidence* hata *document* ni shahidi. Sisi tunachotaka hapa ushahidi. Ndio maana nikasema vipi Mheshimiwa tulitengua kanuni kando kwa kuongeza muda ili kwa kumaliza shughuli yetu hii.

Mheshimiwa mimi sikutaka lazima anisomee yeye Mhe. Waziri nipate ile fursa na kinga yangu ya kuupata ule mkataba. Hii tukisema kuwa tunamazowea Mheshimiwa sasa mazoea hata mimi nitajenga mazoe leo kwa kusema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nadhani hatujafahamiana, Mhe. Waziri mkataba anao na kakubali kuutoa lakini upite kwa Spika, uje kuuchukua. Hiyo tumeshakubaliana hakuna tatizo. Kwa hiyo tunataka kukubali au kukataa ili tuendelee. Mkataba nitapewa, utakuja kuuchukua utauangalia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sasa ina maana nende kwa Spika, bila ya kuandika maandishi sio, nende nikachukue tu, atakubalia Mhe. Spika.

Mhe. Mwenyekiti: Si tushakwambia. Tunaendelea.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	230,566,000

Kifungu 0501 Idara ya Viwanda

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi. Nilipokuwa nikitoa michangio yangu na mimi niliulizia sana juu ya masuala ya viwanda hivi. Lakini Mhe. Mshimba amezungumza kwenye viwanda viwili cha sukari na cha Chakula cha Kuku. Mimi naulizia kuhusu ile habari ya Kiwanda cha Maziwa, sikumsikia Mhe. Waziri majibu yake alivyokuwa anajibu juu ya suala hili. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anipeyale ambayo niliyahitaji katika kiwanda kile. Nilitaka kujua maendeleo ya kiwanda kile kwamba kimeuzwa au kimekodishwa au utaratibu gani uliotumika pale au serikali nayo inasheha kama hichi.

Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko: Kiwanda cha Maziwa kimeuzwa na kipo chini ya mikono ya muwekezaji, kwa bahati nzuri kiwanda hicho nimekitembelea, nimekiangalia hali yake nzuri bado, suala lake kumbwa hapati maziwa ya kuya *process.*
Nimewasiliana na wizara husika kuangalia angalau wale wapate maziwa lita 8,000 kwa siku. Mpango huo sasa hivi katika Wizara ya Mifugaji na Uvuvi wanafanya mikakati hiyo ya kuweza kuzalisha maziwa angalau kipindi kijacho tupate maziwa kuanzia lita 8,000 kwenda juu ili kiwanda kile kianze kazi. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa Majibu mazuri kwamba kiwanda kile kimeuzwa kwa hivyo muwekezaji mwenyewe anao utaratibu wake wa kukiendesha. Vipi kuhusu lile eneo la pele mbele ya kile kiwanda, lile eneo lote nalo mlimpa au vipi?

Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko: Nilieleza kwamba kile kiwanda kinauzio na kipa mipaka yake. Sehemu ya mbele sio sehemu ya kiwanda. Sehemu ya mbele ilikuwa ipo chini ya mamlaka ya Wizara ya Ardhi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Kwa hivyo suala hili liende kwenye Wizara ya Ardhi, au siyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio utaratibu, tunaendelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwenye suala hili nimetaka ufafanuzi kutaka kujua kuhusu Kiwanda cha Mahonda, serikali vipi imefikia wakati hatuoni maendeleo ya kiwanda kile na badala ya sukari sasa Wazanzibari wanaona uzalishaji wa spriti ambayo ilikuwa ni lengo na malengo ya Wazanzibari. Sasa naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Kiwanda cha Sukari Mahonda hakizalishi sukari. Kwa muda huu kinazalisha lita 6,000 za spriti kila siku. Si uongo ni kweli. Serikali hairidhiki na suala zima la muundo wa kiwanda cha sukari, na ndio maana ikaamua kuunda Kamati tatu kushughulikia suala hili kutoka BLM. Kamati tatu nzito ambazo kwamba zina mawaziri wazito.

Kamati ya Kwanza inaongozwa na Mhe. Ali Juma Shamuhuna ambayo mimi nilikuwa ni mjumbe, Waziri wa Fedha Mjumbe, Waziri Machano Mjumbe na wengine wajumbe, tupo mawaziri saba tunafanya kazi chini ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna, kushughulikia suala hilo katika sehemu ya Mahonda.

Vile vile imeundwa Kamati nyengine ambayo mwenyekiti wake ni mwanasheria mkuu pamoja na Waziri wa Sheria, wanashughulikia suala zima la mkataba. Huo mkataba ambao kuwa anautaka Mhe. MShimba basi unachambuliwa na hao wana sheria, kipengele kwa kipengele. Isitoshe imeundwa kamati nyengine ya Makatibu Wakuu ambao sasa hivi wanafanya kazi. Wamekwenda katika kiwanda kizima kuangalia sehemu iliyolimwa, heka ngapi, mashine mpya zimefungwa ngapi, hata bolti iliyofugwa inahesabiwa mpya na kongwe. Hiyo kazi sasa hivi ndio inafanywa.

Kwa hivyo, uwamuzi utakaotoka mtausikia. Sisi hatutaki kukurupuka, hili ni sula zito sio la kukurupuka. Muwekezaji amekuja, ameekeza fedha zake, ikiwa tutamfurusha kinyume na utaratibu inaweza ikakuletea mashaka makubwa sana. Kwanza inaweza ikasababisha wawekezaji wote wa nje wakatoa tangazo kwamba Zanzibar si pahali pa kuwekeza kwa sababu hapafatwi sheria wala hapana utawala bora.

La pili vile vile huyu muwekezaji ikiwa tutamfurusha bila ya kutumia sheria anaweza akenda kutushtaki tukalipa gharama kubwa zaidi ambayo serikali ikawa ni mzigo mkubwa zaidi tumeipa badala ya kuisaidia. Naomba tuisaidie serikali ili kuona kwamba inafanya kazi vilivyo. Sasa hivi ni miezi miwili tangu ifanye kazi hiyo inaendelea, ikimalizika hapa naamini kwamba mtapata ripoti yote kwenye kadhia ya suala la Mahonda. Serikali hairidhiki na hali halisi ilivyo na ndio maana ikachukua hatua hizo. Kwa hivyo tunakuombeni muwe na subira na haya tunayashughulikia. Kazi mlizotupa ndio hizi kwavyo

tupeni nafasi tuzifanye. Kila kazi ukimpa mtu umpe na muda, kama hampi muda atashindwa kuzifanya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sijaridhia kwa sababu Mhe. Waziri anasema serikali imeunda Kamati tatu, kamati ya Mhe. Shamuhuna kwa niaba ya Serikali, Kamati ya Mwanasheria Mkuu kwa niaba ya Serikali na Kamati ya Makatibu Wakuu pia kwa niaba ya Serikali. Wananchi wanavyohisi serikali hapa imejikwaa na hata tuunde kamati 600 bado kutakuwa hakuna suluhu kwa sababu serikali ndiyo iliyojikwaa.

Sasa nadhani Mhe. Waziri labda atukubalie badala ya kamati hizi tatu za serikali labda sasa tuunde kamati moja ya wananchi kwa maana ya Wawakilishi. Kwa sababu tunahisi hata tuunde kamati ngapi madamu serikali ndiyo iliyotia saini mkataba na ni mkataba wa serikali imejikwa, hakuna suluhu. Labda wangetukubalia wananchi kwa maana ya wawakilishi tukaunda kamati tukawasaidia juu ya hili. Kama atakubali hilo tuendelee.

Mhe. Manasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mhe. Hija, fikra zake kwamba serikali inapojikwaa basi haiwezi kusimama tena ikaangalia hatua gani muafaka za kuchukua. Lakini katika suala hili ni suala la mkataba na iliyoingia mkataba ni serikali. Kama ni serikali ni wajibu wake kuangalia hata hilo analolisema yeye kama ilijikwaa ilijikwaa wapi? Ndio inachofanya sasa hivi. Na itakapoona kama imejikwaa kazi yake kama ni sehemu moja.

Serikali inapoingia kwenye mkataba haiwi serikali, haina hadhi ya kwamba ni serikali. Inakuwa sawa sawa na ule upende mwengine wa mkataba. Kwa hivyo ni wajibu wake kujua wapi na hatua gani ichukue baada ya hapo. Kama ni kukatisha mkataba basi itabidi ikatishe mkataba.

Kamati ya Baraza hata ikiundwa haiwezi ikaja ikatoa maelekezo kwa serikali kwamba lazima ikatatishe mkataba, bila ya kufuata utaratibu. Ni lazima ipite mle mle ambamo serikali itapita kwamba kwa sababu kipengele hiki kwa sababu ya matatizo haya basi tunashauri mkatishe mkataba. Lakini kamati yenyewe haitokuwa na uwezo wala Baraza hili halitokuwa na uwezo wa kukatisha mkataba. Itakayokuwa na uwezo wa kukatisha mkataba ni serikali baada ya kuona wapi kuna tatizo na ichukue hatua hizo.

Mimi nadhani inachofanya sasa hivi serikali ni hatua sahihi na haiwezekani kuchukua hatua za kukatisha mkataba bila ya kwanza kufanya tathmini ya huo mkataba wenyewe ukoje na baadaye ndiyo ichukue hatua. Kwa hivyo anachotaka Mhe. Hija tufikie kwa kupitia Kamati, ndio kile kile ambacho serikali itakifikia kwa kupitia taratibu zake za ndani. Kwa sababu ndio iliyoingia kwenye mkataba, serikali yenyewe ndio wa kwanza kuhakikisha

kwamba inachukua hatua hizo lakini baada ya kupitia taratibu. Kwa hivyo sioni kwa hili kama kuna haja ya kuunda kamati ya Baraza wakati serikali inashughulikia jambo hilo hilo na ndio yenye wajibu wa kushughulikia jambo hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sipingani na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Wazo langu ni kwamba serikali siku zote inawajibika kwa wananchi na wananchi milioni moja laki tatu ndio sisi humu wajumbe 81. Sasa serikali ikiwa imeunda Kamati tatu, mimi nilitegemea kamati ya Mwanasheria Mkuu ingelikuwa ndio top ya Kamati kwa sababu ndiyo inayojua mambo yote ya kisheria.

Lakini bado tunaendelea kuunda kamati nyengine, keshokutwa mtatwambia tuunde Kamati ya Wakuu wa Mikoa na Masheha, bado tunapoteza mali ya serikali. Wananchi hawa ndio watakaosema kwamba serikali imejikwa kwa hivyo kuna uzembe na nani anastahiki kuwajibishwa. Lakini kwa speed hii ikiwa Mwanasheria Mkuu kamati yake imekwenda bado imeonekana haijatosha, tunapeleka Makatibu Wakuu, keshokutwa Wakurugenzi, nadhani mwenyekiti fedha za umma zinapotea ovyo, pengine ni kwa sababu ya uzembe wa mtu mmoja.

Lakini tukiwapeleka wananchi hawa ndio watasema nani anafanya uzembe. Wananchi wanashauri mengi Mhe. Mwenyekiti. Sisi kama wananchi tunaweza tukaishauri serikali na wawekezaji kwamba jamani hapa tumalizeni. Hatuamini kwamba muwekezaji ana tatizo na serikali iivumilie. Sisi imani yetu kwamba serikali imejikwaa ndio maana muwekezaji akaachiwa. Kama muwekezaji anatatizo serikali isingevumilia, mimi naamini hivyo. Atakayejua serikali imejikwaa ni mwananchi ambao ni wawakilishi.

Nadhani kama kawaida ya serikali haikubali kuunda tume lakini mujizoeshe sasa kuunda tume. Ama mufanye mambo yenu ya wananchi kwa umakini au muturuhusu wananchi tuchunguze. Haiwezekani kwamba serikali ina mawaziri na waziri husika wa sekta ile, Mwanasheria Mkuu ameunda tume haiwezekani hadi hii leo iwe hatujaona ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasisitiza kuna haja ya kutupeleka tukaona Kiwanda kile hakina uzalishaji na wananchi wanaendelea kuhoji. Sisi kama tupo kwa niaba ya wananchi. Mwanasheria Mkuu nadhani mtupe nafasi tuwasaidie kuliko kujichunguza wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka kwanza Mhe. Hija, mdogowangu afahamu kwamba hizi kamati zilikuwa zina majukumu tofauti.

Kamati ya Mhe. Shamuhuna ilikuwa ina jukumu la kuongea na wananchi na kusikiliza maelezo ya wananchi. Tumefanya kazi vizuri, tumeongea na wananchi wamewasikiliza *concern* yao na tumewasikiliza nini muelekeo ambao wao wengependa tuende. Lakini vile vile nataka nimwambie Mhe. Hija, mdogo wangu, hawa waliokwenda ni mawaziri lakini na wao ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hivyo sisi tumekwenda pale tukiwa ni wawakilishi wa wananchi lakini ni serikali.

Kamati ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wao kazi yao ilikuwa ni kuutazama mkataba, mkataba ule muwekezaji ameuvunja katika eneo gani ili tunapokwenda tukimwambia sasa ondoka, basi aweze kuondoka bila matatizo. Kwa sababu mwekezaji tumemkodisha kiwanda kile kwa ajili ya kutengeneza sukari, sasa yeye hatengenezi sukari, ndio tatizo letu hilo. Mhe. Mwenyekiti, hili ndio tatizo letu kwa nini hatengenezi sukari yeye anatoa sababu zake na sisi tumemwambia mkataba wetu utengeneze sukari. Mhe. Mwenyekiti, tunaangalia jinsi ya kumuondoa kwa kupitia mkataba huo huo aliyotilia saini. Kwa hivyo, kama Mhe. Hija anataka kujua tatizo ni hili, angelikuwa mwekezaji huyu anatengeneza sukari ingekuwa hatuna tatizo naye.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kumbe tatizo mwekezaji amevunja mkataba aliambiwa afanye sukari yeye anafanya *spirit* na bado serikali wanambembeleza, hilo ndio tatizo ambalo tumejikwaaa. Kumbe tatizo yeye ameambiwa fanya sukari uwasaidie wa Zanzibar yeye anatufanyia ulevi na madawa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu wewe ndiye mwenye uwekezaji labda wananchi wanataka uwambie lini huyu jamaa ama atajirekebisha au atatuachia kiwanda chetu tuendelee na sukari.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Hija mdogo wangu hizi ripoti zetu kwa sababu lazima tukubali hata kama yule unaona anavunja yale makubaliano lazima uangalie katika mikataba yetu kipengele cha kumuondoa, vyenginevyo akikupeleka Mahakamani mnaweza nyinyi ndio mkamfidia yeye. Kwa hivyo, mimi nataka nimwambie kwamba hizi ripoti tunazijumuisha sasa tukishakuzijumuisha patakuwa na maelekezo pale katika ripoti zetu na tutatoa sisi taarifa ya serikali kuhusu mwekezaji huyu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa na sikusudii kuchelewesha wakati unajua sisi tupo hapa kwa niaba ya watu, lakini mara nyengine atupe muda kwa hivyo siku nyengine atupe muda ili tuweze kulielewa jambo hili.

Kifungu 0501	Idara ya Viwanda	181,460,000

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sina kubwa ila nataka kutoa tahadhari tu ndogo juu ya zao la karafuu. Kama nilivyokuwa nachangia nikasema kwamba uondoshwe urasimu, lakini urasimu wenyewe sasa umekuwa wa hatari kidogo. Kwa hivyo, naomba wizara pamoja na serikali kwa jumla ichukue tahadhari kwa sababu nchi yetu tumekubali kwenda pamoja na utawala bora na haki za binadamu.

Kwa hivyo, kweli tunazuia usafirishaji wa magendo wa zao la karafuu, lakini kuna taarifa ambazo tunazipata zinazoonesha kunaanza *over reaction* kwa baadhi ya viongozi. Kwanza kuna taarifa kwamba watu wakionekana na jamvi la karafuu lilokwishakuwa linakauka karafuu zile zinakunjwa na sheha zikapelekwa polisi. Mhe. Mwenyekiti, hili si jambo la kawaida nadhani tungeimarisha ulinzi, tungeimarisha taaluma ya imani kwa watu kuipenda serikali yao na nchi yao, lakini tusi-*over react* tukavunja haki za binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, pili kumejitokeza baadhi ya masheha ambao tunawajua wengi wana Manaibu wao kutokana na maeneo ambayo wanakaa. Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya masheha wamekuwa wakitoa shindikizo la wananchi kuwafuata hata kama anakaa wapi bila ya kutumia Naibu Sheha na maeneo mengine ni makubwa na yatasababisha kuuzwa hizi karafuu kwa magendo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba huu urasimu uliopo uwaondoshee na uzia wananchi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mhe. Rashid ni mzuri na ninauchukuliwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyokwambia langu ni hilo tu naomba tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia suala la karafuu kuna taarifa kwamba waheshimiwa na wao huwa wanashiriki katika kusafirisha hayo magendo ya karafuu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri haoni kwamba kuna sheria ya mwaka 1970 imefutwa sheria hiyo, kwa hiyo haoni haja sheria hii ambayo inaambatana na kifo kwa nini wizara yake isituandalie na ikatuletea ili kuondoa kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, wazo la Mhe. Mshimba gumu kidogo sisi tunaamini kwamba sheria ambazo sasa hivi zipo ni sheria nzuri na ni sheria ambazo zinakidhi haja. Kwa hivyo, tungeomba kwamba atuache tutumie sheria hizi hizi tulizonazo sasa hivi mpaka hapo

mbele, lakini kwa sasa hivi sheria hizi zinakidhi haja na hatuna haja ya kubadilisha sheria.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Mwenyekiti, nataka kuongezea majibu ya Mhe. Waziri kwa hoja ya Mhe. Mshimba kwamba nadhani alilouliza yeye ni suala sio hoja yake aliyoitoa wakati akichangia. Lakini pamoja na hilo ni kwamba sheria anayosema ya mwaka 1970 sasa hivi haitumiki, sheria inayotumika kwa masuala yote ya karafuu na makosa yake ni sheria Nam. 11 ya mwaka 1985 ambayo haina adhabu ya kifungu na haimlindi wala haimuheshimu mtu yeyote kwa jina lolote awe mheshimiwa au mtu wa kawaida ile inazungumzia *any person* na haina *privilege* wala haina *protection* wala haina haki maalum kwa wengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mshimba kama ana ushahidi kuna mheshimiwa yeyote amefanya kosa chini ya sheria hii ana wajibu yeye kama mwakilishi ambaye ana haki ya kulinda sheria za nchi kuripoti suala hilo katika vyombo vinavyohusika na hatua zitachukuliwa. Lakini nadhani sio vizuri kusema kwa dhana ni vizuri tukawa na ushahidi na ninamuhakikishia hatua zitachukuliwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mewnyekiti, mwalimu wangu huyu Mwanasheria lakini sasa nilipochangia mimi nilimsifu sana Mhe. Waziri kwa suala la ulinzi. Kwa hivyo, hoja niliyofikiria kuwa nina uwezo wa kusema kwamba hoja hiyo kuna sheria kwa kuweka ule umadhubuti wa ulinzi ndio nikasema kuna sheria ya mwaka 1970 imefutwa. Lakini je, hatuoni haja tukairejesha ile ili kwa kukomesha magendo. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kuhusu karafuu nilisema kuwa zamani kulikuwa na vituo vingi sana na watu walikuwa hawana tabu kuuza karafuu zao sasa vimevunjwa. Na kwa makusudi kabisa nikaomba kwamba kituo cha Uondwe Mtambwe Kaskazini kwenye watu wengi wanaozalisha karafuu kuliko wote katika Jimbo la Mtambwe kilivunjwa na nikaomba kijengwe tena kwa maslahi ya serikali yetu. Pia kwa sababu hapo Uondwe na Daya haipunguwi kilomita nane vyenginevyo itabidi watu wasafirishe karafuu zao kwa kupitia baharini na njia ambayo sio nzuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sikuiona hatua yoyote aliyoizungumza Mhe. Waziri kuhusu urejeshwaji wa kituo kile haraka inavyowezekana sawa sawa na Ngomeni ambako mheshimiwa ndi alikokuzungumza.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, namuahidi kwamba kituo cha Uondwe kitajengwa.

Kifungu 0601	Idara ya Biashara	255,397,000

Kifugu 0701	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	556,177,000
Kifungu 0702	Baraza la Biashara Zanzibar	200,000,000
Kifungu 0703	Mamlaka ya Mizani na Vipimo	200,000,000
Kifungu 0704	Kamisheni ya Kusimamia Ushindani wa Biashara	250,000,000
Kifungu 0705	Mamlaka ya Viwango Zanzibar	

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nazungumza kuhusu biashara iliyokuwa haina ubora yaani vipodozi, nikasema kwamba biashara hii aidha iwe inawekwa maandishi ya Kiswahili kwa sababu watu wetu wanunue ili wapate kujua natumia vipi na hii haitoniathiri. Kwa sababu dawa zile zinakuja tu lakini wale wauzaji waweke alama kwamba hii ina maana fulani, sasa mtu yeyote atajua kwamba hii dawa anakwenda kuitumia vipi. Kwa hivyo, naona sikupata jibu sahihi, naomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, namueleza Mhe. Mwanajuma suala la vipodozi liko Wizara ya Afya kule ndio kuna hiyo Bodi ambayo ni ya Chakula, Madawa na Vipodozi. Lakini hata hivyo kwa sababu sisi ni serikali tuseme kwamba tunashajihisha sana waletaji bidhaa wajaribu vitu kama hivyo vina *chemical* kali watumie lugha ambayo kwamba inaeleweka.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0705	Mamlaka ya Viwango Zanzibar	250,000,000
	Jumla ya Fungu	**2,362,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 21 – WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0601	Idara ya Biashara	300,000,000
	Jumla ya Fungu	**300,000,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha za wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale waliokubaliana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ya mwaka 2011/2012 wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 7:45 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirejea)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunategemea kuendelea lakini naona wajumbe wako kidogo mno. Lakini hata hivyo, kwa kuwa wajumbe wapo *around* hapa tunawaita waingie ukumbini haraka ili tuweze kuendelea na shughuli yetu. Naomba basi nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waingie ndani ili tuendelee na shughuli hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kuzingatia Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mhe. Spika awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehema kwa mara nyengine tena kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima na afya njema wakati tunakaribia kukamilisha kikao cha bajeti ya kwanza ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Aidha, napenda nimshukuru kwa kipekee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake imara ambao katika kipindi kifupi tumeanza kuuona.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sasa inaundwa na idara kumi na moja pamoja na kusimamia taasisi tisa zinazojitegemea na taasisi tatu za kifedha za Muungano zenye ushirikiano wa karibu na ofisi yangu. Taasisi tano zilizo chini ya ofisi yangu. Taasisi hizo tano zinapata fedha zake kwa njia ya ruzuku.

II: MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeendelea kuwa na majukumu makuu yafuatayo:

1. Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya kitaifa, ikiwemo DIRA 2020, MKUZA na Mkakati wa Kukuza Uchumi;
2. Kusimamia taarifa za ukuaji wa uchumi wa nchi;
3. Kuandaa mikakati ya kuongeza mapato ya serikali;
4. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali;
5. Kushajiisha upatikanaji wa misaada na mikopo katika kugharamia program na miradi ya maendeleo;
6. Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
7. Kusimamia deni la serikali;
8. Kusimamia ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu; na
9. Kusimamia mali za serikali.

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina majukumu ya kitaifa na yale ya kisekta. Utekelezaji wa majukumu haya ya Ofisi unaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010, DIRA ya Maendeleo ya 2020, MKUZA II, Malengo ya Milenia pamoja na maelekezo mbali mbali ya Baraza la Mapinduzi na miongozo ya Baraza la Wawakilishi, ikiongozwa na Katiba ya nchi, Sheria za Kodi, Fedha, Manunuzi, Mitaji ya Umma na Uwekezaji nchini.

III MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2010/11

Mhe. Spika, pamoja na kuwa ofisi yangu ni msimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, bado ina jukumu la kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya ndani ya ofisi kama zilivyo wizara nyengine. Katika kipindi cha mwaka 2010/11, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 3.24 bilioni kutoka vianzio vya ofisi hii, ambapo hadi kufikia Juni 30, 2011, ofisi ilikusanya jumla ya Shilingi 5.63 bilioni sawa na asilimia 174.0 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, kwa mwaka 2010/11 Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 92.505 bilioni, kati yake shilingi 23.834 bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida, Shilingi 23.671 bilioni kwa kazi za maendeleo na Shilingi 45.00 bilioni matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya Shilingi 23.671 bilioni ambazo zilitengwa kwa kazi za maendeleo, Shilingi 10.447 bilioni ni mchango wa serikali na Shilingi 13.224 bilioni zilikuwa ni Ruzuku na Mikopo kutoka nje.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wake, ofisi imeweza kutumia jumla ya Shilingi 32.62 bilioni. Kati ya hizo shilingi. 23.77 bilioni sawa na asilimia 99.7 kwa kazi za kawaida na Shilingi 8.58 bilioni kwa kazi za maendeleo. Aidha kati ya 8.85 bilioni za kazi za maendeleo, Shilingi 4.62 bilioni ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 37.3 na Shilingi 4.24 bilioni ni mchango wa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 32.1. Matumizi ya Shilingi 41.86 bilioni yalifanyika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 93 ya makadirio ya mwaka 2010/11.

IV UTEKELEZAJI WA MALENGO KI-IDARA KWA MWAKA 2010/2011 NA MWELEKEO KWA MWAKA 2011/2012

A. URATIBU WA MIPANGO, UCHUMI NA MAENDELEO YA SEKTA

Mhe. Spika, kufuatia kuanza kwa utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba, wizara imeundwa upya. Mambo mawili makuu yaliyojitokeza ni kwanza wizara kuwa chini ya Ofisi ya Rais na pili ni Mipango ya Maendeleo kupewa uzito mkubwa zaidi. Kutokana na muundo huu mpya wa ofisi yangu, serikali imo katika hatua za kuiunda upya Tume ya Mipango ili iweze kutekeleza na kusimamia vyema mipango ya nchi. Kwa sasa mapitio ya Sheria, Muundo na Majukumu ya Tume yameendelea kukamilishwa. Tume inatarajiwa kuwa chemchem ya mawazo ya Mipango na Maendeleo (*Think Tank*).

Mhe. Spika, Pamoja na kwamba muundo sahihi wa Tume ya Mipango bado kukamilika na kuidhinishwa na serikali, zipo idara ndani ya Ofisi ambazo majukumu yake yatasimamiwa moja kwa moja na Tume hio. Idara hizo ni Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini, Idara ya Kukuza Uchumi, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, wakati mageuzi ya tume yakiendelea, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Mipango ilisimamia idara nne zinazoratibu shughuli za mipango na

uchumi kitaifa. Kwa pamoja idara hizi zinasimamia Mipango ya Taifa na Maendeleo ya Kisekta, utekelezaji wa MKUZA, ukuaji wa uchumi, maendeleo na mipango ya watendakazi, idadi ya watu na maendeleo yao nchini, pamoja na usimamizi wa ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu nchini. Maelezo ya utendaji wa kila idara kwa mwaka 2010/2011 na mpango kwa mwaka 2011/2011 ni kama hivi ifuatavyo:

A.1 IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango ya kitaifa, programu na miradi ya maendeleo pamoja na kufanya mapitio ya sekta mbali mbali kwa kushirikiana na sekta husika. Aidha, idara hii ilikuwa ikiratibu utekelezaji wa miradi midogo midogo ya wananchi Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 182.098 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 5,488.81 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/11, Idara:

i. Ilisimamia ukamilishaji wa utayarishaji wa MKUZA II, pamoja na kuratibu kazi za mapitio ya DIRA ya maendeleo 2020 na kutayarisha Mpango Mkuu wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUZA II, imeimarisha Tume ya Mipango na kuandaa ripoti za mapitio ya kazi hizo ambazo kwa sasa zipo katika hatua za mwisho kukamilika; na
ii. Imeandaa Ripoti za mapitio ya kazi hizo ambazo kwa sasa zipo katika hatua za mwisho kukamilika;na
iii. Imeandaa na kusambaza vitabu vya mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/11 pamoja na mwelekeo wa hali ya uchumi na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/12.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo maafisa mipango na Waratibu wa Miradi, Idara iliandaa mafunzo ya uendeshaji wa shughuli za miradi (*Project Cycle Management*), ambapo maafisa 75 Unguja na Pemba walishiriki. Mafunzo haya yamesaidia katika kuibua na kuandaa miradi ya maendeleo. Aidha kupitia MKUMBITA kazi ya mapitio ya tozo kwa wajasiriamali wadogo imekamilika. Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, idara ilitumia Shilingi 179.161milioni, sawa na asilimia 98.4 kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,854.425 milioni, sawa na asilimia 33.8 kwa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara imekusudia:

i. Kukamilisha ripoti za mapitio ya DIRA ya Maendeleo ya 2020, na uimarishaji wa Tume ya Mipango;
ii. Kukamilisha Mpango Mkuu wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa MKUZA II;
iii. Kuratibu utekelezaji wa Mipango ya kitaifa, program na miradi ya mendeleo;
iv. kuaandaa Mpango wa Utekelezaji wa MKUZA II na Ripoti ya Utekelezaji wake kwa mwaka 2010/2011;na
v. kuendelea kusimamia utekelezaji wa program za MKUMBITA, *UNDAP* na *MCC*.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, idara inaombewa jumla ya Shilingi 262.97 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 23.651bilioni kwa program tatu na miradi miwili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo zimo shilingi 17.700 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa *program* za *UNDAP* itakayotekelezwa na sekta mbali mbali.

A.2 IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe. Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi ina majukumu la kufuatilia na kutathmini mwenendo wa uchumi wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi unaolenga katika kukuza uchumi mpana unaonufaisha masikini. Kadhalika, idara inatathmini na kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Milenia (*MDGs*) na Dira ya Maendeleo 2020 katika nyanja zote za maendeleo ya kiuchumi.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara imeweza kutekeleza yafuatayo:

(i) kuendeleza matayarisho ya Modeli ya Kiuchumi (*MacMod*) ambayo inasaidia kukadiria mwenendo wa kiuchumi na viashiria vyake;

(ii) kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoa taarifa za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka (*QNA*);

(iii) Kuchambua na kutoa taarifa za hali ya mfumko wa bei na mwenendo wake kila mwezi kupitia Kamati ya Kutathmini Hali ya Mfumko wa Bei ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya hatua za muda mfupi na mrefu za kudhibiti mfumko wa bei nchini.

(iv) kuendelea kutoa mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia Kitengo cha Sera za Kodi pamoja na kutoa ushauri juu ya mwenendo wa kodi;

(v) kukamilisha Modeli ya kodi (*Tax Model*) ambayo itasaidia katika kufanya makadirio ya kitaalamu ya kodi na viashiria vyake na kuweza kutoa mapendekezo ya makusanyo ya kodi kiusahihi zaidi;

(vi) kuendelea na kazi za kukusanya takwimu za kifedha kupitia Kitengo chake cha Kutunza Taarifa za Takwimu za kifedha za serikali, takwimu ambazo zinapelekea kuweza kufanya uwiano mzuri wa kiuchumi baina ya nchi yetu na nchi nyengine;

(vii) Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wake katika nyanja mbali mbali za kiuchumi; na

(viii) Kushiriki katika majadiliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Kifedha wa Afrika Mashariki (*East African Community Monetary Union*) pamoja na ushiriki katika Shirikisho la Maendeleo la Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, idara hii itaendelea na kutekeleza lengo lake kuu la kuhakikisha kuwepo kwa utulivu wa Uchumi Mkuu. Aidha idara imepanga kuandaa taarifa za maendeleo ya kijamii na kiuchumi pamoja na kufanya uchambuzi na utafiti wa kiuchumi na kutoa taarifa.

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, idara inaombewa kutumia jumla ya Shilingi 111.10 milioni kwa kazi za kawaida.

A.3 IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Spika, jukumu la idara hii ni kusimamia uratibu wa masuala ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi kitaifa pamoja na kuratibu masuala ya Idadi ya Watu. Aidha, idara inaratibu Programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 84.24 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 424.64 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2010/11, Idara:

i. Iliendelea na mchakato wa utayarishaji wa Utafiti wa Hali ya Utumishi kupitia Jumuia ya Afrika Mashariki ambapo hatua mbali mbali za

matayarisho zilitekelezwa ikiwemo uhamasishaji wa wadau mbali mbali Unguja na Pemba;

ii. Kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Rais Ikulu inayoshughulikia masuala ya Wazanzibari waishio nje ya nchi na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, hatua mbali mbali zitazotuwezesha kukusanya takwimu za Wazanzibari walioko nje ya nchi zimeandaliwa;

iii. Iliratibu maadhimisho ya siku ya Idadi ya Watu duniani kitaifa yaliyofanyika katika wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

iv. Imeufanyia mapitio na kuutafsiri kwa lugha ya Kiswahili Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Idadi ya Watu kabla ya kuchapishwa na kuzinduliwa rasmi;

v. Imeshiriki katika ziara za kimafunzo nchini Uganda na Ghana kwa msaada wa *UNFPA*, kuangalia uzoefu wa nchi hizo juu ya mipango ya idadi ya watu na maendeleo;

vi. Ilifanya ukaguzi na tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto kila baada ya miezi mitatu;

vii. Imeratibu mikutano ya masheha katika wilaya zote kumi za Unguja na Pemba;

viii. Imeratibu mchakato wa haja ya kuwa na Bajeti inayozingatia mahitaji Ia Watoto; na

ix. Imeandaa taarifa juu ya maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika yanayofanyika tarehe 16 Juni ya kila mwaka.

Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilishatumia Shilingi 80.34 milioni, sawa na asilimia 95.4 kwa kazi za kawaida na Shilingi 200.80 milioni, sawa na asilimia 47.3 kwa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, imepanga kuendelea na;

i. Zoezi la utekelezaji wa Utafiti wa Hali ya Utumishi kupitia Jumuia ya Afrika Mashariki;

ii. Kuendelea na Uimarishaji wa Daftari la Taasisi za Kiuchumi (*Central Register of Establishment – CRE*) katika shehia zote za Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali;

iii. Kuandaa tafiti ndogo ndogo ambazo taarifa zake zitatumika katika mipango na maendeleo ya watendakazi Zanzibar;

iv. Kuendelea kuratibu masuala ya idadi ya watu Zanzibar;

v. Kushiriki katika maadhimisho ya siku ya idadi ya watu Duniani;

vi. Kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) kufanya Uchambuzi wa Mahitaji ya uanzishwaji mafunzo ya idadi ya watu katika vyuo vikuu vya Zanzibar;

vii. Kutayarisha taarifa ya mwaka ya masuala ya idadi ya watu Zanzibar;

viii. Kuendelea kuratibu Program ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto Zanzibar kwa kufanya tathmini katika utekelezaji wake;
ix. Kuchapisha madaftari na kutoa mafunzo kwa walengwa juu ya ujazaji wa daftari la masheha; na
x. Kuendelea na mchakato juu ya uandaaji wa bajeti inayowajali Watoto kwa msaada wa *UNICEF*, kama sehemu ya mageuzi yanayokusudiwa kufanywa katika Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, idara inaombewa jumla ya Shilingi 136.24 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 130.00 milioni kwa program moja na miradi miwili ya maendeleo.

A.4 OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, takwimu ni nyenzo muhimu katika kuandaa mipango ya nchi na hatimae kufikia maendeleo endelevu. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ina jukumu la kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu za nchi, kwa lengo la kuiarifu serikali na jamii juu ya mwenendo wa uchumi na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2010/2011, Ofisi iliidhinishiwa jumla Shilingi 1,609.0 milioni ambapo Shilingi 639.0 milioni ni kwa kazi za kawaida na Shilingi 970.0 milioni kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/11, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Serikali ilitekeleza majukumu yafuatayo:

i. Ilikamilisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za Hali ya Uchumi na maendeleo ya jamii (2010 Zanzibar *Socio-economic Survey*);
ii. Ilikamilisha Sensa ya Uzalishaji Viwandani (*Census of Industrial Production*) na kuwasilisha taarifa kwa wadau mbalimbali;
iii. Imekamilisha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (2009/10 *Zanzibar Household Budget Survey*) na taarifa yake tayari imeshawasilishwa kwa wadau; na
iv. Kwa sasa Ofisi inaendelea na Utafiti katika sekta ya utalii kupitia katika hoteli ikiwa ni miongoni mwa juhudi za kuimarisha takwimu za utalii na kuweza kupata Faharisi ya bei ya sekta hii.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Takwimu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taasisi za SMZ na Mashirika ya Kimataifa pia iliweza kukamilisha shughuli zifuatazo:-

i. Kuzifanyia uchambuzi takwimu zilizotokana na utafiti wa hali ya Demografia na Afya (*Tanzania Demographic and Health Survey*);

ii. kuzichambua takwimu zilizotokana na Sensa ya Kilimo na Mifugo (*2007/08 Tanzania Agriculture and Livestock Sample Census*) pamoja na kuandaa taarifa yake;
iii. kukusanya takwimu zilizotokana na Utafiti wa Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Panel Survey*) pamoja na kutoa taarifa;
iv. Kufanya utafiti juu ya Miji na Makaazi;
v. Kuandaa matayarisho juu ya Utafiti wa Hali ya UKIMWI na Malaria (*2011 Tanzania HIV/AIDS and Malaria Indicator Survey*);
vi. Kufanya utafiti wa hali ya uwekezaji Zanzibar; na
vii. Kufanya Sensa ya watumiaji wa huduma ya maji kwa Mikoa ya Pemba.

Hadi kufikia mwisho wa Juni 2011, Ofisi ilipatiwa jumla ya Shilingi 1,431.0 milioni sawa na asilimia 88.9 ya bajeti. Kati ya hizo Shilingi 630.0 milioni zilitumika kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 99 ya bajeti na Shilingi 801.0 milioni sawa na asilimia 83 kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kufanya tathmini ya hali ya ukuaji wa ukadiriaji wa pato la Taifa (*GDP*) kwa mwaka 2011 kwa kutumia takwimu zitakazokusanywa;
ii. Kuendelea na ukusanyaji wa takwimu za msingi kwa kufanya tafiti na Sensa mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango wa "*Survey*" na Sensa (*National Multi-year Program*) unaoendeshwa kwa pamoja na Taasisi ya Takwimu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
iii. Kukamilisha matayarisho ya Sensa ya watu na Makaazi ikiwa ni pamoja na kufanya Sensa ya majaribio ifikapo Agosti 2011, na kukamilisha kazi ya utengaji wa maeneo ya kuhesabia kabla ya Disemba 2011;
iv. Kuimarisha uwezo wa watendaji kwa kuwapatia mafunzo;
v. Kutekeleza mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania; na
vi. Kuendeleza kazi za mradi wa *ZANSTAT* na kuanza mchakato wa uandaaji wa mradi huu katika awamu ya pili.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ofisi inaombewa kutumia jumla ya Shilingi 1,510.0 bilioni, kati yake Shilingi 860.0 milioni ni kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,346,48.0 bilioni ni kwa miradi miwili ya maendeleo.

B. UKUSANYAJI WA MAPATO, HUDUMA ZA BAJETI NA UHASIBU SERIKALINI

Mhe. Spika, kimuundo jukumu hili linasimamiwa na idara tatu na taasisi tatu zinazojitegemea kama ifuatavyo:

B 1 IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, majukumu makubwa la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni:

i. Kutunza Hazina ya Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Bajeti;
ii. Kusimamia na kudhibiti mapato na matumizi ya serikali;
iii. Kusimamia mwenendo wa deni la taifa.
iv. Kusimamia shughuli za uhasibu na ukaguzi wa ndani wa serikali;
v. Kusimamia ugawaji wa fedha kwa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
vi. Kuhakikisha kwamba taratibu zote zinazohusika kisheria katika kudhibiti mapato na matumizi zinafanyika; na
vii. Kutoa miongozo ya kihasibu.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, idara ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 1,317.3 bilioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,720.27 bilioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, jumla ya Shilingi 355.75 bilioni sawa na asilimia 80.13 ya Makadirio ya Mwaka ya Shilingi 444.0 bilioni zilikusanywa, kati ya fedha hizo Mapato ya Ndani ni Shilingi 181.41 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya mwaka ya Shilingi 171.68 bilioni. Misaada ya Kibajeti (*GBS* 4.5%) iliyopokelewa ilifikia jumla ya Shilingi 37.60 bilioni sawa na asilimia 68 ya makadiro ya mwaka ya Shilingi 55.24 bilioni. Aidha, jumla ya Shilingi 136.67 bilioni ziliweza kupatikana kwa njia ya misaada na mikopo kutoka nje, ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi 211.0 bilioni, sawa na asilimia 64.5.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 matumizi halisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yalifikia Shilingi 348.01 bilioni, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa Shilingi 188.29 bilioni, sawa na asilimia 98 ya lengo la Shilingi 193.43 bilioni. Mchango wa serikali kwenye Miradi ya Maendeleo ni Shilingi 30.49 bilioni sawa na asilimia 77 ya lengo la Shilingi 39.49 bilioni. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kupitia kwa Washirika wetu wa Maendeleo jumla ya Shilingi 129.23 bilioni zilitumika hadi kufikia Juni, 2011.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/11 idara imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kwa kushirikiana na Idara ya Bajeti imeendeleza kusimamia ukusanyaji na ugawaji wa fedha za serikali;
ii. Kutayarisha na kufunga Hesabu za Serikali;
iii. Kusambaza Miongozo ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu;
iv Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani;
V. Kufanya tathmini ya matumizi ya serikali na uwajibikaji wa kifedha (*PEFA*); na
vi. Kusimamia deni la taifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mbali na majukumu yake mengine, idara itaendelea kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali katika kusimamia ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya serikali. Aidha, idara itahakikisha kwamba fedha zinazotolewa kwa Mawizara na Taasisi za Serikali zinazingatia Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi (*MTEF*). Pamoja na majukumu hayo Idara pia itatekeleza yafuatayo:

i. Kufanya jumuisho la hesabu na kuliwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria;
ii. Kuendelea kutoa kipaumbele kwa malipo ya mishahara, malipo ya wastaafu na matumizi mengineyo;
iii. Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watendaji wake; na
iv. Kusimamia deni la taifa.

Mhe. Spika, kuhusu malipo ya Wastaafu na Wazee katika hotuba yangu ya Bajeti ya Serikali niliyoitoa mwezi Juni, 2011 nililielezea Baraza lako tukufu kuwa, serikali imekusudia kuongeza kiwango cha pencheni cha wastaafu wetu. Kwa heshima kubwa napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa serikali imeongeza kiwango cha chini cha pencheni kutoka TZS 25,000 kwa mwezi hadi kufikia TZS 40,000 kwa mwezi. Kiwango hicho ni wastani wa ongezeko la aslimia 60 na kitaanza mwezi wa Oktoba, 2011. Kwa upande wa wastaafu ambao pencheni zao zinatoka moja kwa moja katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)*, viwango vyao vipya vya pencheni vitaanza mara tu baada ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kufanyiwa marekebisho yanayotarajiwa kuwasilishwa katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha mwezi wa Oktoba/Novemba mwaka 2011.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara inaombewa kutumia jumla ya TZS 1,677.59 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 20.00 milioni kwa program mbili za maendeleo.

B. 2 IDARA YA BAJETI

Mhe. Spika, sehemu muhimu ya usimamizi wa fedha za Umma ni kupitia Bajeti ya Serikali. Idara ya Bajeti ina jukumu la msingi la kusimamia utayarishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa Bajeti ya Serikali. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 12,026.98 milioni kwa kazi za kawaida, (ikiwemo TZS 11,890.00 milioni kama Ruzuku kwa Taasisi za Wizara) na TZS 6,090.80 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara imeweza kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake kutokana na mwenendo mzuri wa mapato ya ndani licha ya changamoto zilizojitokeza kutokana na Uchaguzi Mkuu na uundwaji wa Serikali mpya ya Awamu ya saba. Katika mwaka 2010/2011 Idara imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. imeratibu shughuli za kibajeti kwa kuhakikisha kwamba Wizara na Taasisi zinatekeleza bajeti zao kulingana na mfumo wa *MTEF*;
ii. imetowa miongozo miwili ya utayarishaji wa Bajeti ya 2011//2012;
iii. imetoa mafunzo juu ya misingi ya uandaaji mzuri wa bajeti ya Serikali kwa Wizara zote;
iv. imeanza kutumia *Codes* mpya kwa vifungu vyote vya matumizi zinazozingatia majukumu ya Serikali *(Classification of Functions of the Government-COFOG);*
v. imeanza maandalizi ya kutumia mfumo mpya wa Bajeti unaozingatia program maalum ndani ya kila Taasisi *(Program Based Budgeting).* Mfumo huo unatoa fursa ya kuimarisha uwazi na ufanisi katika Bajeti na kurahisisha ufuatiliaji wa Matumizi.

Mhe. Spika, mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 12,026. 98 milioni, sawa na asilimia 100 kwa kazi za kawaida na TZS 2,440.086 milioni, sawa na asilimia 40 kwa program na miradi ya maendeleo. Matumizi haya yamejumuisha utekelezaji wa kazi za Idara ya Ukuzaji wa Uchumi wakati Idara hizi zilipokuwa zikifanya kazi chini ya Idara moja ya Ukuzaji Uchumi na Bajeti.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, Idara inakusudia kukamilisha maandalizi mfumo wa *Program – Based Budgeting* kuanza kutumia rasmi mfumo huo wa Bajeti katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Idara itaendelea na jukumu lake

la kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012 ya TZS 613.08 bilioni, kupitia Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Aidha, Idara itaendelea kutoa miongozo na mafunzo maalum kwa Wizara zote juu ya misingi na utaratibu wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia program maalum zitakazoandaliwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara inaombewa jumla ya TZS 19,666.57 milioni kwa kazi za kawaida (zikiwemo TZS 19,424.00 milioni ikiwa ni fungu la marekebisho ya mishahara kitaifa), na TZS 20.00 bilioni kwa miradi na program ya maendeleo.

B.3 IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Spika, kama nilivyoelezea kabla, mapato ya Serikali yanajumuisha mapato ya ndani na ya Misaada kutoka nje (Ruzuku na Mikopo). Idara ya Fedha za Nje ina jukumu la kutafuta, kusimamia, kuratibu na kufanya tathmini ya misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa MKUZA II na Malengo ya Milenia. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Idara ilitarajiwa kutafuta, kuratibu na kusimamia upatikanaji wa jumla ya TZS 211.714 bilioni ambazo kati ya hizo, TZS 79.022 bilioni ni ruzuku na TZS 132.792 bilioni ni mikopo kama ilivyoainishwa katika Bajeti ya mwaka 2010/2011. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 77.053 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 70.00 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Juni 2011, jumla ya TZS 136.674 bilioni sawa na asilimia 64.5 ya makadirio zimepatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 84.764 bilioni ni mikopo na TZS 51.910 bilioni ni ruzuku. Katika kuhakikisha fedha zinazotoka kwa washirika wa maendeleo zinatumika kama ilivyokusudiwa, Idara imekuwa na mashirikiano ya karibu na baadhi ya taasisi zisizo za Kiserikali kwa ajili ya kupata taarifa ya misaada inayotolewa na Washirika wa Maendeleo kupitia taasisi hizo. Jumla ya TZS Tsh 2.390 bilioni zimetolewa na baadhi ya taasisi hizo kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 74.382 milioni, sawa na asilimia 96.53 kwa kazi za kawaida na TZS 45.80 milioni, sawa na asilimia 65.4 kwa mradi wa maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka 2011/12, Idara inatarajiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. kusimamia na kuratibu upatikanaji wa TZS 340.96 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 124.0 bilioni ni ruzuku na TZS 216.0 bilioni ni mikopo;

ii. kuendeleza juhudi za kuimarisha mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo;

iii. kufuatilia fedha ili ziweze kupatikana kwa wakati pamoja na matumizi ya fedha hizi kwa nia ya kuhakikisha kuwa matumizi yanaendana na malengo yaliyokusudiwa; na

iv. kuandaa Sera ya Misaada kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 109.571 milioni kwa kazi za kawaida.

B. 4 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* ni wakala Mkuu wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi za ndani. Pia ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusiana na Sera za Kodi. Kwa mwaka 2010/2011, *ZRB* imeweza kukusanya jumla ya TZS 105.075 billioni sawa na asilimia 103 ya makadirio ya TZS 101.846 billioni. Kiwango hicho cha makusanyo kinamaanisha ongezeko la mapato kwa TZS 15.80 bilioni sawa na asilimia 18 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2009/2010 ambapo *ZRB* ilikusanya TZS 89.2 bilioni. Kwa mwaka 2010/2011, *ZRB* iliidhinishiwa ruzuku ya TZS 4.8 bilioni.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa kazi nyengine mbali ya ukusanyaji wa mapato, *ZRB* ilitekeleza mambo yafuatayo kwa mwaka 2010/2011:

i. Kuwapatia fursa ya kushiriki mafunzo ndani na nje ya nchi wafanyakazi wake 29, ambapo wafanyakazi 22 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi 7 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu Tanzania Bara;

ii. Kukamilisha ukarabati wa jengo la *ZRB* Shangani tokea mwezi Novemba 2010. Aidha ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya *ZRB* hapo Mazizini unatarajiwa kumalizika rasmi mwezi Septemba 2011;

iii. Kufanya utafiti unaohusu ukusanyaji wa mapato katika sekta ya utalii na utafiti wa mifumo ya ukusanyaji na kompyuta kwa ufaadhili wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* kupitia mradi wa Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ; na

iv. Kwa kushirikiana na *TRA*, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kimefanya utafiti wa kuangalia njia gani kodi za ndani za Muungano zinavyoweza kusimamiwa na *ZRB*. Kukamilika kwa tafiti hizi kutatoa mapendekezo yatakayosaidia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *ZRB* imepangiwa kukusanya mapato ya Serikali yenye jumla ya TZS 120.660 bilioni ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2010/2011 yenye jumla ya TZS 105.075 bilioni. Ongezeko hili la TZS 15.585 bilioni ni sawa na asilimia 14.8 ya makusanyo halisi ya mwaka 2010/2011. Katika kuhakikisha kwamba malengo hayo yanafikiwa, *ZRB* itaendelea na utekelezaji wa Mpango wake Mkuu wa Pili wa miaka mitano. Ili kutekeleza majukumu yake, *ZRB* inaombewa ruzuku ya TZS 5.4 bilioni kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

B. 5 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, tawi la Zanzibar ina jukumu la kukusanya mapato ya kodi yatokanayo na vianzio vya Muungano. Kodi hizo ni pamoja na Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Biashara na Kodi ya Mapato *(Income Tax)*. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Mamlaka ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 69.240 bilioni, ambapo mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Mamlaka ilikusanya jumla ya TZS 76.357 bilioni, sawa na asilimia 110.3 ya makadirio. Kiwango hiki kinaashiria ukuaji wa mapato kwa asilimia 27.07 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2009/10. Makusanyo ya TZS 76.357 bilioni yanatokana na ukusanyaji wa TZS 48.686 bilioni kutokana na Kodi za Forodha na TZS 27.671 bilioni zinazotokana na Kodi ya Mapato.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 *TRA* imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 100.580 bilioni, ambapo Idara ya Forodha inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 49.440 bilioni na Idara ya Kodi za Ndani kukusanya TZS 51.140 bilioni. Kati ya mapato ya ndani TZS 18.0 bilioni zinategemewa kukusanywa kama kodi ya mapato ya wafanyakazi wa taasisi za Serikali ya Muungano wanaofanyakazi Zanzibar. Makadirio ya mwaka 2011/2012 ni zaidi kwa TZS 24.22 bilioni au asilimia 31.4 ya makusanyo halisi ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, *TRA* itaendelea kuchukua hatua maalum zinazolenga katika kuongeza mapato kwa kuziba mianya iliyopo. Aidha, *TRA* itaendelea kutoa elimu kwa wananchi na walipa kodi ili kuwajengea uwezo na uelewa wa masuala ya kodi na wajibu wa kulipa kodi kwa hiari kwa mujibu wa sheria.

B. 6 MFUKO WA BARABARA

Mhe. Spika, serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara kama hatua maalum ya kuweka utaratibu wa kuaminika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Lengo ni kuhakikisha kuwa barabara zetu zinazojengwa kwa gharama kubwa zinakuwa endelevu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Barabara ulitarajia kupokea makusanyo ya jumla ya TZS 5.451 bilioni kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara na uendeshaji wa Mfuko. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 4.609 bilioni ni kwa kazi za matengenezo ya barabara ikiwa ni pamoja na ukarabati mkubwa, matengenezo ya sehemu zenye matatizo, matengenezo ya dharura na gharama za usimamiaji na uendeshaji kwa kazi za matengenezo. Jumla ya TZS 0.842 bilioni zilitengwa kwa ajili ya kazi za uendeshaji wa Mfuko ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Ofisi mpya ya Mfuko hapo Maisara.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya TZS 5.018 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 92 ya makadirio. Matumizi halisi yalifikia TZS 4.182 bilioni**,** ambapo TZS 3.516 billioni ni kwa kazi za matengenezo ya barabara na TZS 0.666 bilioni ni kwa kazi za Uendeshaji Mfuko yakiwemo malipo ya ujenzi wa Ofisi ya Mfuko hapo Maisara. Aidha, kazi za ukarabati wa barabara zenye thamani ya TZS 0.546 billioni zinaendelea na malipo yake yatafanywa mara zitakapokamilika.

Mhe. Spika, katika mwaka huo huo Mfuko umeweza:

i. kuitisha vikao na wadau mbalimbali Unguja na Pemba pamoja na kufanya mashauriano mbali mbali kwa lengo la kushajiisha shughuli za matengenezo ya barabara za ndani; na
ii. wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa Mfuko wamehudhuria semina na warsha mbali mbali juu ya utendaji kazi za matengenezo ya barabara pamoja na zile za uendeshaji Mfuko;

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/12 Mfuko unakadiria kukusanya jumla ya TZS 6.432 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 5.463 bilioni ni kwa matumizi ya kazi za matengenezo ya barabara, utunzaji wa kawaida na matengenezo ya dharura. Aidha TZS 0.969 bilioni zimekadiriwa kutumika kwa Uendeshaji wa Mfuko ikiwemo malipo ya mwisho kwa Jengo jipya la Ofisi ya Mfuko. Hadi kukamilika kwake jengo la Ofisi ya Mfuko linategemea kugharimu jumla ya TZS 0.697 bilioni.

C: USIMAMIZI WA MALI ZA SERIKALI
IDARA YA UHAKIKI MALI NA MITAJI YA UMMA

Mhe. Spika, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ina jukumu la kusimamia Mali za Serikali, kuhakikisha zinatunzwa na kuwekewa kumbukumbu. Idara pia ndio msimamizi wa masuala ya ununuzi na uondoaji wa mali Serikalini. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 168.63 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 3.8 bilioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma imeweza:

i. kuendeleza Uhakiki *(Verification)* wa Mali za Serikali katika Wizara na Taasisi za Serikali;
ii. kufanya uhakiki katika Wizara za Kilimo na Maliasili, Mawasiliano na Miundombinu, Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais;
iii. kuwapatia mafunzo ya ndani wakaguzi kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kitaalamu zaidi;
iv. kusimamia uanzishwaji wa Bodi za Zabuni na Vitengo vya Manunuzi *(PMUs)* katika Wizara mpya zilizoundwa ili manunuzi yote ya Serikali yafanywe kwa mujibu wa Sheria;
v. kuwapatia elimu ya taratibu na Sheria za Manunuzi watendaji wakuu na maafisa wa manunuzi kutoka Serikalini na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi; na
vi. kusimamia ufungaji wa hesabu kwa Mashirika ya Umma kwa mujibu wa sheria ya *Public Investment* No. 4. ya 2002;

Mhe. Spika, kama tulivyoeleza kabla, Idara imeandaa na kusambaza fomu za Daftari la Mali za Kudumu za Serikali *(Asset Register).* Changamoto kubwa iliyojitokeza kabla ni tathmini ya mali zilizopo. Changamoto hiyo imetokana na gharama kubwa ya kutia thamani mali hizo, ambazo nyingi ni za zamani sana. Hata hivyo, nina furaha kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa kazi hii sasa ipo tayari kuanza kufuatia msaada kutoka Serikali ya Norway na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Kwa sasa Ofisi yangu imo katika juhudi za kutafuta Mkadiriaji *(Valuer)* ili aweze kuzitathmini Mali za Serikali, kulingana na orodha kamili ya mali zinazopaswa kuwepo kila Wizara kwa mujibu wa Daftari.

Mhe. Spika, uchambuzi wa hesabu za Mashirika ya Umma kwa jumla unaonesha kuwa ukiacha Benki ya Watu wa Zanzibar, karibu mashirika yote yanaonesha hali yao kifedha sio nzuri. Hali hiyo inatofautiana baina ya Shirika

moja na jengine. Kutokana na hali hiyo, kuna haja kubwa ya kuyafanyia mapitio *(restructure)* mashirika ya Serikali ili yaweze kufanya vizuri.

Mhe. Spika, mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 157.98 milioni, sawa na asilimia 93.7 kwa kazi za kawaida na TZS 674.15 milioni, sawa na asilimia 17.74 kwa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. kukamilisha tathmini ya mali za kudumu na kukamilisha uandaaji wa Daftari la Mali za Serikali;
ii. kuendeleza uhakiki wa Mali za Serikali katika Wizara na Taasisi za Serikali;
iii. Kusimamia na kuratibu ufungaji wa hesabu za mwaka katika Mashirika ya Serikali;
iv. kusimamia ununuzi na uondowaji wa mali Serikalini kwa mujibu wa Sheria;
v. kuendelea kusimamia Sheria ya Manunuzi ya No. 9. ya 2005 pamoja na Sheria ya Mitaji ya Umma No 4. ya 2002;
vi. kuendelea kujenga uwezo watendaji katika masuala ya Ununuzi Serikalini; na
vii. kufanya ukaguzi *(Performance Audit)* katika manunuzi yanayofanywa na taasisi za Serikali.
viii. kuanzisha Daftari maalum la Wakandarasi na watoa huduma nyengine wenye sifa za kupewa kazi hizo Serikalini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 197.60 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 5.50 bilioni kwa program moja na miradi miwili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo TZS 5.3 bilioni ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali zikiwemo Jengo la Wizara ya Katiba na Sheria – Unguja; Miundombinu na Mawasiliano – Unguja; Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Pemba; Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto – Pemba; Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Unguja na Biashara, Viwanda na Masoko – Pemba. Fedha zilizobakia TZS 200 milioni ni kwa ajili ya kusimamia tathmini ya Mali za Serikali.

D. HUDUMA ZA UTAWALA, URATIBU, SEKTA YA FEDHA NA UWEKEZAJI

D.1 HUDUMA ZA UTAWALA NA URATIBU

Mhe. Spika, ORFUMM ina Idara tatu na Ofisi ya Wizara Pemba ambazo zinasimamia maendeleo ya Sekta na huduma za Utawala. Aidha, Sekta ya

Fedha kwa hapa Zanzibar inahusisha Taasisi tatu za Serikali ambazo ni Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)*, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)*, na Shirika la Bima *(ZIC)*.

D 1.1 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Kufuatia muundo mpya wa Serikali wa kuwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa kila Wizara, jukumu kuu la Idara hii ni kusimamia na kuimarisha mazingira bora ya kazi, kuendeleza wafanyakazi wa Wizara na kusimamia huduma za TEHAMA na sheria. Aidha, Idara inasimamia masuala yote ya utawala, ustawi wa wafanyakazi na kuimarisha utoaji wa huduma kwa watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 9,502.78 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 1.458.4 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011, Idara ilitarajia kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi kwa upande wa Pemba. Kwa bahati mbaya ujenzi haukwenda kama tulivyotarajia kutokana na kuwa taratibu za ujenzi hazikufuatwa, na hivyo kupelekea Ofisi yangu kusimamisha ujenzi, baada ya kufanyika uchunguzi na kupata ushauri wa kitaalamu. Kwa sasa Ofisi inaendelea na hatua za kudai kurejeshewa gharama za ujenzi kutoka kwa Mkandarasi na Msimamizi. Tayari tumeshawasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu juu ya nia na azma yetu ya kufungua kesi kama tutashindwa kukubaliana nje ya Mahakama.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, OR- FUMM imeweza kuajiri vijana wapatao 156 waliohitimu fani ya uhasibu na kuwasambaza katika mawizara mbalimbali Unguja na Pemba. Pia vijana 28 wa fani ya ununuzi na ugavi *(Procurement and Supplies)* waliajiriwa na kusambazwa katika vitengo vya manunuzi vya mawizara mbali mbali. Katika kipindi hicho hicho vijana 18 pia waliajiriwa wakiwemo wa fani ya uchumi, sheria na teknolojia ya Habari na Kompyuta. Aidha, wafanyakazi 12 walistaafu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa upande wa ujenzi wa uwezo wa watendakazi, Idara imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 54 wakiwemo wanawake 29 na wanaume 25 ndani na nje ya nchi katika fani za Uhasibu, Fedha, Uchumi, Utawala na Manunuzi. Wafanyakazi wengine 34 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 9.494 bilioni, sawa na asilimia 99.9 kwa kazi za kawaida na TZS 0.142 bilioni, sawa na asilimia 9.75 kwa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara inakusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuanza ujenzi wa ofisi ya Pemba;
ii. kuendelea na utekelezaji wa mapendekezo ya Mshauri Mwelekezi ya kujenga uwezo katika Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo;
iii. kuwapatia wafanyakazi 83 wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi; na
iv. kuandaa mafunzo ya ndani *(In house training)* kwa wafanyakazi 60 kwa lengo la kuwaongezea uwezo, ujuzi na uzoefu katika utendaji wa kazi zao.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara inaombewa kutumia jumla ya TZS 9,760.51 milioni kwa kazi za kawaida.

D 1.2 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la:

i. kuratibu uandaaji na utekelezaji wa sera mbali mbali zinazoihusu sekta ya Fedha;
ii. kusimamia shughuli za utafiti za Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na mipango ya Maendeleo;
iii. kusimamia utekelezaji wa maeneo yanayohusu sekta ya fedha chini ya Mpango wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA);
iv. kuratibu masuala Mtambuka (*HIV/AIDS*, Jinsia, mazingira na idadi ya watu) ndani ya Ofisi;
v. kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ofisi;
vi. kuratibu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi; na
vii. kuandaa Mpango kazi wa Ofisi pamoja na kuratibu utekelezaji wake.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 150.04 milioni kwa kazi za kawaida, na TZS 88.023 milioni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11 Idara imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo;

i. kusimamia matayarisho ya Mpango Mkakati (Awamu ya Pili);
ii. kuandaa Mapitio ya Sekta ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo;

iii. Kuendelea kuratibu matayarisho ya *MTEF* ya Ofisi;
iv. kushiriki katika vikao mbalimbali Tanzania Bara hasa vile ilivyojadili Mageuzi ya Sekta ya Fedha nchini Tanzania yanayoratibiwa na Benki Kuu ya Tanzania;
v. kusimamia hatua za awali za utayarishaji wa Sera ya Taasisi ndogo ndogo za Fedha *(Microfinance Policy)* nchini;
vi. kuandaa warsha na semina mbili za kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi kwa wafanyakazi wa Ofisi; na
vii. kutoa mafunzo ya ndani juu ya usimamizi wa taarifa *(Management Information System)* kwa maafisa wake.

Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 145.22 milioni, sawa na asilimia 96.8 kwa kazi za kawaida na TZS 39.53 milioni, sawa na asilimia 4.5 kwa program na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara itaendelea na majukumu yake ya kawaida ya:

i. kuratibu shughuli zote za mipango, sera na utafiti;
ii. itachukua hatua maalum kushajihisha Idara na Taasisi za Ofisi kuibua maeneo ya tafiti na kuratibu utekelezaji wake;
iii. itasimamia utekelezaji wa mradi wa *E-government;* na
iv. itasimamia marekebisho ya Sheria mbali mbali za Sekta kama vile Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu *(Anti-money Laundering)*, Sheria za *ZIPA*, *ZSSF* na Tume ya Mipango.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara inaombewa jumla ya TZS 107.80 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 49.11 milioni kwa kusimamia program moja na mradi mmoja wa maendeleo.

D 1.3 OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO- PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Pemba ina majukumu yafuatayo:

i. kusimamia shughuli za Ofisi kwa upande wa Pemba;
ii. kuratibu shughuli zote za usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali;
iii. kusimamia na kuimarisha mazingira bora ya kazi;
iv. kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ile ya wananchi;
v. kusimamia udhibiti wa mali za Serikali kwa upande wa Pemba; na
vi. kuratibu utekelezaji mradi wa Wilaya ya Milenia ya Micheweni.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ilipangiwa kutumia jumla yaTZS 501.66 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Ofisi imeweza kutekeleza kazi mbali mbali zikiwemo:-

i. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 10 katika ngazi mbali mbali ikiwemo shahada ya Uzamili kwa wafanyakazi 2, Shahada ya kwanza wafanyakazi 6 na Stashahada wafanyakazi 2;

ii. Kukamilisha kwa asilimia 80 ukusanyaji wa taarifa za mali za serikali pamoja na kuzifanyia ukaguzi;

iii. Kufanya ukaguzi wa vituo 45 vya ukusanyaji wa mapato ya wizara mbali mbali na Taasisi zake kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ; na

iv. Kufanya ukaguzi wa *Sub-Accounts* za Mawizara na Taasisi zilizoko Pemba uliosaidia kutambua uwezo wa wahasibu, wakusanyaji wa mapato na wakaguzi wa ndani.

Mpaka kufikia mwezi Juni 2011, Idara ilitumia TZS 483. 21 milioni, sawa na asilimia 96.3 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Ofisi imepanga kutekeleza majukumu
yafuatayo:

i. kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi;
ii. kusimamia udhibiti wa matumizi ya Fedha na Mali za Serikali;
iii. kuratibu utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kitaifa, kisekta na kijamii;
iv. kuratibu utekelezaji wa Sera mbali mbali za ofisi kwa upande wa Pemba; na
v. kuratibu shughuli za usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali na kukusanya taarifa za mali za Serikali pamoja na kufanya ukaguzi wa *Sub Accounts* zote za Wizara na Taasisi zake.

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi inaombewa jumla ya TZS 716.26 milioni kwa kazi za kawaida.

D 1.4 IDARA YA URATIBU SHUGHULI ZA SMZ – DAR ES SALAAM

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Shughuli za SMZ Dar es salaam ina jukumu la kuratibu kazi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa SMT hususan Wizara za Fedha, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Mipango ya Serikali ya Muungano. Aidha, Idara inaratibu masuala ya SMZ na Afisi za Balozi mbali mbali zilizopo Tanzania, wadau wa maendeleo pamoja na mashirika ya Kimataifa yenye ofisi zao Dar es salaam. Kwa mwaka 2010/11 Idara iliidhinishiwa kutumia TZS 188.97 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara ya Uratibu kwa kushirikiana na Idara ya Mafunzo ya Utumishi wa Umma Dar es salaam, KOICA, JICA, Singapore, Jumuiya Ya Madola na wengineo, iliweza:

i. Kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi kumi na tano (15) katika fani mbali mbali;
ii. Kushiriki katika kikao cha uteuzi wa mafunzo ya nje yaliyotolewa na Serikali ya Algeria; na
iii. Kuwakilisha Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika mikutano mbalimbali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Washirika wa Maendeleo.

Hadi mwisho wa Juni 2011, Idara ilitumia TZS 182.54 milioni sawa na asilimia 96.6 ya bajeti yake.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara imepanga kuendelea na jukumu lake la kuratibu na kukuza ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia Idara itaendelea kuratibu ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo baina ya SMZ na Afisi za Balozi za nje na Mashirika ya Maendeleo yaliyo na ofisi zake Dar es salaam, pamoja na kushiriki kikamilifu katika mikutano na mijadala mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa faida ya serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi inaombewa jumla ya TZS 190.57 milioni kwa kazi za kawaida.

D. 2 SEKTA YA FEDHA

D 2.1 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Mhe. Spika, jukumu kubwa la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ni kupokea na kutunza

amana za wateja na kukopesha kwa mujibu wa taratibu ziliopo. Hadi kufikia mwezi Juni 2011 amana za wateja zilifikia TZS 124.67 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.0 ikilinganishwa na amana za TZS 105.76 bilioni zilizofikia mwezi Juni 2010. Aidha, Mikopo iliyotolewa kwa Wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, baadhi ya Taasisi za Muungano na wafanyabiashara ilifikia TZS 53.20 bilioni, ikilinganishwa na TZS 40.40 bilioni mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 31.

Mhe. Spika, Katika kusogeza huduma karibu zaidi na wateja, PBZ imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) kufungua Tawi jipya Jijini Dar Es Salaam;
ii) kuimarisha tawi la Mwanakwerekwe kwa kulihamishia kwenye jengo la kisasa la ZSSF lilioko Mwanakwerekwe;
iii) kufungua tawi la kuwahudumia wateja wakubwa lilioko katika jengo la Muzammil hapo Mlandege;
iv) kuanzisha huduma ya Benki ya Kiislamu;
v) kufanikisha utaratibu wa kupokelea mishahara ya wafanyakazi wa Serikali kupitia kwenye akaunti zao;
vi) Kuimarisha mtandao wa mashine za ATM; na
vii) Kuendeleza ujenzi wa jengo lake la benki la Chake Chake.

Mhe. Spika, kwa ujumla, PBZ imeendelea kupata mafanikio kutokana na mageuzi yanayoendelea. Kwa sasa mtaji wa PBZ umefikia TZS 15.40 bilioni ikilinganishwa na TZS 12.45 bilioni kwa mwaka 2009/2010. Kiwango cha sasa cha mtaji kimepelekea PBZ kufikia kiwango cha chini cha TZS 15.0 bilioni kinachotakiwa na Benki Kuu kwa kila benki ya biashara.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2011/12 PBZ itaendeleza:

i. kusogeza huduma na kuendeleza majukumu yake ya msingi ya ukusanyaji na utunzaji wa amana na utoaji wa mikopo;
ii. kukamilisha miradi yake iliyoanza katika mwaka 2010, ikiwa ni pamoja na:
   a) uimarishaji wa rasilimali watu (*Manpower*) na mawasiliano ya habari ya Teknohama,
   b) kuweka vituo vidogo vidogo vya Benki (*Service Centers*) kwa Kaskazini na Kusini Unguja na Wete na Mkoani huko Pemba, na
   c) kuanzisha huduma za Benki kupitia mtandao (*Internet Banking*) pamoja na huduma za Benki kupitia simu (*SMS alert*); na
iii. kuanzisha huduma za Benki ya Kiislam Dar Es Salaam na Pemba.

D 2.2 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII – ZANZIBAR

Mhe. Spika, Jukumu kubwa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kupokea mafao ya wafanyakazi na hatimae kuyarejesha kwa walengwa muda unapofikia. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko:

i. Umesajili wanachama waajiri 81 na wanachama waajiriwa 3,893;
ii. Umekusanya jumla ya TZS 14.869 bilioni sawa na asilimia 99 ya makusanyo yaliyotegemewa kutoka kwa wanachama wote waliosajiliwa na Mfuko;
iii. Umelipa mafao TZS 2.805 bilioni kwa wanachama wastaafu wapatao 562;
iv Umerejesha michango ya wanachama 124 yenye thamani ya TZS 0.289 bilioni;
v Umelipa pencheni TZS 0.662 bilioni kwa wanachama 3,105; na
vi Umekamilisha tathmini ya hali ya Mfuko na uendelevu wake (*Acturial Valuation*) kwa msaada wa Benki ya Dunia. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa Mfuko unahitaji kufanyiwa mageuzi makubwa ili uwe endelevu.

Mhe. Spika, Kwa upande wa uwekezaji, Mfuko umechukua hatua kadhaa zikiwemo zifuatazo;

i) Kuwekeza TZS 43.72 bilioni katika maeneo ya muda mrefu (Dhamana za Hazina na Majengo);
ii) Kuwekeza TZS 33.08 bilioni katika maeneo ya muda mfupi (hati fungani);
iii) Kuendelea na mchakato wa matayarisho ya ujenzi wa viwanja vya kufurahishia watoto Kariakoo; na
iv) Kujifunza teknolojia ya ujenzi wa nyumba za mkopo nafuu nchini China,

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2011/2012, Serikali imekusudia kuufanyia mageuzi makubwa mfumo wa Hifadhi ya jamii chini ya Mfuko huu. Sheria ya ZSSF itafanyiwa marekebisho ili iweze kwenda sambamba na Mageuzi hayo.

D 2.3 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Spika, huduma za Bima ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na hifadhi ya jamii. Tokea kuregezwa masharti ya biashara hii, Makampuni manne ya Bima kati ya ishirini na sita (26) yaliyosajiliwa Tanzania yamefungua Ofisi zake Zanzibar. Pamoja na ushindani huo wa kibiashara, Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) bado linaendelea kutoa huduma zake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/11, ZIC imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuendeleza utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Shirika wa miaka mitatu;
ii. Kukusanya jumla ya TZS 8.20 bilioni sawa na asilimia 85.4 ya makadirio ya mwaka;
iii. Kulipa TZS 4.1 bilioni kwa madai mbali mbali;
iv. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ambapo ujenzi umefikia kiwango cha asilimia 85 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwaka huu; na
v. Kuendeleza wafanyakazi ambapo watano wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wawili ya muda mfupi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ZIC inatarajia kukusanya jumla ya TZS.10.500 bilioni na kutumia jumla ya TZS 2.800 bilioni kwa kazi zake za kawaida. Juhudi zitaendelezwa kuliimarisha zaidi Shirika kwa mtaji, wataalamu na kufanya mageuzi ya huduma zake kwa lengo la kukabiliana na ushindani. Shirika litakamilisha utafiti juu ya uwezekano wa kuanzisha huduma za Bima zinazoendana na maadili ya Kiislam (TAKAFUL).

D 2.4 CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA, ZANZIBAR

Mhe. Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha (*ZIFA*) kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani ya fedha na zile zinazolingana, zikiwemo Uhasibu, Ukaguzi wa hesabu, Benki na Manunuzi. Chuo pia kinajihusisha na kutoa huduma za Ushauri (*Consultancy*) katika masuala ya fedha na Uongozi na kuendesha mafunzo ya muda mfupi katika fani za Fedha, Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Chuo kimeweza kusajili jumla ya wanafunzi wapatao 878, miongoni mwao wanafunzi 251 wa ngazi ya Cheti, 483 katika Stashahada ya Kawaida, 9 Stashahada ya Juu na 135 Shahada ya Kwanza. Kwa ujumla Chuo kimetambulika vyema na kupata maombi mengi ya wanaotaka kujiunga kwa kozi mbali mbali. Aidha, Chuo kimeweza kuhudhuria mikutano na semina zilizoandaliwa na NACTE na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Mhe. Spika, katika hatua za kujiimarisha kitaaluma, Chuo kimechukua hatua kadhaa, miongoni mwake ikiwa ni pamoja na:

i. Kupeleka masomoni walimu sita, wawili kwa masomo ya Shahada ya Uzamivu (PhD) na wanne Shahada ya Uzamili (*Masters*);
ii. Kuajiri wafanyakazi tisa (9);
iii. Kuanzisha kituo cha Utafiti kwa kukarabati jengo na kununua vifaa;
iv. Kuendelea na ujenzi wa Dakhalia;

v. Kuimarisha maslahi ya wafanyakazi;
vi. Kuendesha mafunzo ya muda mfupi na semina kwa wadau mbalimbali;
vii. Kuwapatia wafanyakazi watatu wasiokuwa walimu mafunzo ya muda mfupi;
viii. Kuandaa semina nane (8) za mafunzo kwa wadau mbali mbali; na
ix. Kuanzisha mafunzo ya Stashahada ya Ununuzi na Ugavi (*Procurement and Supplies*)

Mhe. Spika, kwa mwaka wa Fedha 2011/2012, Chuo kimepanga:

i. kusajili wanafunzi wapatao 1100 katika mikondo ya Shahada ya Uongozi wa Fedha katika Uhasibu, Uongozi wa Fedha katika Benki, Stashahada ya Uhasibu, Teknohama, Ununuzi na Ugavi na Cheti cha Uhasibu;
ii. kitaanzisha Shahada ya Kwanza katika fani ya Benki na Fedha pamoja na Stashahada ya Uzamili katika fani ya Uhasibu;
iii. kukamilisha ujenzi wa dakhalia na ununuzi wa samani;
iv. kufanya tafiti mbali mbali za kitaifa;
v. kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa walimu na wafanyakazi wasiokuwa walimu; na
vi. kuwapeleka walimu wawili katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, wafanyakazi wanne katika ngazi ya Shahada ya Uzamili, walimu 12 na wafanyakazi watano (5) wasiokuwa walimu mafunzo ya muda mfupi.

Mhe. Spika, Chuo kinaombewa ruzuku ya TZS 1.558 bilioni ambapo kati yake TZS 1.058 bilioni ni kwa matumizi ya kawaida na TZS 0.50 bilioni kwa utekelezaji wa mradi mmoja wa maendeleo.

D.3 HUDUMA ZA UWEKEZAJI

MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (*ZIPA*)

Mhe. Spika, Jukumu kubwa la Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) ni kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini. Lengo ni kukuza uchumi, kuongeza mapato ya Serikali na ya wananchi, kuingiza teknolojia mpya na kuzalisha ajira kwa ajili ya wananchi. Ili kukamilisha yote hayo, Mamlaka imekuwa ikitoa miongozo na kukutana na wawekezaji. Katika hatua ya kuimarisha maeneo huru ya uchumi pamoja na bandari huru, Mamlaka imeweza kuvutia wawekezaji watatu katika maeneo hayo wenye lengo la kuwekeza humo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ZIPA imeweza kuidhinisha jumla ya miradi 43 ikiwa katika sekta za hoteli, viwanda, biashara, kilimo,

elimu n.k. Miradi hii kwa jumla ilitarajiwa kugharimu jumla ya USD 129.069 milioni na kuainisha nafasi za ajira 1,867 wakati wa kukamilika kwake na kuanza kazi. Katika hatua za kuijengea uwezo taasisi, jumla ya wafanyakazi saba wamepatiwa mafunzo katika ngazi za Cheti, Stashahada, Shahada ya Kwanza na Stashahada ya Uzamili katika vyuo mbalimbali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ZIPA imekusudia kushajiisha zaidi wawekezaji ili kuongeza miradi ya wawekezaji ya utalii wa daraja la juu, kutangaza fursa zilizopo kwenye uvuvi, viwanda, huduma za afya, mawasiliano, kilimo na elimu. ZIPA imedhamiria kuendeleza maeneo ya Bandari huru na maeneo huru ya uchumi kwa kuimarisha miundombinu kwenye maeneo hayo.

Mhe. Spika, Mamlaka inaombewa ruzuku ya TZS 300 milioni kwa mwaka 2011/12.

V. PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2010/2011 NA MWELEKEO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2010/2011, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilipangiwa kutekeleza na kuratibu utekelezaji wa Programu nane (8) na miradi kumi na nne (14) ya maendeleo. Utekelezaji halisi wa Program na Miradi hii ni kama ilivyoelezwa chini ya Idara na Taasisi mbali mbali katika hotuba hii. Kwa upande wa utekelezaji kifedha, Program na miradi hii ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 23.671 bilioni, zikiwa TZS 13.224 bilioni ni misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 10.247 bilioni ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia mwezi Juni 2011, jumla ya TZS 8.803 bilioni sawa na asilimia 58.6 zilishatumika kwa utekelezaji kutokana na mchango wa Serikali.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imepanga kutekeleza jumla ya Program tano (5) na miradi tisa (9) ya maendeleo. Program na miradi hio itagharimu jumla ya TZS 80.217 bilioni zikiwa TZS 7.24 bilioni ni mchango wa Serikali na TZS 72.977 bilioni ni misaada na mikopo kutoka nje.

VI HITIMISHO

Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011 ulifanyika kwa mashirikiano makubwa na taasisi zote zilizomo ndani ya ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, taasisi nyengine za serikali na zisizokuwa za Serikali. Mchango mkubwa wa rasilimali na ushauri ilitolewa wa Washirka wenzetu wa Maendeleo pamoja na ule wa asasi nyengine za Kiraia katika

utekelezaji huo. Ni imani yangu kuwa kwamba ushirikiano huu utaoneshwa kwa nguvu zaidi katika utekelezaji wa bajeti ijayo na MKUZA II.

Mhe. Spika, katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2010/2011, shukurani zangu maalumu nazitoa kwa Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa imani yake kwangu iliyopelekea kunipa jukumu la kuongoza taasisi za fedha kwa maendeleo ya nchi yetu. Nawashukuru pia Mhe. Makamo wa Kwanza na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano na miongozo yao mbali mbali ambayo imesaidia sana kurahisisha utekelezaji wa majukumu niliyokabidhiwa.

Aidha, Mhe. Spika nakushukuru wewe na Wajumbe wote wa Baraza lako kwa miongozo mbali mbali. Shukrani za pekee nazitoa kwa Waheshimiwa wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Baraza lako ambazo tunakutana nazo mara kwa mara kama vile Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Mhe. Omar Ali Shehe, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, pongezi nyengine ziwaendee Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, Naibu Katibu Mkuu (Fedha), Wakuu wote wa Idara na Taasisi za Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na ushauri walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ni matumaini yangu kuwa tutayaimarisha zaidi mashirikiano haya kwa lengo la kuleta ufanisi katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa dhamana tulizonazo.

Mhe. Spika, Ofisi yangu itatekeleza kwa vitendo agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar linalowataka Viongozi na Watendaji wote wa Umma kubadilika katika utendaji wetu wa kazi.

Mhe. Spika, napenda pia kumshukuru mke wangu Narman na watoto wangu, kwa kunivumilia wakati wote nikiwa natekeleza majukumu ya serikali. Nawaomba waendelee kunivumilia kwani shughuli ninazozifanya zina mastahi na sisi pia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo itasimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato ya Zanzibar, yanayokadiriwa kufikia jumla ya TZS 221.24 bilioni, misaada ya Kibajeti yenye thamani ya TZS 30.28 na TZS 340.96 bilioni ikiwa ni misaada na mikopo kutoka nje kwa ajili ya Program na Miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaomba Baraza lako tukufu kuidhinishiwa jumla ya TZS 174.86 bilioni ambapo TZS 47.021 bilioni ni kwa matumizi ya Kawaida (ikiwemo ruzuku kwa taasisi za ofisi), TZS 80.22 bilioni kwa kazi za Maendeleo na TZS 47.62 bilioni kwa matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali kama inavyoonekana hapa chini;

			TZS bilioni
I.	**Matumizi ya Kawaida**		**47.021**
	-	Mishahara	1.902
	-	O/C	11.610
	-	Ruzuku kwa Taasisi	14.084
	-	Marekebisho ya Mshahara	19.425
II.	**Matumizi ya Kazi za Maendeleo**		**80.22**
	-	Mchango wa Serikali	7.240
	-	Ruzuku na Mikopo	67.280
III	**Mfuko Mkuu wa Serikali**		**47.620**
JUMLA KUBWA			**174.86**

Mhe. Spika, uchambuzi wa mapendekezo ya mapato na matumizi haya pamoja na muhtasari wa maelezo mengine, unaonekana katika viambatanisho (i-xiii).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja**.**

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Kiambatisho Nam. i

MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2010/11

IDARA	MAKADIRIO 2010/2011	MATU JUNI 2
AFISI KUU PEMBA	501,659,851.00	
MIPANGO NA SERA	150,040,000.00	
UKUZAJI UCHUMI NA BAJETI	12,026,976,846.00	
MHASIBU MKUU WA SERIKALI	951,986,619.00	
URATIBU SHUGHULI ZA SMZ DSM	188,971,000.00	
FEDHA ZA NJE	77,052,826.00	
MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI	84,238,000.00	
IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KI SEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI	182,098,000.00	
MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	168,631,000	
UTAWALA NA HUDUMA	9,502,775,550.00	
JUMLA	**23,834,429,692.00**	

Kiambatisho Nam. ii

MATUMIZI KWA KAZI ZA MAENDELEO 2010/2011

KASMA	PROGRAMU/MIRADI	MC SM
	OFISI YA RAIS FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO	
	Programu ya kuimarisha Fedha na Uchumi:-	
72163	Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST)	
72166	Mfumo wa Pamoja wa Usimamizi wa Fedha IFMS	
	Maendeleo ya mfumo wa kibajeti	
72165	Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma PFMRP	
	Uimarishaji wa kitengo cha mishahara	
	MCA-T Coordination	
	Ununuzi wa Vifaa vya kufundishia	
72216	Uratibu wa Mageuzi ya msingi	
72162	Ujenzi wa Chuo na Dakhalia Chwaka	
71248	Uratibu wa programu ya MCC	
	Programu ya Mkakati wa Utekelezaji MKUZA	
71150	Miradi midogo midogo ya wananchi	
	Ujenzi wa Milaya ya Milenia Micheweni Pemba	
72221	Ufuatiliaji wa mpango wa kupunguza umasikini	
	Pillar III	
	Uimarishaji wa Tume ya Mipango	
72218	Uwezeshaji kwa wanyonge	
71121	**Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali**	

	Ujenzi wa Ofisi za SMZ	2
	Miradi	
71229	Ujenzi wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo (Pemba)	
	Uimarishaji uwezo wa wafanyakazi	
71244	Kuoanisha masuala ya idadi ya watu, afya ya uzazi, jinsia na umasikini	
71140	Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto	
71245	Utafiti wa watenda kazi	
71228	Kufanya tathmini mali za serikali	
72167	Kuimarisha usimamizi wa Misaada	
72140	Uimarishaji Takwimu	
71230	Mradi wa Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)	
72044	ZANSTAT	
	Management Information System (MIS)	
	JUMLA YA FUNGU	

kiambatisho Nam. iii

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWA

KASMA	IDARA	MAKISIO KWA MWAKA 2010/2011
3	AFISI KUU PEMBA	501,659,851.00
4	MIPANGO, SERA NA UTAFITI	150,040,000.00
5	UKUZAJI UCHUMI	12,026,976,846.00
6	BAJETI	0
	RUZUKU	
7	MHASIBU MKUU WA SERIKALI	951,986,619.00
8	URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ - DSM	188,971,000.00
9	FEDHA ZA NJE	77,052,826.00
10	MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI	84,238,000.00
11	MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI	182,098,000.00
13	MITAJI YA UMMA NA UHAKIKIMALI	168,631,000.00
19	UTAWALA NA HUDUMA	9,502,775,550.00
	JUMLA	**23,834,429,692.00**

Kiambatanisho Nam.iv

ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ITAKAYOTEKELEZ
OFISI YA RAIS - FEDHA , UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

KASMA	JINA LA MRADI	MAKISIO KWA MWAKA	MAKISIO KWA MWAKA

		2010/2011 SMZ	2011/2012 SMZ
	1	*2*	*3*
	Programu ya Kuimarisha Uwezo - Wizara ya Fedha na Uchumi		
72163	i) Kuijengea Uwezo Wizara ya Fedha na Uchumi	*120,000*	40,000
72166	ii) Kuandaa Modali za Bajeti	150,000	20,000
	iii) Uimarishaji kitengo cha mishahara	190,000	
72165	v) E-government		20,000
72162	**Programu ya Changamoto ya Milenia (MCA - T)**	60,000	60,000
72217	**Programu ya pamoja ya UN (PIII)**	80,000	
72219	**Programu ya UNDAP**		
	Program ya Mkakati wa Utekelezaji wa MKUZA		
71150	i) Miradi Midogo Midogo ya Wananchi	600,000	
72221	ii) Ufuatiliaji wa Mpango wa Kupunguza Umasikini	50,000	
72216	iii) Uwezeshaji kwa Wanyonge	50,000	
71150	iv) Uratibu wa Uimarishaji Mazingira ya Biashara Tanzania (BEST)	15,000	15,000
72161	v) Kuimarisha jitihada za kupunguza umasikini		40,000
72221	**Programu ya Uratibu wa Mageuzi ya Msingi**	60,000	
72218	**Programu ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar**	3,000,000	5,300,000
	i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko		
	ii)Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano		
	iii) OR - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo		

71230	iv) Wizara ya Ustawi wa Jamii,Vijana,Maendeleo ya Wanawake na Watoto		
71140	v) Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Sheria		
71167	vi) Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora		
72140	**Programu ya Kuimarisha Huduma za Miji (ZUSP)**	60,000	80,000
72042	**Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma PFM**	25,000	20,000
72044	**Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA)**		
71229	**Miradi**		
72214	i) Mfumo wa Pamoja wa Usimamizi wa Fedha IFMS	680,000	
71228	ii) Ujenzi wa Chuo na Dahalia Chwaka	1,000,000	500,000
72215	iii) Ununuzi wa vifaa vya madarasa ya kusomea na dakhalia	150,000	
72169	iv) Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto	46,000	30,000
71167	v) Kuimarisha usimamizi wa Misaada	70,000	
	vi) BEST Wizara ya Fedha na Uchumi-URT	20,000	
	vii) Uimarishaji wa Takwimu	600,000	400,000
72042	viii)Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya	20,000	
72044	ix) ZANSTAT (OCGS)	350,400	250,000
71229	x) Ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Fedha na Uchumi (Pemba)	900,000	
72214	xi) Kuoanisha masuala ya idadi ya watu katika afya ya Uzazi, jinsia na kupunguza Umasikini	120,000	40,000
72215	xii) Mradi wa Utafiti wa Watenda kazi	190,000	60,000

72169	xiii) Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Pili		40,000
71228	xiv) Mradi wa kufanya tathmini ya Mali za Serikali	1,500,000	200,000
	xv) Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba		40,000
	xvi) Matarajio	61,000	
71229	xvii) Ujenzi wa Wilaya ya Milenia Micheweni Pemba	50,000	
	xviii) Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha TUME YA MIPANGO	150,000	85,000
	JUMLA YA FUNGU	**10,447,400**	**7,240,000**

Kiambatanisho Nam. V

MALIPO YA MISHAHARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2010 HA

FUNGU	WIZARA/TAASISI	MISHAHARA MAKISIO YA MWAKA
5	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais	428,348.
6	Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais	290,827.
7	Ofisi ya Rais Uhusiano	59,996.
8	Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi	504,503.
9	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ	240,261.
10	Ofisi ya Rais Ikulu	1,320,935.
11	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar	645,589.
12	Tume ya Ukimwi	107,503.
13	afisi ya waziri kiongozi	299,397.
14	Mahkama Kuu Zanzibar	1,001,544.
15	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar	197,029.
16	Baraza la Wawakilishi	3,668,879.
17	Jeshi la Kujenga Uchumi	3,867,629.
18	Chuo Cha Mafunzo	2,933,137.
19	Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo	1,647,342.
20	Wizara ya Kilimo, Maliasili	5,326,306.
21	Biashara Viwanda na Masoko	540,784.
22	Wizara ya Mifugo na Uvuvi	598,391.
23	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	32,393,951.
24	Wizara ya Afya	8,922,108.
25	Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati	1,576,133.
26	Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano	2,667,483.
27	Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika	259,661.35

28	Wizara Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto	644,969.50
29	Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo	5,153,000.00
30	Tume ya Uchaguzi	529,551.02
31	Kamisheni ya Utalii	216,996.00
32	Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	1,280,447.46
33	Wizara Katiba na Sheria	351,685.22
34	Kikosi cha Volantia	1,907,410.06
35	Mkurungenzi wa Mashtaka	369,710.46
36	wizara ya katiba na sheria	309,413.72
37	Mkoa wa Mjini Magharibi	408,201.31
38	Mkoa wa Kusini (U)	396,038.00
39	Mkoa wa Kaskazini (U)	384,334.88
40	Mkoa wa Kusini(P)	328,367.70
41	Mkoa wa Kaskazini(P)	380,443.00
42	Wizara ya Habari, Utalii na Michezo	1,961,318.96
43	Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	248,910.00
44	Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora	328,742.99
		84,697,286.79
	JUMLA	**84,697,2**

kiambatisho Nam.vi

MALIPO MENGINEYO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI JUNI

FUNGU	WIZARA/TAASISI
5	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais
6	Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais
7	Ofisi ya Rais Uhusiano
8	Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi
9	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ
10	Ofisi ya Rais Ikulu
11	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar
12	Tume ya Ukimwi
13	afisi ya waziri kiongozi
14	Mahkama Kuu Zanzibar
15	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar
16	Baraza la Wawakilishi
17	Jeshi la Kujenga Uchumi
18	Chuo Cha Mafunzo
19	Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
20	Wizara ya Kilimo, Maliasili
21	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko
22	Wizara ya Mifugo na Uvuvi
23	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
24	Wizara ya Afya
25	Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
26	Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano
27	Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
28	Wizara Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto
29	Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo
30	Tume ya Uchaguzi

31	Kamisheni ya Utalii	
32	Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	
33	Afisi ya Rais Katiba na Sheria	
34	kamisheni ya Utalii	
35	Mkurungenzi wa Mashtaka	
36	Wizara ya Katiba na Sheria	
37	Mkoa wa Mjini Magharibi	
38	Mkoa wa Kusini (U)	
39	Mkoa wa Kaskazini (U)	
40	Mkoa wa Kusini(P)	
41	Mkoa wa Kaskazini(P)	
42	Wizara ya Habari Utamaduni,Utalii na Michezo	
43	Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	
44	Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora	
	JUMLA	
	Mfuko Mkuu wa Serikali	

kiambatisho Nam.vii

MALIPO MENGINEYO NA RUZUKU JULAI HAD

FUNGU	WIZARA/TAASISI	
5	**ofisi ya makamo wa pili wa rais**	
6	**ofisi wa makamo wa kwanza wa raisi**	
7	Ofisi ya Rais Uhusiano	
8	Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi	
9	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ	
10	Ofisi ya Rais Ikulu	
11	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar	
12	Tume ya Ukimwi	
13	ofisi ya waziri kiongozi	
14	Mahkama Kuu Zanzibar	
15	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar	
16	Baraza la Wawakilishi	
17	Jeshi la Kujenga Uchumi	
18	Chuo Cha Mafunzo	
19	Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo	
20	Wizara ya Kilimo na Maliasili	
21	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	
22	Wizara ya Mifugo na Uvuvi	
23	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	
24	Wizara ya Afya	
25	Wizara ya Maji ,Ujenzi, Ardhi na Nishati	
26	Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi	
27	Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	
28	Wizara Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto	
29	Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo	
30	Tume ya Uchaguzi	
31	Kamisheni ya Utalii	

32	Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	
33	Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Sheria	
34	Kikosi cha Volantia	
35	Mkurungenzi wa Mashtaka	
36	Katiba na sheria	
37	Mkoa wa Mjini Magharibi	
38	Mkoa wa Kusini (U)	
39	Mkoa wa Kaskazini (U)	
40	Mkoa wa Kusini(P)	
41	Mkoa wa Kaskazini(P)	
42	Wizara ya Habari, Utalii na Michezo	
43	Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	
44	Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora	
	JUMLA KUU	

kiambatisho Nam.viii

MCHANGO WA SERIKALI KATIKA MIRA

CHA JULAI 2010 HADI JUNI 2011 **"0**

FUNGU	WIZARA/TAASISI	MA
5	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais	
6	Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais	
7	Ofisi ya Rais Uhusiano	
8	Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi	
9	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ	
10	Ofisi ya Rais Ikulu	
11	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar	
12	Tume ya Ukimwi	
13	Afisi ya Waziri kiongozi	
14	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	
15	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar	
16	Baraza la Wawakilishi	
17	Jeshi la Kujenga Uchumi	
18	Chuo Cha Mafunzo	
19	Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo	
20	Wizara ya Kilimo, Maliasili	
21	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	
22	Wizara ya Mifugo na Uvuvi	
23	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	
24	Wizara ya Afya	
25	Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati	
26	Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano	
27	Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika	
28	Wizara Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto	
29	Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo	
30	Tume ya Uchaguzi	
31	Kamisheni ya Utalii	
32	Kikosi cha Zimamoto na Uokozi	

34	Kikosi cha Volantia	
35	Mkurungenzi wa Mashtaka	
36	Wizara ya Katiba na Sheria	
37	Mkoa wa Mjini Magharibi	
38	Mkoa wa Kusini (U)	
39	Mkoa wa Kaskazini (U)	
40	Mkoa wa Kusini(P)	
41	Mkoa wa Kaskazini(P)	
42	Wizara ya Habari Utamaduni,Utalii na Michezo	
43	Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	
44	Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora	
	JUMLA KUU	3

Kiambatisho Nam
ix

MUHTASARI WA USAJILI WA WANAFUNZI ZIFA KUANZIA 2006/0
2010/2011

MWAKA	CHETI	STASHAHADA YA (1)	SHAHADA YA KWANZA	STASHAHADA YA JUU	NTA LEVEL 4	NTA LEVEL 5 (ICT)	I
2006/07	73	88	51	48			
2007/08	134	97	60	39			
2008/09					134		
2009/10					154	59	
2010/2011	251	483	135	9			

kiambatisho Nam x

MAPATO YATOKANAYO NA ADA ZA MASOMO

2006/2007 – 2010/2011 (TZS MILIONI)

MWAKA	ADA ZA MASOMO	ADA NYENGINEZO
2006/07	244.846	46.896
2007/08	315.602	25.149
200809	220.347	50.603
2009/10	566.876	163.476
2010/2011	546.94	112.814
Jumla	**1,894.61**	**398.94**

kiambatisho Nam xi

USAJILI WA WAAJIRI NA WAAJIRIWA ZSSF 20

USAJILI WA WAAJIRI NA WAAJIRIWA ZSSF 2005/06

WAAJIRI				
TAASISI	**2006/07**	**2007/08**	**2008/09**	**2**
SERIKALI	71	71	71	
MASHIRIKA	20	20	20	
BINAFSI	525	635	683	
JUMLA	**616**	**726**	**774**	
WAAJIRIWA				
SERIKALI	31,162	32,000	31,931	
MASHIRIKA	2,678	2,570	2,585	
BINAFSI	16,065	19,796	20,715	
JUMLA	**49,905**	**54,366**	**55,231**	

kiambatisho Nam xii

MWENENDO WA ULIPAJI WA MAFAO – ZSSF 2006/07 – 2010/11 (TZS M

AINA YA MAFAO	**2006/07**	**2007/08**	**2008/09**
KIINUA MGONGO	976.89	929.7	1,436.75
PENCHENI	181.37	242.84	385.84
URITHI	27.11	193.14	284.45
ULEMAVU	193.83	40.38	45.03
JUMLA	**1,379.20**	**1,406.06**	**2,125.06**

kiambatisho Nam xiii

UKUSANYAJI WA MICHANGO –ZSSF -2006/2007-2010/2011(TZS MILIONI)

TAASISI	**2006/07**	**2007/08**	**2**
SERIKALI	3,602.55	5,281.69	6,
MASHIRIKA	607.79	687.13	
SEKTA BINAFSI	2,039.32	2,682.20	3,
JUMLA	**6,249.67**	**8,597.02**	**10,**

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeungwa mkono na kwamba sasa iko tayari kwa mjadala. Kabla ya mjadala naomba niseme maneno mawili na baadae tuwatambulishe wageni wetu waliofika leo hivi jioni.

Waheshiwa Wajumbe, nilikuwa sifahamu kama kumbe humu ukumbini mkiwa kidogo kumbe baridi huwa inazidi. Sasa nilipoingia nimekuta kuna wajumbe wangu kidogo sana, baridi kiasi cha kunitia hoja ilikuwa inaingia. Nikaangalia hapa na pale nikamuona na msaidizi wangu mkuu wa mambo ya dua, Maulani Abdalla Juma na yeye anatoka. Nikasema sasa hata wa kusaidia kuomba dua humu ndani hayupo. Kumbe alikwenda kusoma dua nje kule. Lakini imesaidia

sana dua hiyo pamoja na wengine waliokuweko huko kuitikia Amin, baadae nikawaona wajumbe wanaingia.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa kunipa mashirikiano makubwa sana ya kuendesha kikao hiki. Wageni wetu kwa jioni ya leo, amehudhuria Mhe. Abdalla Ali Hassan Mwinyi, Mbunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki na amefuatana na Mr. Methiew Kella, pamoja na Bi Lillet Tillahun. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wageni wetu tunawakaribisha sana katika shughuli zetu jioni ya leo na tumefurahi kwamba mmekuja kushiriki katika bajeti hivi jioni. *You're most welcome*. Kwa kuwa hoja imeungwa mkono, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo. *(Makofi).*

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO JUU YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2011/2012

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo (Mhe. Salmin Awadh Salmin): Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu, Muumba wa kila kitu kwa kutujaalia sote uzima na afya kwa siku hii ya leo. Aidha, nitumie nafasi hii kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha , Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa kuteuliwa kuwa waziri wa wizara hii, bila ya shaka sote tunaufahamu utendaji wake. *(Makofi)*

Aidha pamoja na wasaidizi wake wote wanaomsaidia katika kutimiza majukumu yao waliokabidhiwa wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo mbali mbali vya ofisi hii. Juhudi zao zinazoonekana na hatuna budi kuwapongeza sana.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii pia, kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ushauri mzuri kwa serikali wakati kamati hii ilipofanya kazi zake.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kuwatambua kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti,
Mhe. Abdalla Mohamed Ali - Makamu Mwenyekiti,
Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mjumbe,
Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe,
Mhe Mahmoud Muhammed Mussa - Mjumbe,
Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe,
Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe,
Ndg. Amour Moh'd Amour - Katibu na
Ndg. Asha Said Mohamed - Katibu

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina majukumu ya Kitaifa na Kisekta. Majukumu hayo yanaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010/2015. Miongozo mbali mbali ya Baraza la Wawakilishi, ikiambatana na Katiba ya Nchi, Sheria za Kodi, Fedha, Manunuzi na Uwekezaji nchini.

Mhe. Spika, naomba nianzie mchango wangu kwa kuyalenga maeneo ya Mipango na Uchumi, Shughuli za Fedha na huduma za Uhasibu Serikalini, Usimamizi wa Mapato, Usimamizi na Utunzaji wa Mali za Serikali, Maendeleo ya Sekta ya Fedha na huduma za Utawala, pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

Mipango na Uchumi:

Mhe. Spika, Mipango na Uchumi ni suala la msingi kwa maendeleo ya nchi. Idara ya Mipango ya Kitaifa, Sera za Kisekta na Kupunguza umasikini ina jukumu hilo la kuratibu mipango hiyo. Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, idara imepanga kusimamia shughuli za Tume ya Mipango, Kukamilisha Mapitio ya Dira 2020, pamoja na utekelezaji wa *MKUZA* II.

Aidha idara imepangiwa kutekeleza jumla ya *Programs* nne na miradi mine kwa mwaka ujao. Maeneo hayo ni muhimu kutekelezwa kwa wakati kwani itasaidia kupunguza matatizo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wetu, hivyo kamati inashauri utaratibu uwe wa kujituma na kujikubalisha kikweli kweli na uwe wa kudumu.

Mhe. Spika, katika kufuatilia kwa makini mipango na uchumi wa nchi hii, Idara ya Ukuzaji Uchumi ina jukumu la kufuatilia mwenendo wa uchumi wa nchi. Kutokana na matatizo ya mfumko wa bei ambayo yanajitokeza mara kwa mara; idara itaanza kutumia mfumo wake wa ukadiriaji wa ukuaji wa uchumi wa *MACMOD*, ambao umo kuandaliwa kwa ajili ya kuwapa habari wananchi

wetu juu ya masuala tofauti ya mwenendo wa uchumi na hatimaye kuwapa ushauri unaofaa. Hiyo ni hatua nzuri na kamati inapongeza juhudi hizo.

Mhe. Spika, katika eneo hilo hilo la mipango na uchumi, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi wakishirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali wamekamilisha utafiti wa hali ya Utumishi Serikalini. Hii ni hatua muhimu kwani utafiti huo utasaidia katika kuandaa Sera na Miundo ya Utumishi ya Kada mbali mbali.

Halkadhalika wafanyakazi wanajenga matumaini makubwa kuona kwamba hata kipato chao cha mwezi nacho kimefanyiwa utafiti, ambao utawezesha kujua ni mahitaji gani halisi waliyonayo ukilinganisha na vipato vyao, hivyo serikali kwa kuoanisha mapato yake halisi, itajua viwango wanavyostahili kulipwa. Kamati ingependa kusisitiza sana tafiti hizi ziwe zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo ili tija ipatikane.

Mhe. Spika, suala la kuwa na Sensa katika nchi ni muhimu sana, kwani matokeo yake ndiyo yanayotoa mwelekeo na vigezo thabiti vinavyoonesha mahitaji halisi, hayo ndiyo yatakayowezesha matumizi bora ya raslimali za taifa na mgawanyo wake.

Hivyo, katika kuendeleza zoezi hili ni vyema serikali ikatoa elimu ya kutosha kwa wananchi, ili wakati wa kutoa taarifa zinazokusanywa wazitoe kwa uhakika na ukweli, kwani kutokusema ukweli wakati wa kujibu maswali ya wadadisi taarifa zao hazitasaidia madhumuni yaliyokusudiwa.

Shughuli za Fedha na Huduma za Uhasibu Serikalini:

Mhe. Spika, katika kusimamia shughuli za fedha na huduma za uhasibu serikalini, Idara ya Bajeti na Idara ya Mhasibu Mkuu Serikalini zinahusika na jambo hili. Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Bajeti imepanga kuzidi kuimarisha Kitengo chake cha *Pay Roll*, ili kutoa taarifa sahihi za mishahara nchini.

Hili ni jambo zuri kwani itapelekea kulipwa mishahara kwa wafanyakazi wale tu ambao wanastahiki kulipwa. Hivyo kamati inawaomba watendaji wawe na mashirikiano ya karibu katika kufikia lengo hili, ili tuepukane na wafanyakazi hewa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. Miongoni mwa mambo mengine, itaendelea na jukumu lake la kudhibiti mapato na matumizi ya serikali kwa kuhakikisha kwamba Sheria na Kanuni za Fedha zinatumika katika kukusanya mapato na

kugawanya matumizi kwa Idara na Taasisi mbali mbali kwa mjibu wa bajeti. Jambo ambalo litakuwa linatekelezwa na Wahasibu na Wakuu wa Idara na Taasisi hizo. Kwa maana hiyo basi suala la mafunzo kwa maafisa wahasibu ni muhimu sana.

Mhe. Spika, upotevu wa fedha za serikali, unaotokana na uzembe au tamaa kwa wale walokabidhiwa dhamana ya utunzaji wa fedha za serikali ni lazima ushughulikiwe ipasavyo. Ili kupunguza tatizo hili ni vyema mafunzo ya mara kwa mara kwa wahasibu, sambamba na kuangalia maslahi yao yazingatiwe ili kupunguza vishawishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Halkadhalika Vitengo vya Ukaguzi wa ndani navyo viimarishwe, ili katika hatua ya awali visaidie kugundua makosa ya kiutendaji na kuwa washauri wazuri wa matumizi bora ya raslimali za serikali na wakuu wanaosimamia matumizi nao wawe tayari kupokea ushauri wanaopewa. Kamati inaiomba wizara iendeleze mafunzo kwa watendaji hao kila mara kwa kuzingatia umuhimu huo.

Mapato ya Serikali:

Mhe. Spika, katika kukuza uchumi wa nchi, serikali lazima isimamie vyema suala la ukusanyaji mapato yake. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015 imeeleza wazi kuwa, serikali itajenga mazingira yatakayowezesha uchumi wa Zanzibar kufikia kiwango cha ukuaji wa asilimia 10 na mfumuko wa bei kufikia kiwango cha chini cha asilimia 7, na pato la kila mwananchi kuongezeka kutoka shilingi 726,000/= za sasa hadi shilingi 884,000/= ifikapo mwaka 2015.

Lakini pia itaimarisha udhibiti wa mapato na matumizi ya serikali, kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya serikali na kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hii ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Fedha ikiwemo Sheria ya Kodi na kuimarisha miundo mbinu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, ili azma hiyo iweze kufikiwa ni lazima serikali isimame kidete katika kusimamia mapato yaliyopo na kuangalia uwezekano wa kuanzisha vianzio vengine vya mapato. Sote tunafahamu kwamba utaratibu wa matumizi yetu ni kwanza tukusanye halafu ndio tutumie, jambo ambalo linaonesha ni kiasi gani tulivyokuwa maskini. Hivyo, tunahitaji mkazo wa hali ya juu kuhakikisha kwamba kile kidogo tunachokusanya kinadhibitiwa vya kutosha. *(Makofi)*

Usimamizi na Utunzaji wa Mali za Serikali:

Mhe. Spika, katika jukumu la kusimamia na utunzaji wa mali za serikali Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ina wajibu mkubwa wa kuratibu uwekaji wa kumbukumbu kwa kuzitambua mali zote na pale zilipo, thamani yake, aliyekabidhiwa, misingi na sababu za kukabidhiwa kwake na kwa zile zinazoondoshwa mikononi mwa serikali nazo ziwe zinaondoshwa kwa taratibu za kisheria na kanuni zilizopo.

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi wetu kwa kuona mali za serikali zikiuzwa kwa bei poa na wakati mwengine bila ya hata kufata taratibu za kisheria ikiwemo utangazaji wa *tender*. Lazima tukumbuke kwamba mali hizi ni za wananchi ambao ni walipa kodi wa nchi hii, kwa hivyo haipendezi hata kidogo kuwadhulumu mali zao. Madamu tunajua taratibu zipo ni lazima zifuatwe vyenginevyo tutawatoa imani wananchi wetu na kuona kwamba mali hizo kumbe hazina mwenyewe.

Mhe. Spika, suala la ujenzi wa Ofisi za Serikali ni muhimu sana lakini nalo linahitaji umakini mkubwa katika utekelezaji wake. Eneo hili nalo huipelekea serikali kwenye gharama kubwa ya upotevu wa fedha, kwani wakati mwengine sheria hupingwa na wakapewa wajenzi, ambao hawana uwezo kwa sababu ya tamaa ya watu kupata chochote. *(Makofi)*

Matokeo yake ni kutumia fedha nyingi ambapo ujenzi wenyewe haulingani na thamani ya fedha zenyewe. Tuelewe kwamba wizara hii ndio msimamizi wa sheria na taratibu hizo, hivyo ni lazima wajisafishe wenyewe kwanza. Hatutaki kurejea mfano wa jengo la ofisi hii lilioko Pemba, lakini ni vyema liwe fundisho na kuona kwamba ule haukuwa mfano mzuri hata kidogo. Hata hivyo kamati ingependa kufahamu tu ni hatua zipi zilizochukuliwa katika kufanikisha upatikanaji wa jengo jengine, kwani tatizo la mahitaji ya kuwa na jengo la ofisi Pemba bado lingalipo.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar:

Mhe. Spika, tunaelewa fika madhumuni ya kuwepo kwa Mfuko huu, kama ambavyo yalivyoanishwa kwenye Sheria hiyo Nam. 2 ya Mwaka wa 2005. Mfuko huo pamoja na kuwatunzia fedha wanachama wake ambao ni wafanyakazi, lakini pia huwa wanaekeza katika miradi mbali mbali kama ambavyo Mhe. Waziri ametueleza, ili kuwa na faida ya kuwezesha kulipa mafao mazuri na kwa wakati wa Kiinua Mgongo, Pencheni na mengineyo.

Mhe. Spika, miongoni mwa miradi ambayo Mfuko iliyonayo ni nyumba za kupangisha zilizopo Mbweni, Nyumba nyengine ya Maduka na Benki iliyopo Mwanakwerekwe Sokoni pamoja na Viwanja vya Kufurahisha Watoto vya Tibirinzi, Pemba na Kariakoo, Unguja.

Mhe. Spika, Mfuko una malengo ya kujenga nyumba kwa ajili ya wanachama wao kwa mkopo nafuu. Nia hiyo ni nzuri lakini kamati inasisitiza tena kwamba lengo libaki hilo hilo, kwani tunaweza kukusudia walengwa wengine na matokeo yake waliokusudiwa wakakosa na wakapata wengine. Nyumba hizo zisiishie mikononi mwa matajiri na viongozi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeamua kuvitengeneza upya Viwanja vya Kufurahisha Watoto ambavyo viko katika hali mbaya sana. Bila ya shaka gharama hizo zitakuwa ni kubwa mno.

Kamati haina mashaka na uanzishwaji wa miradi mbali mbali, lakini inatoa indhari kwamba upembuzi yakinifu katika kuuingiza Mfuko huu kwenye gharama kubwa tukikumbuka kwamba fedha hizi ndizo tunazozitegemea katika kufanya malipo kwa wanachama wake wanaostaafu kwenye utumishi. Hofu yetu ni kwamba tusijekufika siku, mafao ya wanachama yakacheleweshwa na kutolewa kwa foleni ya muda mrefu. Hatutaki kurejea tena nyuma tulikotoka.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo huo ni vyema Mfuko ukawa na Takwimu ya kujua kwa kila mwaka unaofuata ni wanachama wangapi watakaostaafu na hivyo kujua ni matumizi gani yatahitajika. Kama utaratibu huo haupo basi ni vyema ukaandaliwa na kuwa wazi, ukijulikana na kila mdau.

Aidha ni vyema kila mara Mfuko uwe na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa kuangalia mwenendo mzima wa shughuli zake na kuona sheria zilizopo bado zinaendana na hali halisi ya dhana ya Mifuko ya aina hii. Tuendelee kujifunza kutoka kwa wengine. *(Makofi)*

Benki ya watu wa Zanzibar (*PBZ*):

Mhe. Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hisa zake zote, inatekeleza majukumu yake kama zilivyo benki nyengine katika kuhifadhi, kupokea na kuziendeleza dhamana kwa wateja wake.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza sana benki hiyo kwa kuweza kujiimarisha sana katika ushindani wa biashara hii. Imeweza kufungua matawi yake mengine mawili lile la Dar-es-Salaam na jengine lile Tawi kwa ajili ya Wateja wakubwa liliopo Mlandege, Mjini Unguja. Aidha uimarishaji wa jengo lao katika Tawi la Chakechake, Pemba. Juhudi hizi zinaonesha ni kwa namna gani benki hiyo inavyokusudia kufikia malengo yake ya kuongeza ufanisi.

Mhe. Spika, hivi karibuni serikali imetoa agizo kwa watumishi wake kuwa na utamaduni wa kupokea mishahara yao benki na mwelekeo wake ni kuwa wengi

wa watumishi hao wataitumia Benki ya Wananchi wa Zanzibar. Hii itakuwa ni changamoto kubwa wakati wa zoezi hili litakapokamilika, kwani idadi ya wateja kwa benki hiyo itaongezeka na watakuwa ni wateja wataohitaji huduma kwa wingi hasa mwishoni kwa kila mwezi.

Mhe. Spika, changamoto hizo zitakuwa katika maeneo mawili. Kwanza ni umbali wa kupatikana huduma hizo hasa kwa wafanyakazi walioko Pemba, kwani tawi linalotegemewa kutoa huduma hizo lipo Chakechake wakati watumishi wapo maeneo ya Wilaya zote za Pemba. Halikadhalika hili pia litawapata na watumishi wa Unguja ambao wapo maeneo ya vijijini.

Mhe. Spika, eneo la pili linahusiana na wingi wa wateja watakaokuwepo kwa wakati mmoja ukilinganishwa na watoa huduma wa benki waliyopo. Aidha huduma ya kutolea pesa (*ATM*) nazo ni chache , na uzoefu uliyopo kwa hizo zilizopo ni kuwa zimekuwa na maharibiko ya mara kwa mara kiasi cha watumiaji kuanza kutoziamini sana.

Mhe. Spika, kamati inashauri kwamba ili zoezi hili la upokeaji mishahara benki lifanikiwe na watumishi wengi kuichagua benki yetu hii, basi mambo yafuatayo ni vyema yakafanyika:-

1. Kila mwisho wa mwezi makarani wa kutoa huduma wawe wengi wa kutosha kuwahudumia wateja,
2. Mashine za kutolea pesa (*ATM*) ziongezwe hadi vijijini na ziwe zinaangaliwa kila mara, ili kuondoa yale maharibiko yanayotokea na
3. Benki ifikirie tena uwezekano wa kuongeza idadi ya matawi yake.

Shirika la Bima:

Mhe. Spika, Huduma za Bima ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na hifadhi ya jamii. Kwa kulifahamu hilo Shirika la Bima la Zanzibar linahakikisha kuwa linaendelea kutoa huduma zake kwa ufanisi na kwa dhamira hiyo limeanzisha mradi rasmi wa ujenzi wa Makao Makuu yake hapo Maisara, kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kiutawala na uekezaji, ambao utahusisha ukodishwaji wa shughuli nyengine za kibenki na kiofisi.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuliimarisha shirika, juhudi zake zinalenga katika ukuzaji wa mitaji na kuimarisha wataalamu wa kufanya mageuzi ya huduma zake, ili kukabiliana na ushindani wa kibiashara uliopo. Kwa maana hiyo, shirika linakamilisha utafiti juu ya uwezekano wa kuanzisha huduma za bima zinazoendana na maadili ya kiislamu (*Takaful*). Hiyo itakuwa ni hatua

muhimu ya kuongeza idadi ya wateja katika shirika hilo na kamati yetu inazipongeza jitihada hizo. *(Makofi)*

Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Zanzibar:

Mhe. Spika, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi imepewa jukumu kubwa la kuwa kichocheo cha uimarishaji wa uchumi wetu, kuongeza kipato kwa wananchi wetu na kuitekeleza kivitendo ile dhana ya upunguzaji wa umasikini. Majukumu hayo ni katika kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuweza kuwekeza nchini.

Ili kutimiza azma hiyo mamlaka ni vyema ikawa na miongozo inayoeleweka ikiainisha maeneo na aina ya uwekezaji unaohotajika. Utangazaji wa miongozo hiyo na namna ambavyo Muekezaji anavyohudumiwa bila ya kusumbuliwa na baadhi ya mambo yanayoleta mvuto kwa watu wanaotaka kuekeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati hii imekuwa mara kwa mara ikisisitiza juu ya utekelezaji wa dhana ya *One Stop Centre*, ili kuwe na maamuzi ya uhakika nay a muda mfupi. Bado suala hili halijapata ufanisi unaostahiki kwani washiriki wake mara nyingi huwa ni maafisa wasio na maamuzi ya haraka na hivyo ile nenda rudi inabaki pale pale, ambayo ni kinyume na dhana hii tunayoikusudia ya *One stop Centre.*

Mhe. Spika, kamati inashauri kuimarishwa kwa utaratibu huu na hivyo wale washiriki wa Kamati ya Maamuzi wawe ni watu wenye nafasi ya maamuzi kwa niaba ya taasisi zao. Lengo letu ni kuondoa haya yanayotokea juu ya maamuzi yanayotolewa ama kukubaliwa au kukataliwa kwa baadhi ya miradi inayotaka kuekezwa. Malalamiko haya huwa ni ya pande mbili, kwa waekezaji wenyewe na wakati mwengine yanatokana na wananchi maeneo ambayo yanaekezwa.

Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka:

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa kabisa na juhudi zinazofanywa na Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Fedha katika masuala mazima ya uandaaji wa mafunzo, kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo maalum ya muda mfupi yanayohusiana na uhasibu, benki, manunuzi, utafiti na kadhalika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo kubwa ambalo limekuwa likisumbua chuo ni upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya wanachuo. Kamati inaomba suala hili liangaliwe kwa mapana, ili wanafunzi wetu wapate muda mzuri na utulivu wakati wa mafunzo.

Aidha suala la ujenzi wa dakhalia ambao uko katika hatua ya awali liharakishwe, ili lipunguze adha kwa wanafunzi ambao wanapanga katika nyumba binafsi na wengine kuendelea kulala mjini, jambo ambalo haliwapi muda mzuri wa kujisomea masomo yao wakati wa ziada.

Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*):

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar ndio Wakala Mkuu wa Serikali wa uksanyaji wa mapato yanayotokana na kodi za ndani. Kwa msingi huu Bodi hii ni mshauri wa Serikali juu ya Sera inayohusiana na Kodi.

Mhe. Spika, kamati imeridhika na uvukaji wa malengo ya makusanyo ya mwaka uliomalizika wa 2010/2011, ambapo jumla ya shilingi bilioni 101.846/= zilikadiriwa kukusanywa na bodi ilikusanya shilingi bilioni 105.075/= ikiwa ni sawa na asilimia 103. Hiyo ni hatua ya kutia moyo sana.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo, kamati bado inasisitiza kuangalia maeneo mengine ya vyanzo vya kukusanya kodi. Aidha ni vyema kuangalia tena mwenendo wa kukusanya mapato unaofanywa na wizara na idara Mbale mbali za serikali. Kwa mnasaba huo huo utawawezesha kuainisha ni mapato yepi yaendelee kukusanywa na wizara hizo au yahamishwe na yakusanywe na bodi hiyo. Lengo ni kuwa na ufanisi na kuepusha usumbufu kwa walipa kodi.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*):

Mhe. Spika, Mamlaka ya Mapato, Tanzania inakusanya mapato ya kodi yatokanayo na Ushuruwa Forodha, Ushuru wa Biashara na Kodi ya Mapato. Mamlaka nayo kwa upande wa Tawi lake la Zanzibar imevuka malengo yaliyowekwa mwaka wa 2010/2011, ambapo jumla ya shilingi bilioni 69.240/= zilikadiriwa na jumla ya shilingi bilioni 76.357/= zilikusanywa. Kamati yetu imefarijika sana na juhudi hizo, na inashauri ziendelee ili na mwaka huu malengo yaliyowekwa nayo yavukwe.

Mhe. Spika, kamati inaamini kwamba miongoni mwa changamoto inayopunguza mapato ni suala la misamaha mingi ya kodi. Hivyo, kamati inashauri kwamba bado kuwe na busara katika kuangalia umuhimu wa kutoa misamaha hiyo na iwe kwa pale tu ambapo panastahiki kisheria, ili kupunguza kwa kiasi kikubwa kiwango cha idadi ya misamaha hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine linaloonekana katika changamoto hii ni kuwa na mamlaka zaidi ya moja zinazoweza kutoa misamaha ya kodi. Kwa mfano, Mamlaka ya Ukuzaji wa Vitega uchumi pamoja na ile inayohusiana na Umiliki wa Ardhi. Kamati inashauri kwamba mamlaka ya utoaji misamaha iwe ni moja tu. Nayo

iwe ni ya waziri anayeshughulikia na masuala ya kodi na sio venginevyo, taasisi na mamlaka zote nyengine ziombe kwake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati inashauri serikali ifanye marekebisho ya sheria hizo, ili kupunguza utitiri wa watoaji misamaha.

Mhe. Spika, Suala la kukusanya kodi ya Mapato (*Income Tax)* kwa watumishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaoishi Zanzibar ni la busara sana. Kamati inaomba zoezi hilo liendelezwe na lianzie rasmi mwaka huu wa fedha likwa na utaratibu mzuri utakaoleta ufanisi. Kwa hili ni vyema Mhe. Waziri wakati wa kufanya majumuisho yake akatueleza ni makadirio ya kiasi gani ambacho tunaweza kupata kwa makusanyo ya kodi hiyo.

Mfuko wa Barabara:

Mhe. Spika, madhumuni ya kuwepo kwa Mfuko wa Barabara ni hatua muhimu sana ya kuweka utaratibu wa kuaminika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Mfuko huu umefanikiwa kutekeleza azma hii kwani barabara nyingi zimefanyiwa matengenezo kupitia mpango huu. Mwaka huu ulioishia mwezi Juni, 2011 Mfuko umeweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 5.018/= wakati makadirio yalikuwa ni shilingi bilioni 5.451/=, ikiwa ni sawa na asilimia 92 ya malengo.

Mhe. Spika, kamati inaupongeza sana Mfuko huu kwa uamuzi wake wa kujenga ofisi yake. Huo ni uamuzi mzuri na wa busara kwani ofisi wanayoitumia sasa haiwatoshi na haipo katika katika mazingira mazuri. Hata hivyo, kamati yetu inasisitiza kwamba kwa vile mahitaji ya matengenezo ya barabara zetu bado ni makubwa, basi ni vyema serikali ikahakikisha kuwa fedha zinazokusanywa kwa madhumuni hayo zitumike kama zilivyokusudiwa.

Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ – Dar-es-Salaam:

Mhe. Spika, idara hii inaendelea na jukumu lake la kuratibu na kukuza ushirikiano baina ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zile za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na hayo kubwa ambalo kamati inaliangalia kwa uzito wake ni suala la kuratibu ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo baina ya *SMZ* na Ofisi za Balozi za Nje na Mashirika ya Maendelo ya Kimataifa yaliyo na ofisi zake Dar-es-Salaam.

Mhe. Spika, kamati inasisitiza sana kwamba idara hii ni lazima ihakikishe kwamba, zile fedha ambazo hutolewa kisekta kwa Tanzania ikiwa ni kwa mkopo, msaada au ufadhili basi na Zanzibar nayo inapata kupitia sekta za aina

hiyo ambazo Zanzibar zipo, hata kama ni kwa utaratibu huo huo wa mgao wa asilimia 4.5. *(Makofi)*

Tume ya Pamoja ya Fedha:

Mhe. Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya kazi nyingi tangu kuanzishwa kwake, lakini yenyewe haiwezi hata kidogo kujitathmini kutokana na kuwa ripoti ya kazi zake inazozipeleka kwenye serikali zote mbili (SMT na SMZ) haipati majibu ya mapendekezo yao. Jambo ambalo linaendeleza kuonekana kuwa ni moja kati ya kero za muungano.

Mhe. Spika, kamati yetu imekuwa mara nyingi ikikumbushia sana juu ya jambo hilo na leo tena inamuomba Mhe. Waziri aeleze hatma ya ripoti hizo na maendeleo yake yamefikia wapi kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, ambapo wizara imekadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 174.86, kati ya hizo jumla ya shilingi bilioni 80.22 kwa kazi za maendeleo na shilingi bilioni 47.02 ikiwemo ruzuku kwa Taasisi za Ofisi, kwa ajili ya kazi za matumizi ya kawaida.

Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato ya Zanzibar, yanayokadiriwa kufikia jumla ya shilingi bilioni 221.24/=, Misaada ya Kibajeti yenye thamani ya shilingi bilioni 30.28/= na shilingi bilioni 240.96/= ikiwa ni msaada na mikopo kutoka nje kwa ajili ya *Programs* na Miradi ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naunga mkono hoja hiyo na nikiwataka wajumbe wenzangu wamuunge mkono Mhe. Waziri, ili wizara itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika bajeti hii ya Wizra ya Fedha. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza.

Mhe. Spika, kwanza nizungumze kwamba Wizara ya Fedha pamoja na majukumu yake mengi, lakini nataka niunganishe suala la mwanzo kwa

mchango wangu leo na suala ambalo nililizungumza jana kuhusu Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Kwa kweli mara nyingi nilipokuwa nikitoa michango yangu kuhusu idara hii ilikuwa pia nikiuliza idara hii mbali ya kuitwa Idara ya Bajeti ndani Wizara ya Fedha, je ina uhusiano na utaratibu mzima wa bajeti za wizara nyengine? Mhe. Spika, jibu tayari nimeshapewa kwamba hivyo ndivyo ilivyo.

Sasa pamoja na malengo mazuri ambayo ameyataja Mhe. Waziri humo. Lakini inaonekana hii Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, ambayo ingeshughulikia Bajeti ya Serikali pamoja na kutoa miongozo kwa bajeti au vitengo vya bajeti vya wizara nyengine ina kazi kubwa.

Kwanza Mhe. Spika, katika kutoa vipaumbele juu ya bajeti za maeneo mbali mbali ya uzalishaji na huduma. Katika utaalamu ambao kwa kiwango fulani tuliopewa, basi idara hii ingelisimamia utaratibu mzima wa kutoa vipaumbele wakati wa upangaji wa bajeti, bahati mbaya kulikuwa na kipindi tulikuwa tukielezwa wakati bajeti ya serikali inasomwa kila wizara itapewa bajeti asilimia ngapi ya bajeti kuu ya serikali, lakini katika bajeti hii haukuweka ufafanuzi huo. Jana nilipokuwa nikichangia nikasema kwamba kama ingelikuwa tuliwekewa vile viwango basi mchango wetu baadhi yake ingekuwa ni vyengine, mfano Wizara nzima ya Biashara, Viwanda na Masoko bajeti yake ni chini ya bilioni tatu, yaani bilioni 2.6 kama hivyo.

Lakini Idara ya Uendeshaji na Mipango ya Wizara Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo karibu bilioni sita, sasa huu uwiano wa aina hii uko wapi, sasa ndio nikasema kwamba wakati tunapopanga ikiwa hatuweka mizania ya kuangalia vipaumbele tunamalizia kuona kwamba masuala mengi hayapati majibu. Hivyo hivyo ukitizama na Wizara nyegine. Kwa hivyo tunaomba sana katika bajeti inayokuja wakati inaposomwa bajeti ya serikali kuwe na ufafanuzi wa kutosha juu ya mchanganuo wa kila clastar na kila Wizara namna gani itakavyochangiwa katika bajeti ya serikali, ili tokea mwanzo kuona uwiano uliopo na kuweza kuishauri serikali na kuweza kuongoza namna gani ya kuweza kutoa vipaumbele.

Lakini suala la pili katika Idara ya bajeti wenzetu katika ulimwengu sasa hivi wanakwenda katika kuelekea kwenye kuona gharama halisi za uendeshaji wa mambo, kwa hivyo kuweka bajeti iliyokuwa inakusanya mambo ya jumla jumla inakuwa haitoi picha halisi, sasa kuna baadhi ya Wizara ingebidi zitizamwe upya katika utekelezaji au upangaji wa bajeti zao na Idara hii ndio husika.

Mhe. Spika, Nilipokuwa nikichangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilisema kwamba elimu inagawika katika sehemu tatu kubwa, kwanza kuna sehemu ya utawala, halafu kuna sehemu zile zilizo brack kwa mfano Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi, Idara ya sekondari. Sasa wakati tukipata mchanganuo huo ndio tunaweza kuelekeza hasa nchi yetu kwamba sisi katika skuli za msingi tunamsomesha mwanafunzi kwa kiwango hiki, na katika sekondari tunamsomesha kwa kiwango hiki. Kwa hivyo turejekebishe wapi katika felia, sasa ikiwa bajeti haitafsiri mapungufu yetu na mafanikio yetu hapo inaonyesha kwamba tunapata matatizo, lazima katika kupanga bajeti wakati tunapopata matatizo tuweze ujua bajeti zetu zilikwenda kombo wapi hata tukapata matatizo ya aina hii.

Sasa nende katika suala la maslahi ya wastaafu. Mhe. Spika, haitoshi kwa kubadilika mwaka au waziri kila mmoja akaja akasema mimi nampa ishirini na tano yule akasema mimi nampa arubaini, haioshi kabisa, wastaafu wanahitajiwa kupangiwa kiwango ambacho kila atakayekuja atajua kwamba utaratibu ni huu na mimi nijirekebishe vipi. Katika mchango wangu niliotoa bajeti ya mwaka uliopita nilisema hapa kwamba wastaafu wangestahiki kupewa kiwango kile kile cha n ngazi ya chini ya mshahara anaopewa ikiwa ndio ahsante yake, sasa kama hatuna uwezo basi tungesema tunaanza na asilimia hamsini, asilimia sabini na tano lakini ikawa imeshajulikana sio kwamba mtu anakuja kusema tu mimi nampa ishirini na tano elfu, mimi nampa arubaini.

Lakini *base* line iwe ni kitu gani tunavyomtizama malipo yake, sasa tukianza na kwamba atunampa asilimia sabini na tano ya mshahara wa chini atakayekuja atajua sasa uwezo upo tumpe asilimia yote, uwezo upo tumpe mara mbili ya mshahara wa ngazi ya chini. Au kadiri unavyopanda ngazi ya chini na yeye atakuwa anapanda lakini mimi sikubaliani kabisa na hoja kwamba wastaafu wapewe shilingi ishirini na tano elfu mimi sikubaliani nalo, naona bado hatujakuwa na utaratibu. Tukubaliane utaratibu wa namna gani kuwalipa wastaafu, kila mfanyakazi ni mstaafu anayengojea ikiwa mwenyezi Mungu atampa uhaki akafika basi kila mfanyakazi ni mstaafu anayengojea.

Kwa hivyo tuwatizame wafanyakazi wanavyokula dhiki katika kipindi chao cha kazi, kwa nini tusiwaone katika kipindi chao cha kupumzika, kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja atuelezee hukaaje kaaje wakaamua leo ishirini na tano kesho arubaini bila ya kutizama hasa utaratibu ambao hata akija waziri gani ataweza kuangalia mambo ambayo yapo.

Mhe. Spika, moja kati ya majukumu makubwa ya Wizara hii ni kukusanya mapato, katika mapato vile vile kuna kukuza uchumi sasa huu utaratibu wa kukuza uchumi bado haujaonekana na mwelekeo wa Zanzibar, kwa sababu mapato yetu yanaonekana kwenda katika mtiririko ule ule tu wa mazoea, lakini

hakuna kitu kipya ambacho kimeibuliwa ambacho kitazidisha mapato. Ndio kama nilivyosema wizaa kama ya biashara na viwanda ilikuwa ni sehemu ambayo ingetoa mapato zaidi kwa nchi kwa hivyo tungeitegemea Wizara ya Fedha basi ingeliitizama ikaiwekea mikakati ili kukuza uchumi wa Zanzibar tunalikabidhi jukumu wizara hili na hili na tunaipa hichi na hichi ili kutimiza malengo hayo. Kwenye kwa mazoea hakutotufikisha mbali lazima tuende kwa mikakati mimi naamini sana uwezo alioanao Mhe. Waziri, na ile ari ya kufanya kazi na kuleta maendeleo nilimuona nayo ndani ya uso lakini ile inataka kutafsirira ndani yah ii bajeti ambayo tunaipanga.

Hapa Ofisi yetu ya mara hii inaitwa Uchumi na Mipango ya Mande sasa lazima kionekane basi kile kinachosimamiwa cha maendeleo kionekane, wataalam weanasema Zanzibar kuna mapato mengi ambayo yamebezwa ndani ya Taasisi za Muungano na Nje ya taasisi za Muungano. Kwa hivyo hebu tukae upya tuitizame kweli sisi hatuna uwezo wa kuzidisha pato la mtu kwa mwaka, zaidi ya hivi hapa tulipofika, mara nyingi ninapozungumza kuhusu *DGP* na mara moja nashukuru nilijibiwa kwamba kuna na *GNP*. Hebu tuangalie huu uwezo wa kuongeza *DGP* na kuitizama *DGP katika GNP* je haitokuwa na tofauti ya namna gani mipango yetu tunavyoipanga.

Sisi tunapata fedha nyingi na misaada mingi kuokana na *DIASPORA* ambao wako nje, sasa suala langu liko kwa Wizara ya Fedha katika kupanga mipango yetu ya maendeleo sekta hii inayoshughulikia kitengo cha maendeleo kinatoa miongozo gani kwa nchi katika kulishughulikia suala zima la *DIASPORA.* Kwa sababu Wizara ya Fedha ndio iliyokabidhiwa dira yote ya kuona kwamba mambo ya kimapato yanakwenda kama yalivyopangwa.

Mhe. Spika, kunakuwa na migongano kidogo wakati wa kusoma bajeti za maendeleo, baadhi ya vitabu haionyeshwi kwamba bajeti ya maendeleo ni kiasi fulani utakuja kuiona kwenye kitabu kikubwa, sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri katika kitabu hiki anachosoma Mhe. Waziri kama bajeti ya maendeleo inayochangiwa na wahisani haikuoneshwa, hakuna athari katika kutumia bajeti ile au tunakwenda kwa mazoea. Kwa sababu wakati mwingi inayosomwa ni ile ambayo ni mchango wa serikali, lakini ukiuliza unaambiwa hizi ziko Wizara ya Fedha basi sijui hizi zilizotajwa na Wizara ya Fedha bilioni 47.62 za maendeleo ni kwa Wizara ya Fedha tu au kwa ajili ya wizara zote ambazo bajeti yao ya maendeleo zilizochangiwa na wahisani hawakuzitaja hili ndio suala langu. Kama sivo hivyo ni vipi njia sahihi ya tunakoelekea wazitaje wao au waendelee kuzinyamazia kama ambavyo inafanyika.

Mhe. Spika, *JFC* kwa sababu ni suluhisho la namna gani Zanzibar itapata mapato yake ndani ya Muungano na kufanya mgao, hii kuchukua muda mrefu hatuoni kwamba ndio kujikosesha kwa sababu walalamikaji ndio sie, upande wa pili wa muungano hawalalamiki wao. Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze hii kucherewa kwa taarifa hizi hakutuathiri katika hali ya uchumi wetu na ofisi yake sasa itachukua hatua gani za dharura kulishughulikia hili jambo.

Mhe. Spika, usimamizi wa mali za serikali hapa pana kizungumkuti kidogo, wakati mwingi katika wizara hii au nyengine inavyotajwa hutajwa hati miliki, lakini katika bajeti zilizopita katika michango mbali mbali ambayo tuliitoa tulisema kwamba wizara yenyewe hii ya Fedha inahusika moja kwa moja na kuona kwamba mali za serikali zinasimamiwa. Sasa ili kusimamia mali za serikali inabidi ufanye jitihada ya kuweza kupata hati miliki, sasa namuuliza Mhe. Waziri katika hii *seeling* inayofanywa katika Mawizara tofauti kiwango gani kilichowekwa kuhakikisha kwamba Wizara inashughulikia haki miliki na gedha zile wanazitumia kweli katika kufuatilia hakimiliki za maeneo yao. Kwa sababu mara nyingi unapowauliza Mawaziri wanasema wanafuatilia lakini katika michango yetu ya bajeti zilizopita tulisema kwamba wizara hii ihakikishe kwamba ama wenyewe inabeba jukumu hili, au kunakuwa na kifungu maalum cha wizara kushughulikia hati miliki. Je, kiko kifungu hicho cha Wizara kushughulikia hati miliki na kama kipo kinatumiwa ipasavyo ili kuona kwamba mali za serikali zinatunzwa.

Mimi nasema sana kwamba wakati mwengine tunatumia maneno yaani kwa kuyafitiliza, mali ya serikali ni sawa sawa na mali ya umma ikipotea mali ya serikali ina maana kila mtu amepoteza, sasa ikiwa mali za serikali hazitunzwi haziwekwi katika rekodi wako watu binafsi watazitumia vibaya, kwa hivyo watawachukulia mali zao zote wale watu wengine.

Mhe. Spika, sasa twende katika jengo la Wizara ya Fedha lililoko Pemba hebu Mhe. Waziri twambie ukisema kwamba umempelekea madai mzabuni na kandarasi lile jengo halifai tena, halafu moja katika madhumuni yako ulisema kwamba unataka kujenga jengo la ofisi Pemba ni lile lile au litang'olewa kwanza, saiti ndio ile ile au umepata saiti nyengine lile linasubiri kesi. Maana yake suala la kufeli kwa jengo la Wizara ya Fedha Pemba kumeleta athari kubwa kwanza Wizara husika ni wizara mama, katika kufeli ujenzi wa jengo lile wizara husika ni wizara mama lakini pia kulikuwa na tatizo kubwa la ofisi kule Pemba na *solution* yake lilikuwa lipatikane jengo hili ambalo halikupatikana athari nyengine ya pili, athari ya tatu kuna ukosefu mkubwa wa viwanja. Sasa kufeli kwa jengo lile kumepelekea kuwa gharama kuliondosha, sasa hebu tueleze kinaga ubaga wahusika ni hawa makandarasi tu au na wengine wamo ambao wangepaswa kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, jengo lile kwa kweli ni aibu kabisa kabisa lakini hawa ofisi ya Pemba ambao sasa hivi kuna mitandao mingi inayotumika katika utaratibu wa kifedha, matamimeloji makubwa makubwa yanatumika katika uhaulishaji wa fedha. Nauliza je katika kipindi hiki ofisi wanayotumia inatosheleza haja au ofisi yako itakodi jengo jengine wakati jengo hili linangojewa, kwa sababu najua kwamba kuna majengo ya watu binafsi ambayo yapo na yanaweza kukodiwa.

Mwisho Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo kwa kuweza kulipa mishahara ya wafanyakazi kwa wakati, pili kulipa mafao ya wastaafu kwa wakati, lakini la tatu ni kuweza kutoa kauli kwamba masuala ya misamaha iliyokuwa haina mipango ya kodi inashughulikiwa kikamilifu, tunategemea Mhe. Waziri kwamba utendaji wa wizara hii utaendelea kupata ufanisi siku hadi siku wakijua uhalisia kwamba madhumuni makubwa ni kuwatumikia wananchi. Mahisabu haya makubwa yanaonyesha kwamba Wizara ya Fedha wanatononeshwa sana kwa hivyo ilivyokuwa inatononeshwa hakuna sababu ya kuwa kwa nini wasiwatumikie wananchi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja naomba nifikie hapa *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nitoe hoja na unifikirie kama Spika, kwa sababu hotuba hii ya Wizara ya Fedha ni hotuba nyeti sana na kwa kweli wajumbe wako tunaweza kukosa fursa ya kuichangia vizuri kwa sababu ya muda uliotolewa mfupi kwa huduba hii na kwa sababu kidogo tuna hali ambayo sio nzuri kwenye vichwa vyetu. Tunaomba utuahirishie Baraza hili hadi kesho ili kujipanga kujadili hotuba hii tumsaidie Mkhe. Waziri kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Hivi ndio mnanambia mmekubali na Mhe. Salim Abdalla Hamad unasema hay ohayo. Sasa Waheshimiwa wajumbe pale kabla nilisema humu ndani ukumbini tulikuwa wachache na baadae waheshimiwa wajumbe mliingia ili kuja kushiriki katika shughuli zetu hizi na nimefurahi kunipa mashirikiano hayo, sasa wengi wakati wa hotuba hii inawasilishwa walikuwa wapo nje pale wananong'ona hapa na pale na hatimae wajumbe wakaingia wakati Mhe. Waziri alikuwa yuko zaidi ya nusu ya hotuba na wakati mwengine mnaelewa kwamba wajumbe pale waziri anapotoa ile hotuba ndipo wanamaki sehemu hii nichangie, ambapo kwa bahati mbaya kwa sababu ambazo hazizuiliki wengi hawakusikia.

Sasa sitaki nimwambie Mhe. Waziri aisome tena aa lakini basi tukubaliane kwamba wajumbe mkajisomee, muweke *point* vizuri na kesho penye majaaliwa basi tuweze kuja kuchangia, lakini kwa kuwa muda upo na shughuli ipo hii basi tuone kama wajumbe wote tunakubaliana na hayo makofi niliyasikia. Lakini sasa hebu tuliamue vile waheshimiwa wajumbe hoja ilitolewa na Mhe. hija tuiamuwe basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Baadhi ya Mawaziri wanakataa wanataka shughuli hii ishe, lakini itakwisha kesho.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 1.22 usiku Baraza liliahirishwa Mpaka tarehe 28/7/2011 Saa 3.00 Asubuhi)